Jumanne Juni 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579947

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Wema aswekwa rumande kukaidi amri ya mahakama

UKURASA 3




UKURASA 13

# Bajeti mbadala upinzani tril. 29/-

**WATAJA** vipaumbele vitano, kilimo yatengewa asilimia 20, wapendekeza kushusha malipo deni la taifa...*Endelea ukurasa wa 2*



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile (kushoto), akiangaliwa moja katika mashine 62 za kusafisha damu baada ya kukabidhiwa msaada na Naibu Balozi wa Saudi Arabia nchini, Ahmed Bin Saleh Alghamdi (wa pili kulia), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mratibu wa Magonjwa yasiyoambukiza wa wizara hiyo, Dk. Shadrack Buswelu. Habari Uk. 3.
**PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**MADEREVA WA MALORI WAONDOLEWA VIKWAZO**
SERIKALI imeondoa vikwazo vyote vilivyokuwa vinaleta usumbufu kuanzia eneo la bandarini, mizani hadi mipakani...

**UKURASA WA 25**

**MWENYE DALILI ZA EBOLA AONEKANA NCHINI KENYA**
WAKATI mtoto wa miaka mitano akifariki Uganda kwa ugonjwa wa ebola, madaktari katika Hospitali ya Kericho nchini Kenya, wanamchunguza mwanamke ambaye...

**UKURASA WA 26**

**MWANAFUNZI CHUO KIKUU AUAWA KWA KISU DAR**
MWANAFUNZI wa mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, Anifa Simpolianusy, amedaiwa kuuawa na wezi kwa kuchomwa kisu kifuani akiwa karibu na maeneo...

# Msekwa afunguka kuhusu Muungano



UKURASA 2

# Waibua mazito mkutano wa NEC

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAJICHELEWESHA UWANJA KWA MAKONDA UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Viongozi wa dini watoa angalizo maofisa NEC

**Na Enock Charles**

VIONGOZI wa dini nchini wameitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutatua changamoto zinazojitokeza wakati wa mchakato wa uchaguzi, yakiwamo malalamiko ya wagombea kutowakuta ofisini wakurugenzi wa uchaguzi wakati wa kurejesha fomu.

Akizungumza katika mkutano wa NEC na viongozi hao jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Mch. Osward Mlay, aliitaka tume hiyo kuhakikisha taratibu za uchaguzi zinazingatiwa na wagombea wote wanapata taarifa sahihi za mkurugenzi anayekuwapo wakati wote wa uchaguzi ili kuondoa malalamiko.

Mkutano huo ni mwendelezo wa mikakati ya NEC kupata mawazo ya wadau wakati ikijipanga kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

"Kuhamishwa kwa wakurugenzi kuelekea watu kupokewa fomu za kugombea, pengine kwa kutokujua, kunaweza kuleta malalamiko kwa wagombea maana unakuta aliyekuwapo ndiye anayesubiriwa na wanamfahamu vizuri, sasa unakuta hayupo ofisini, halafu baadaye mgombea anaambiwa hana sifa," Mlay alisema.

Katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam nchini, Sheikh Mussa Kundecha, aliitaka tume kutoa kauli kuhusu viongozi wa serikali wanaotoa kauli zinazohusiana na uchaguzi zikiwa na ishara ya kusababisha uvunjifu wa amani nchini.

"Sasa kiongozi wa serikali anasema 'mimi mheshimiwa haya majimbo yote nitakupa' au, 'nimekuteua mkurugenzi halafu umtangaze mpinzani ameshinda', haya ndiyo chanzo cha vurugu," Sheikh Kundecha alisema.

Akijibu hoja za viongozi wa dini kuhusu kauli za viongozi wa serikali zinazodaiwa kuwakwaza wananchi, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, alisema tume hiyo itafuata sheria na taratibu zote za uchaguzi ikiwamo kuundwa kwa kamati ya maadili inayoshughulikia malalamiko ya wagombea. "Wakati wa uchaguzi, pataundwa kamati ya maadili na tunatarajia hayo yataletwa tutaipa madaraka kwa taratibu za kisheria na wanaweza kuwajibishwa kisheria," Jaji Kaijage alisema.

Kuhusu wakurugenzi wa uchaguzi kukimbia ofisi kwa lengo la kuwahujumu baadhi ya wagombea, Jaji Kaijage alisema wakurugenzi hao hawapo juu ya sheria.

Alisema wanaweza kuwajibishwa kisheria, huku akiwataka wanasiasa kufikisha malalamiko yao mahali husika badala ya kukimbilia kwenye vyombo vya habari.

Akitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Athuman Kihamia, alisema katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Buyungu mkoani Kigoma, tume ililazimika kuunda kikosi cha wataalamu kuchunguza malalamiko yaliyotolewa. "Mwenyekiti, sisi tunajitahidi sana, mfano katika uchaguzi mdogo wa Buyungu tulilazimika kuunda kikosi cha wataalamu kuona ukweli wa kilichosemwa kwamba haijabandikwa na mengine, tukakuta mkurugenzi amefuata taratibu zote," alisema.

Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292, vinaitaka tume kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura walau mara mbili baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu kabla ya kuingia katika Uchaguzi Mkuu mwingine.

# Upinzani waja na bajeti kivuli ya tril. 29/-

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imetaja maeneo makuu matano ya vipaumbele katika bajeti yake mbadala ya mwaka 2019/20 ambayo ni zaidi ya Sh. trilioni 29.037, huku ikielekeza asilimia 20 kwenye kilimo.

Bajeti hiyo mbadala ni chini ya ile iliyopendekezwa na serikali ya Sh. trilioni 33.1 ambayo iliwasilishwa bungeni wiki iliyopita na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Wakati bajeti hiyo mbadala ikiwasilishwa jana Bungeni na Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ililazimika kutosoma kwa kuondoa aya 13 kwa maelekezo ya Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson.

Maeneo ya kipaumbele yaliyomo katika bajeti hiyo ni elimu Sh. 4,354,671,500 (asilimia 15), kilimo Sh.5,806,228,742,000 (asilimia 20), viwanda Sh.4,354,671,556,500 (asilimia 15), maji Sh. 2,903,114,371,000 (asilimia 10), afya Sh. 2,903,114,371,000 (asilimia 10) na mengineyo yakichukua asilimia 30 sawa na Sh.8,709,343,113,000.

"Katika bajeti yetu mbadala, badala ya kulipa deni la taifa la Sh. trilioni 10 kama ambavyo bajeti ya serikali inaonyesha, sisi tutalipa Sh. trilioni saba. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika biashara yoyote kuna nafasi ya majadiliano, hivyo tutafanya majadiliano ya kulipa kiasi hicho.

"Kwa upande wa serikali, sura ya bajeti inaonyesha nakisi ni asilimia 2.3 ya pato la taifa sawa na Sh. trilioni 2.976, lakini ukiangalia fedha zote kutoka nje (yaani mikopo na misaada ya kibajeti) ambazo kimsingi ndiyo nakisi yenyewe; ni takribani Sh. trilioni 10 ambayo ni asilimia 30 ya bajeti yote," alisema.

Kutokana na hali hiyo, kambi hiyo imeionya serikali kuacha kukokotoa nakisi ya bajeti

INAENDELEA UK. 8



Mfugaji wa ng'ombe wa maziwa kutoka Halmashauri ya Mji wa Njombe, Restuta Mlelwa, akipita na ng'ombe wake kwenye maonyesho ya kitaifa ya ng'ombe bora wa maziwa, katika viwanja vya Nanenane Nzuguni, jijini Dodoma jana. Ng'ombe huyo, anadaiwa kutoa lita 32 za maziwa kwa siku. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msekwa afunguka kuhusu Muungano

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa zamani wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa, ametaja sababu za kuwapo kwa usiri mkubwa katika mchakato wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Katika kitabu chake cha 'Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar' alichokitoa hivi karibuni, Msekwa anaeleza kuwa usiri huo ulikuwa na lengo la kukwepa hujuma kutoka kwa maadui wa Muungano.

Katika kitabu hicho, Msekwa (84), anaeleza kuwa marais Julius Nyerere na Abeid Karume walikuwa na hofu kwamba endapo lengo lao la kuunganisha nchi hizo mbili lingejulikana mapema, maadui wangepata nafasi ya kufanya hujuma za kukwamisha lengo hilo.

Msekwa, mmoja wa watu watatu waliobeba siri ya Muungano huo (wawili wakiwa wameshafariki dunia - Nyerere na Karume), anabainisha kuwa dalili za hujuma zilijitokeza siku za mwisho wa mchakato, zilipotengenezwa fitina na maneno ya uongo yaliyosambazwa wakati Rais Karume alipokwenda Dar es Salaam kukamilisha mipango ya kutia saini Mkataba wa Muungano.

Anasema gazeti la 'TANU The Nationalist' la wakati huo lilifichua fitina hiyo katika toleo lake la Aprili 22, 1964 kwa kuchapisha kuhusu uvumi uliozagaa kwamba 'Rais Karume na familia yake wamekwenda kuishi Tanganyika'.

"Ilibidi Waziri wa Mambo ya Nje, Oscar Kambona, akanushe uvumi huo kwa kusema ' Rais Karume alifika Dar es Salaam kuzungumza na Rais Nyerere na kwamba mazungumzo yao yalijikita katika kuimarisha urafiki wa nchi hizi mbili pamoja na uhusiano kati ya TANU na Afro-Shirazi Party'.

"Waziri Kambona alinukuliwa na gazeti hilo akiendelea kueleza kusema kwamba 'Rais Karume anaamini katika Umoja wa Afrika, na Zanzibar itafurahi kuona Serikali ya Afrika hatimaye imeundwa, ambayo ndiyo vilevile ndoto ya Tanganyika.

"Lakini, kwa lengo la kutunza siri, Waziri Kambona alificha ukweli kwamba mazungumzo ya marais hao yalihusu kuunganisha Tanganyika na Zanzibar.

"Kwa lengo hilo hilo la kutunza siri, hata siku yenyewe ya Aprili 22, 1964 ambayo Nyerere alikwenda Zanzibar kutia saini yake katika Hati ya Mkataba wa Muungano, bado gazeti la The Nationalist lilieleza kwamba Rais Nyerere alikwenda Zanzibar kwa ziara ya kirafiki na Watu wa Jamhuri ya Zanzibar.

"Liliandika kuwa katika ziara hiyo, Rais Nyerere alionana na Rais Karume ikiwa ni ziara yake ya kwanza Zanzibar tangu Serikali mpya ya Mapinduzi ilipotwaa madaraka.

"Gazeti hilo pia lilinukuu maelezo ya Salim Rashid, aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi, aliyesema 'tumemkaribisha Nyerere kuzuru Zanzibar kwa moyo mkunjufu kwani watu wa nchi zetu hizi mbili wakati wote wamekuwa marafiki na wenye ukarimu mno. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ni jambo zuri kwa viongozi wetu wakuu kukutana mara kwa mara kujadili matatizo yetu yanayofanana. Hii ni ziara ya kwanza ya Nyerere tangu Mapinduzi.

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA




Rais wa Bunge la Watoto, Miriam Chirwa, akizungumza na wabunge wa Bunge hilo, kuhusu hali ya haki za watoto, katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wema aswekwa mahabusu siku 7

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imeamuru msanii wa filamu nchini, Wema Sepetu (30), kupelekwa mahabusu mpaka Juni 24, mwaka huu, itakapotoa uamuzi ama afutiwe au aachiwe kwa dhamana baada ya kushindwa kufika kusikiliza kesi yake.

Mahakama hiyo imeamuru Wema kupelekwa mahabusu jana baada ya mshtakiwa huyo kwenda kujisalimisha na kujieleza kwamba alishindwa kufika mahakamani Juni 11, mwaka huu, kutokana na maradhi ya tumbo.

Wema anayekabiliwa na mashtaka ya kuchapisha video ya ngono katika ukurasa wake wa mtandao wa Instagram, aliamriwa kwenda mahabusu na Hakimu Mkazi Maira Kasonde, anayesikiliza kesi hiyo.

Kabla ya amri hiyo, Wema aliieleza mahakama kwamba Juni 11, ilikuwa siku ya kusikiliza kesi yake, lakini alipofika viunga vya mahakama hiyo alipata maradhi ya tumbo ghafla, hivyo akalazimika kwenda hospitalini.

"Mheshimiwa naomba mahakama yako inisamehe kwa sababu nilikuwa naumwa

INAENDELEA UK.8

# Saudia yasaidia mashine 62 za kusafisha damu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imepokea msaada wa mashine za kusafisha damu 62 kutoka Saudi Arabia ambazo zitasambazwa mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar, ili kuondokana na changamoto ya wagonjwa kusafiri kwenda mikoa minne inayotoa huduma hiyo kwa sasa.

Msaada huo ulitolewa jana na Naibu Balozi wa Saudi Arabia nchini, Ahmed Bin Saleh Alghamdi, na kupokelewa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo uliogharimu Sh. bilioni 1.5, huku mashine moja ikiuzwa Sh. milioni 25, Dk. Ndugulile alisema wagonjwa wamekuwa wakisafiri kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kwenda Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Kilimanjaro kwa ajili ya huduma hiyo.

Alisema msaada huo utasaidia wagonjwa badala ya kutumia muda mrefu kusafiri ili kuifikia mikoa hiyo inayotoa huduma hiyo kwa sasa, watapata kupitia mikoa yao.

"Tunaishukuru Saudi Arabia kwa msaada huu kwa sababu utasaidia katika sekta kutoa huduma kwa wagonjwa wenye uhitaji wa kusafisha damu, kwa sasa tuna vituo 19 ambavyo vinatoa huduma hii nchini, vingi vipo mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

"Kusudio la serikali ni kusogeza huduma hizi mikoani na tumeshaanza kujipanga kwa kuhakikisha tunatoa mafunzo ya wataalamu hao ili huduma ziweze kupatikana," alisema.

Dk. Ndugulile alisema changamoto ya magonjwa yasiyoambukiza ni kubwa kwa sasa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa siku imekuwa ikifanya awamu tatu ya kusafisha damu.

"Tunafanya hivyo kuanzia siku ya Jumatatu hadi Jumamosi na mpaka Jumapili kwa siku za dharura tunaona wagonjwa kati ya 90 hadi 120 kwa siku." alisema.

Mgonjwa wa figo anatakiwa kusafishwa mara mbili hadi mara tatu na Hospitali ya Muhimbili kuna awamu tatu kwa siku za kusafisha damu na zipo mashine 42.

Naye Naibu Balozi wa Saudi Arabia, Alghamdi, alisema nchi yao itaendelea kuisaidia Tanzania siyo tu kwa sekta ya afya na nyinginezo muhimu kama ya elimu.

# WMA yaanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

WAKALA wa Vipimo (WMA) umeanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la kuitaka kuhakiki na kusimamia mizani yote itakayotumika kupima mazao ya pamba na ufuta nchini.

Katika utekelezaji huo, WMA pia tayari imetekeleza kwa vitendo wa kukagua na kutoa elimu kwa mikoa ya Kanda ya Kusini inayolima ufuta ambayo ni Lindi, Mtwara na Ruvuma.

Mkurugenzi wa Ufundi wa WMA, Stella Kawa, alisema jana kuwa timu ya maofisa wake wanapita kwenye vyama vyote vya msingi kufanya ukaguzi wa kushtukiza, ili kujiridhisha kama ile mizani waliyoihakiki kabla ya msimu kuanza imeendelea kupima kwa usahihi, ili mkulima apate faida inayostahili kwenye mazao yake.

Stella alisema lengo la ukaguzi huo ni kuchochea wakulima kuongeza uzalishaji kwenye kilimo kwa kuwa na uhakika wa kupimiwa mazao yao kwenye mizani iliyo sahihi na kuchochea nia ya serikali ya kuwa na uchumi wa kati wa viwanda.

"Ili kufikia lengo mahsusi la serikali la kuwa na Tanzania ya viwanda kupitia malighafi za kilimo na matokeo yake ajira kwa Watanzania na pato la taifa vitaongezeka na uchumi wa mtu mmoja mmoja kukua na kufikia ule uchumi wa kati.

"Pamoja na mikoa inayolima pamba na ufuta, maofisa wetu wanapita kwenye AMCOS zote (vyama vya msingi) kufanya kaguzi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha mizani yote inayotumika kupima mazao hayo ni sahihi na mkulima anapata kipato kulingana na jasho lake na si vinginevyo.

"Aidha, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wasimamizi wa vituo vya kuuzia ufuta na pamba kuhakikisha mizani haiharibiwi na wajanja wachache kwa maslahi yao binafsi na atakayekamatwa anadhulumu wakulima kupitia mizani atachukuliwa hatua kali za kisheria," alisema Stella.

Kwa mujibu wa Stella, katika baadhi ya AMCOS ambazo zimekaguliwa katika mikoa ya Lindi na Mtwara, mizani 50 kati ya 52 haikuwa na tatizo, huku mmoja ukikutwa ni mbovu na mwingine ulikuwa na kasoro ndogondogo ambazo zilirekebishwa mara moja.

**TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC).**

**INVITATION TO THE TANZANIA CASHEWNUTS FORUM**

On behalf of the Government of the United Republic of Tanzania, The Tanzania Investment Centre is pleased to invite you to the Tanzania Cashew nuts Forum in Mtwara, to be held on July 12 – 13, 2019, under the patronage of His Excellence the President of the United Republic of Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli.

The Forum will take place at the Bank of Tanzania Conference Hall in Mtwara Branch, and aims to attract potential investors from outside Tanzania as well as domestic investors interested in establishing cashew nuts processing projects as well as industrial parks in Tanzania and more specifically in Lindi and Mtwara regions.

Tanzania is among the World's largest producer of Raw Cashew Nuts (RCN), whereby during 2017/18, it realized a total production of RCN of 313,826 Metric Tons – but about 90% of cashew nuts exported in their raw form owing to the country's low processing capacity.

The Program format includes: Presentations from Senior Government Officials, Expert and Practitioner talks that will also include, networking, One-to-one business and development partnership negotiations, exhibition sessions, Business field tours and optional excursions. Delegates will have the opportunity to learn from extraordinary nationally and internationally acknowledged speakers. The Forum will engage business investment institutions operating in the cashew nuts sub-sector - to showcase the following opportunities:

1. Adding value to raw cashew products through processing:
   - Nuts (kernels) into various products
   - Cashew apples into juices and liquors
   - Cashew shells squeezed into saleable liquids
2. Investing into new cashew farming/plantations and provide extension services so as to increase productivity and total tonnage:
   - Opening new, large scale cashews' plantations in Tanzania
   - Provide agronomic extension services to improve cashews productivity from the current 0.3 MT/year to the real potential of 1.0 MT/year
3. Investing into the production and supply of cashews' machinery/equipment/spare parts:
   - Local manufacture of machinery or equipment to process nuts, cashew apples and cashew shells
   - Manufacture of spare parts.
4. Construction of industrial parks and development of cashew processing industrial zones.
5. Investment in other related areas.

The Forum will be an opportunity for international private investors to (i) meet with the highest government authorities; (ii) identify and seize business opportunities; (iii) create partnerships with local economic operators.

We thank you for your interest and we look forward meeting you at the Forum in Mtwara. To confirm your participation, please register your name through http://tic.go.tz/registerOnline.

**ISSUED BY,**
**EXECUTIVE DIRECTOR,**
**TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC).**

215279902

# Madereva wa malori waondolewa vikwazo

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeondoa vikwazo vyote vilivyokuwa vinaleta usumbufu kuanzia eneo la bandarini, mizani hadi mipakani.

Imesema endapo dereva wa lori atafuata taratibu zote za usafirishaji wa mizigo yake ikiwamo kupata vibali, hatakumbana na kikwazo chochote akiwa barabarani.

Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akigawa vyeti kwa madereva wa malori zaidi ya 1,000 waliohitimu mafunzo ya kuwajengea uwezo katika usafirishaji, yaliyotolewa na Shirika la Umoja la Mataifa linaloshughulikia Chakula (WFP).

Mafunzo hayo yaliwawezesha madereva kujua na kufahamu namna ya kutoa mizigo bandarini kwa haraka, kusafirisha kwa njia salama.

Mhandisi Nditiye, alisema kwa sasa hali ya usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini imekuwa nzuri na kwamba madereva wameondolewa vikwazo walivyokuwa wanakabiliana navyo.

"Madereva walikuwa wakitumia muda mwingi bandarini kutoa mizigo, pia wanatumia muda mwingi kusafirisha mzigo njiani, hivyo kwa sasa hayo mambo hakuna tena, dereva akiwa na nyaraka zote atatoa mzigo kwa wakati na atasafiri bila ya bughudha," alisema Nditiye.

Kadhalika, Mhandisi Nditiye aliwataka madereva nchini kufuata sheria na taratibu wakati wanapokuwa barabarani, na kwamba

INAENDELEA UK.8



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Angellah Kairuki, akiagana na baadhi ya wanawake waliofika kwenye kongamono la wanawake wafanyabiashara lililoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# MV Mbeya kumaliza adha usafiri Nyasa

**Na Mary Geofrey,** KYELA

WANANCHI wa mikoa ya Ruvuma na Mbeya wanaoishi kando ya Ziwa Nyasa, wanatarajia kuanza kunufaika na usafiri wa meli ya Mv Mbeya II ambayo ujenzi wake unatarajia kukamilika Agosti, mwaka huu.

Kwa miaka miwili sasa wananchi wa maeneo hayo, hawana usafiri wa uhakika baada ya meli ya MV Songea iliyokuwa ikitoa huduma katika ziwa hilo, kusitisha safari zake tangu mwaka 2017 kutokana na kuwa na hitilafu.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abeid Gallus, alisema ujenzi wa meli hiyo umefika asilimia 82. Alisema ujenzi wa meli hiyo unagharamiwa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa Sh. bilioni 9.1 na ina uwezo wa kupakia mizigo tani 200 na abiria 200 kwa wakati mmoja, hivyo kukamilika kwake itasaidia kupunguza tatizo la usafiri kwa wakazi wa mikoa hiyo.

"Kukamilika kwa ujenzi wa meli hii, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la usafiri kwa wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Mbeya kwa sababu kwa muda mrefu walikuwa wakitumia usafiri wa boti au mashua, lakini hakuna chombo madhubuti kinachofanya kazi ziwani," alisema Gallus.

Alisema meli hiyo pia itafungua wigo wa biashara kwa nchi za Malawi na Msumbiji, hivyo kuongeza wigo na kibiashara na kuboresha uchumi wa kwa jamii zinazozungukwa na ziwa hilo.

Alisema ziwa hilo ni hatari kidogo kwa sababu lina mawimbi makubwa kwa hiyo kuwapo kwa meli hiyo kubwa kutasaidia kuimarisha usalama wa mizigo na abiria wanaokwenda sehemu mbalimbali.

Gallus alisema ujenzi wa meli hiyo ambao ulianza Julai, 2017, chini ya Kampuni ya Songoro Marine, umefikia hatua ya kufunga mitambo, kuweka vyumba, kufunga viti na umaliziaji.

Mbali na meli hiyo, alisema ziwa hilo lina meli mbili za mizigo zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja ambazo ni MV Njombe na MV Ruvuma.






# Waziri Hasunga awaalika wawekezaji kwenye kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amewaalika wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye kilimo cha mboga na matunda katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwa kuwa mikoa hiyo ina fursa kubwa ya kuwekeza kwenye kilimo hicho ikiwamo ardhi yenye rutuba.

Hasunga alitoa hamasa hiyo jana alipokuwa anafungua kongamano la kuhamasisha uwekezaji wa kilimo cha mboga na matunda lililoandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (Saggot) na Shirikisho la Wakulima wa Mboga na Matunda Tanzania (Taha).

Alisema katika mikoa hiyo kuna hali nzuri ya hewa na maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kwa sasa serikali imeweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji ikiwamo kuondoa baadhi ya kodi ambazo zilikuwa kero.

Alisema serikali inahimiza uwekezaji kwenye kilimo hicho baada ya kubaini kuwa kina manufaa makubwa kwa wakulima na taifa kwa ujumla.

"Taarifa zilizopo ni kwamba sekta hii ndogo ililiingizia taifa Dola za Kimarekani

INAENDELEA UK.8

HABARI KITAIFA

# Dk. Abas: Taasisi za serikali ziwape ushirikiano wanahabari

**Na Yasmine Protace,** BAGAMOYO

TAASISI za serikali zimetakiwa kushirikiana na wanahabari ili vyombo vya habari vitoe taarifa sahihi.

Ushauri huo ulitolewa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abas, alipokuwa akizungumzia na vyombo mbalimbali vilivyoshiriki semina ya siku mbili iliyoandaliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Akizungumzia ushirikiano wa maofisa habari wa serikali na vyombo vya habari, alisema ni wakati mwafaka kwa maofisa habari wa serikali kuwa na ushirikiano na vyombo vya habari ili kuwawezesha wanahabari kupata taarifa sahihi.

Alisema taasisi ziendeleze utamaduni wa semina ili kuwasaidia wanahabari kuwa wabobezi.

Alisema taasisi zitoke ofisini badala yake zitoe semina kwa wanahabari ili kuweza kuzungumzia kazi ambazo zinafanywa na taasisi yake.

Aliongeza taasisi zote ziwe na ushirikiano na vyombo vya habari, na kuongeza kuwa kwa upande wa serikali taasisi zijibu hoja ili wananchi waweze kupata taarifa na kama ushirikiano hautakuwapo kwa wanahabari kupata taarifa, taarifa itolewe ili hatua zichukuliwe.

Kuhusu suala la chakula, Dk. Abas aliwataka waandishi kutumia taaluma yao kuwaelimisha wananchi juu ya ulaji chakula salama.

"Kumekuwa na baadhi ya wenzetu hawana elimu ya chakula salama, hivyo nyie mmepata elimu ya chakula salama muitumie kwa kuwaelimisha wananchi," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Rodrick Mpogolo (kushoto), akisalimiana na Mbunge wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, wakati wa uzinduzi wa Morogoro ya Kijani iliyoandaliwa na uongozi wa CCM mkoa huo. jana. Wengine ni viongozi mbalimbali. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Wauawa tuhuma za kujaribu kupora

**Na Dege Masoli,** TANGA

WATU wanne akiwamo kada wa CCM, Mwinjuma Kupaza (62), wameuawa kinyama katika matukio tofauti likiwamo la majibizano ya risasi na polisi kwenye jaribio la uporaji wa kutumia silaha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema jana kuwa, Shafii Juma (27 - 30), mwingine aliyetambuliwa kwa jina moja la Ramadhani (20-22), waliuawa kwa kupigwa risasi na polisi walipokuwa wakijibizana na waporaji wakati wa uporaji.

Bukombe alimtaja Kimuna Shayo, mkazi wa Kwanjeka, jijini hapa kuwa aliuawa na wananchi wenye hasira baada ya kumtuhumu kutaka kuiba.

Alisema wananchi hao walimshambulia na kupoteza maisha wakati alipokuwa akikimbizwa hospitalini.

Aidha, Kamanda alisema aliyekuwa Katibu wa CCM, tawi la Kivilu, Kijiji cha Kwamkomole, wilayani Lushoto, aliuawa kinyama kwa kushambuliwa na tembo alipokuwa shambani.

Alieleza kuwa matukio ya uporaji yaliyosababisha mauaji ya watu hao wawili yalitokea Juni 16 majira ya saa 3 usiku katika kitongoji cha Kerenge, Kata ya Singeni, wilayani Muheza baada ya watu hao kumvamia

INAENDELEA UK.8

# Jalada la rufani larejeshwa kwa jaji

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi chini ya Naibu Msajili Crescencia Kisongo, imerejesha jalada la rufani ya washtakiwa wanne waliohukumiwa kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kuchoma moto kituo cha polisi Bunju kwa Jaji Mfawidhi ili atoe maelekezo.

Hatua hiyo ilifikiwa jana baada ya rufani hiyo inayohusu kesi moja kufunguliwa tofauti na kwamba majalada mengine bado hayajafikishwa mahakamani hapo.

Aidha, majalada ya watuhumiwa hao yamefunguliwa tofauti na kusababisha mengine kushindwa kufikishwa kwenye kikao cha Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kilichoketi jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Naibu Msajili alisema mahakama yake ina jalada linalomhusu mlalamikaji mmoja, Abrahamu Minga, kwa hiyo anarejesha kwa jaji mfawidhi kwa ajili ya maelekezo mengine.

Mapema mahakamani hapo, wakili wa walalamikaji hao, Prof. Abdallah Safari, alidai kuwa hati ya wito mahakamani aliyo nayo ni ya walalamikaji watatu ambao ni Yusuph Sungu maarufu kama Mayuku ambaye jana hakuwapo mahakamani, Juma Konzo na Minga.

Februari, mwaka huu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, iliwahukumu kifungo cha maisha washtakiwa wanane baada ya kutiwa hatiani katika kesi ya kuchoma moto Kituo cha Polisi cha Bunju A na 10 kati yao waliachiwa huru.

Waliohukumiwa ni Yusuph Sugu (40), Juma Kozo (32), Rashid Liwima (29), Baraka Nkoko (23), Abuu Issa (36), Abraham Mninga (23), Veronica Ephraem (32) na Ramadhan Said (22).

Walioachiwa huru ni Mrisho Majaliwa (30), Hamis Ndege (37), Seleman Gwae (33), Mange'nya Anthony (28), Rehema Hussein (32), Rajabu Ally (25), Ally Athuman (24), Amina Matipwili (33), Gubila Temba (51) na Mariam Honza (44).

Katika kesi ya msingi, walidaiwa kuwa Julai 10, 2015 kwa makusudi walichoma moto kituo cha polisi Bunju.


MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD.

TANGAZO LA MNADA

*NDANI YA SIKU 14*

**MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD** kwa idhini iliyopewa na **African Banking Corporation Tanzania Limited ('BancABC')** na kwa hati iliyowekwa kama dhamana mali hiyo itauzwa kwa njia ya mnada. Shamba la *Pulses & Agro Commodities linalomilikiwa na Mr. Rakesh Vohora* na shamba la *Air Born City Limited linalomilikiwa na Abdallah Abdulatif Mohsen* kwa kufuata sheria zote za mnada kwenye jedwali ya chini






| No | Mali | Eneo | Maelezo ya mali | Tarehe/Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Farm NO. 2489 Loborsoit Village, Simanjiro Districy | Loborsoit Village Simanjiro District, Arusha Municipality | CT.NO.25665, L.ONO.267402 FARM NO.2489 | saa nne asubuhi tarehe 2.07.2019 jumanne |
| 2. | Commercial Property, Land Farm No. 7/2 Essimingor Masai District | Essimingor Masai District Arusha Municipality 9,000 Acres | CT.NO.13669 L.ONO.19096 MP NO.56270 | saa nne asubuhi tarehe 3.07.2019 jumatano |

MASHARTI YA MNADA

1. Mshindi atatakiwa kulipa 25% hapo kwa hapo na kiasi kingine kinachobaki anapaswa kulipa ndani ya siku kumi na nne (asilimia 75%) atakaposhindwa kulipa pesa (asilimia 75%) katika mnada huo, asilimia 25% haitarudishwa na ataitwa mshindi wa 2 au 3 kulipa
2. Shamba au mali itauzwa katika hali iliyokuwepo
3. Dalali ana haki ya kutoa au kumpinga mshindi aliyeshinda aliyekiuka vigezo na kumtangaza mshindi wa pili kulipa hela iliyoahi=diwa
4. Gharama za kwenda kukagua mali pamoja na malazi ni jukumu na la mnunuzi anayeenda mnadani

*TANGAZO LOLOTE KABLA YA TOLEO HILI SIO HALALI*

**Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:**
**Marcas Debt Collectors and Auctioneers Limited**
**Safari Hotel Building 2nd Floor,**
**P.O. Box 16823, Arusha Tanzania**
**Simu Na. 0754 268 383, 0713 268 383, 0787 151 550**
**www.marcasinvestments.com**

*Jukumu letu kupeleka Tanzania Mbele*

215281202



MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | MAKAA INVESTMENT (TAWI LA TEGETA) | BERNARD NGOYAYI LOWASA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO BUNJU A WILAYA YA KINONDONI | 02/07/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | ELIBARIKI MASHULULE MBISE(TAWI LA BUGURUNI) | ELIBARIKI MASHULULE MBISE NA HELLEN E. MBISE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NO. ILA000537 ILIYOKO BUGURUNI MNYAMANI – WILAYA YA ILALA | 05/07/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | MOHAMED RAMADHANI NKUSA (TAWI LA KARIAKOO) | MOHAMED RAMADHANI NKUSA | KIWANJA KICHOENDELEZWA CHENYE HATI YA MAUZIANO KILICHOKO KINYEREZI SONGASI—WILAYA YA ILALA | 08/07/2019 SAA: 04:00 ASUBUHI |
| 004 | FROLIAN CHOGO SIMONI (TAWI LA BUGURUNI) | FROLIAN CHOGO SIMONI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KINYEREZI SONGASI- WILAYA YA ILALA | 08/07/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 005 | ATHUMANI MBWANA KAWESA (TAWI LA BUGURUNI) | ATHUMANI MBWANA KAWESA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA MSIMBAZI – WILAYA YA ILALA | 10/07/2019 SAA 09:00 ASUBUHI |
| 006 | PAULO GIRIMBE RAWE (TAWI LA BUGURUNI) | PAULO GIRIMBE RAWE | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO.139603 PLOT 242 BLOCK 8 KILICHOKO MTAA WA MWONGOZO– WILAYA YA KIGAMBONI | 12/05/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 007 | ALLY MOHAMED BARIKI (TAWI LA TANDALE) | ALLY MOHAMED BARIKI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA TEGETA A – WILAYA YA KINONDONI | 15/07/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 008 | MARIAM GEORGE VANGIRISASI (TAWI LA TANDALE) | MARIAM GEORGE VANGIRISASI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MBEZI TEMBONI – WILAYA YA UBUNGO | 18/07/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, AU
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 669,
DAR ES SALAAM
Tel+255 02221183403

Maseto Auctioneer,
MKURUGENZI MTENDAJI,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU
+255 787 288 442 AU +255 762 260 787

115280702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutumie juhudi zote kulinda watoto

**TAKWIMU** za karibuni kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), zinaonyesha kuwa ubakaji na unyanyasaji watoto nchini unatisha.

Zinataja kuwa watoto wanaobakwa kwa siku ni 394, idadi ambayo ni sawa na watoto 2,365. Ni takwimu za kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2018. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), zinaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017, matukio ya uhalifu dhidi ya watoto yalikuwa 13,457.

Hali hiyo inatisha na kama taifa si mwelekeo unaoifikisha nchi kwenye maendeleo endelevu.

Ni kwa vile watoto ambao ni tegemeo la nchi wanaathiriwa na kuumizwa kiafya na kisaikolojia.

Ubakaji na ulawiti una matokea hasi kwa watoto kwa mfano mimba za udogoni, kuambukizwa maradhi kama VVU na Ukimwi, kaswende na homa ya ini.

Aidha, husababisha kisonono, kuharibu mfumo na viungo vya uzazi vya watoto na kusababisha ugumba.

Matokeo haya yanaathiri maendeleo yao kiafya, kielimu na kwenye uzazi watoto walioathirika na maradhi wanapokuwa wazazi kuna uwezekano wa kupata watoto wenye magonjwa yakiwamo VVU, upofu na homa ya ini.

Hili ni jambo lisilokubalika ndiyo maana tunasema ni wakati wa kila mmoja kuwalinda watoto kuanzia wazazi, walezi, jamii na taifa zima. Tunawashauri wazazi na walezi kuwatunza na kuwalinda watoto kikamilifu. Wawafunze jinsi ya kuepuka kunajisiwa, kubakwa na kuhakikisha kuwa watu wasiofahamika hata jamaa na ndugu zao wa karibu hawapewi nafasi ya kuwa karibu na kuwazoea watoto.

Utafiti unaonyesha kuwa ndugu na jamaa wa karibu wanahusika kuwanyanyasa watoto.

Ni wakati wa kudhibiti tabia hizo na kuachana na mienendo ya kuwaruhusu wageni hata kama ni ndugu zetu tusio na taarifa zao kujumuika na watoto wetu hasa kwa kuwaruhusu kulala nao.

Ingekuwa vyema kuzungumza nao kuhusu ulinzi wa watoto wetu na sisi kama walezi na wazazi kusimama maisha ya watoto wetu. Wapo watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wakitunzwa na bibi au babu, hawa ni jukumu la kijiji na wana idara ya ustawi wa jamii kuwalinda na kuwasimamia maisha yao.

Ikumbukwe kuwa kuna wanaume wanaoa wanawake wenye watoto ili kuwanyanyasa watoto kingono.

Hili nalo ni wakati wa kulimulika na kuwachukulia hatua ili kukabiliana na tatizo hilo.

Ndiyo maana tunasitiza kuwa kupinga unyanyasaji, ubakaji na ulawiti wa watoto ni jukumu la jamii nzima na wakati umefika sasa kila mmoja kwenye nafasi yake awalinde watoto.

Kwa kuwajibika kuripoti vitendo vya unyanyasaji vilivyofichika kwenye jamii yetu.

Hatua hii ni muhimu hasa wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo hufanyika kila Juni 16 na kaulimbiu ya mwaka huu ni hii: "Mtoto ni msingi wa taifa endelevu, tumtunze, tumlinde na kumwendeleza."


Taarifa za kitafiti kutoka LHRC zinasema kuwa Zanzibar vitendo hivyo vinadaiwa kuongezeka.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, Mkurugenzi wa Miradi ya Asasi ya Kulinda Watoto ya SOS Zanzibar, Asha Salim Ali, anasema hayo.

Anasema licha ya serikali kuwa na sheria mbalimbali, sera na mipango ya kuwalinda watoto dhidi ya aina zote za udhalilishaji, bado vitendo hivyo vinaendelea kutokea ikiwamo kubakwa na kulawitiwa. Ni wakati wa kuchukua hatua ya kuwalinda watoto kama kaulimbiu inavyosisitiza kuwa bila watoto hakuna maendeleo endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mikoa ichukue mkakati wa Shinyanga kutokomeza vifo vya uzazi nchini

Na **Raphael Kibiriti**

**NIMEVUTIWA** kuandika Tulonge hii na moja za makala zilizoko katika kijarida cha elimu kwenye gazeti hili yenye kichwa cha habari kisemacho "Shinyanga yaja na sheria ndogo ili kutokomeza vifo vya uzazi" ukurasa wa 15.

Kifupi ni kwamba mkoa huo umekuja na mkakati wa kutunga sheria ndogo zitakazotekelezwa katika ngazi ya kijiji ambapo mjamzito asiyehudhuria kliniki au anayejifungulia nyumbani ama kwa mkunga wa jadi bila kwenda kituo cha afya, atatozwa faini ya Sh. 20,000.

Kwamba mkoa umekuja na mkakati huo baada ya kuona vifo vitokanavyo na uzazi mkoani humo vinaendelea licha ya jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na serikali za kuboresha huduma ya afya mkoani humo na mikoa mingine katika ngazi ya taifa.

Kwa mujibu ya Mratibu wa Huduma ya Uzazi na Mtoto mkoani Shinyanga, Joyce Kandolo kama alivyonukuliwa na Nipashe, idadi ya vifo vya kinamama kutokana na uzazi mkoani humo kwa mwaka 2017 ilikuwa ni 73.

Na kwamba kwa mwaka jana kinamama 56 walifariki kutokana na uzazi na mwaka huu kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki kinamama 18.

Kimsingi idadi hii ya vifo vya uzazi katika mkoa mmoja kwa maoni ya Muungwana si ya kuvutia na hasa ikitiliwa maanani uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na serikali kibajeti ili kuboresha miundombinu na huduma za kiafya kwa ujumla.

Tukiitalii ripoti ya muhtasari wa matokeo ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria ya mwaka 2015-16 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), uwiano wa vifo vitokanavyo na uzazi ni vifo 556 kwa kila watoto 100,000 wanaozaliwa hai.

Kwa maana hiyo na kwa hesabu ya Muungwana, wastani wa vifo hivyo 556 kwa mikoa 26 ya Tanzania Bara ni vifo 21 kwa kila mkoa.

Sasa mkoa unapokuwa na vifo 73 kwa mwaka 2017 au 56 kwa mwaka jana, hakika ni idadi isiyopendeza.

Ni idadi ambayo kimsingi inahalalisha hatua zote stahiki za kukabiliana na hali hiyo kama hizo zinazochukuliwa na mkoa wa Shinyanga wa kuja na sheria ndogo inayolenga kutoza faini wajawazito wasiohudhuria kliniki ama wasiojifungulia katika vituo vya afya.

Kuna mambo mengi yanayosababisha vifo vya uzazi, ikiwa ni pamoja na kuzaa katika umri mdogo, utoaji wa mimba na ukosefu wa huduma za afya zinazostahili kwa kutaja baadhi.

Sasa serikali na wadau mbalimbali wanaendelea kuboresha sekta ya afya kirasilimali watu, vifaa tiba, na miundombinu yake, kwa lengo la kustawisha maisha ya Watanzania, wajawazito wakiwamo.

Serikali inafanya hivyo kwa sababu mbali na kuboresha maisha ya kinamama lakini pia inatimiza dhima ya kusukuma mbele maendeleo ya taifa, ambapo huduma bora ya afya ni moja ya viashiria vya wazi vya namna nchi inavyoendelea.

Kwamba nchi inapofanikiwa kwa mfano kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi, ni dalili ya maendeleo yaliyo wazi yasiyohitaji mwanasiasa kusimama jukwaani na kuhubiri kwamba nchi inaendelea kwa kasi.

Kwa hali hiyo, Muungwana ana maoni kwa mikoa mingine nchini kuja na mikakati kama huu wa mkoa wa Shinyanga, yenye lengo la kutokomeza vifo vitokanavyo na uzazi.

Ana maoni hayo kwa sababu tatizo hili si la mkoa wa Shinyanga tu, bali ni la mikoa karibu yote nchini.

Ninasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa utafiti wa NBS, takribani theluthi mbili kwa maana ya asilimia 63 ya watoto nchini Tanzania wanazaliwa katika vituo vinavyotoa huduma ya afya.

Hivyo bado kuna asilimia 37 ya watoto ambao wanazaliwa nyumbani ama kwa wakunga wa jadi, takwimu zinazokumba takribani mikoa yote nchini.

## MJADALA/BARUA

# Walezi tusifuge tabia zisizo-kubalika

*Mhariri*

*KWA kweli kuna tabia ambayo inanishangaza sana mimi ya baadhi ya wazazi na walezi katika jamii yetu hii ya Kitanzania ambao kwa kiasi kikubwa hawako tayari kusikiliza ushauri wanaopewa na majirani zao juu ya tabia za watoto wao.*

*Katika mtaa ninaoishi hapa Mbalizi mkoani Mbeya, kuna jirani yangu aliye na mtoto mwenye tabia zisizokubalika katika jamii ya wastaarabu na hata katika mwenendo wa kawaida wa maisha ya watu.*

*Mtoto wake huyu ana tabia ya kukwapua mali za watu na hata kukaba hasa nyakati za usiku na mchana kwenye maeneo yasiyo na watu.*

*Anafanya uhalifu huu kwa kushirikiana na vijana wanaotoka maeneo mengine ya jiji hili la Mbeya.*

*Lakini cha kusitikisha zaidi ni kuwa kwa majirani ambao wameshawahi kwenda kuwaeleza wazazi wake juu ya uhalifu anaoufanya kijana wao, mara nyingi wamekuwa wakikataa kuwa kijana wao hana tabia hiyo.*

*Kwamba wanaoenda kulalamika kwao wanamuonea gele kijana wao kutokana na maendeleo anayoyafanya.*

*Naomba serikali ya mtaa wetu ichukue hatua ya kumkanya kijana huyo, ili aachane na tabia hiyo kwani inaweza ikamhatarishia maisha yake siku moja na hasa pale wananchi watakapojichukulia sheria mkononi.*

**Jason Mandyanga-Mbalizi**

# Kilio cha watoto kwenye maadhimisho kisikike, waachwe wapate elimu vizuri



Fursa nzuri ya watoto kusoma kwa uhuru kama hawa ni faida kwa taifa la kesho. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

MAADHIMISHO ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka huu, ambayo yalifanyika Jumapili iliyopita yalikuwa na kaulimbiu isemayo: "Mtoto ni msingi wa taifa endelevu, tumtunze, tumlinde na kumwendeleza."

Siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa Juni 16 ya kila mwaka ikiwa na kaulimbiu mbalimbali zinazolenga kumlinda mtoto ikiwamo kumtimizia mahitaji yake ya muhimu.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, ambayo kimkoa yalifanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi, Makuburi, jijini Dar es Salaam, watoto walilalamikia vitendo vya ukatili ukiwamo wa kutowapa fursa ya kupata elimu.

Miongoni mwa watoto hao ni wanafunzi kutoka shule za msingi za wilaya ya Temeke na Kigamboni ambao wako chini ya mradi kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni kwenye shule 10, unaosimamiwa na asasi ya kiraia ya Ekama Development Foundation.

Shule hizo ni Mivinjeni, Temeke, Keko Mwanga, Tandika, Unubini, Mji Mpya, Kizinga, Juhudi, zote za wilaya ya Temeke na Ufukoni, Mji Mwema za wilaya ya Kigamboni.

Watoto wanasema baadhi ya wazazi na walimu wamekuwa wakifanya vitendo vya ukatili dhidi yao au wenyewe kwa wenyewe kufanyiana vitendo vya ukatili na hivyo kujikuta wakiathirika kadri ya malengo yao ya baadaye kielimu.

Wito wao ni kwamba wazazi wasimamie malezi mema ili kutokomeza vitendo vya ukatili ambavyo baadhi ya watoto wamekuwa wakifanyiwa au kufanyiana wenyewe kwa wenyewe.

Aidha, wanaamini kwamba kaulimbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka huu inaweza kusaidia kukomesha hayo yote iwapo kila mzazi, mlezi, mwalimu atazingatia wajibu wake na kuutimiza kikamilifu.

Wazazi na walezi wanatakiwa kuhakikisha watoto wao wanapata elimu, walimu nao kwa upande wake wanatakiwa kufundisha, lakini pia watoto wenyewe kwa wenyewe hawatakiwi kufanyiana vitendo vichafu.

Kila upande ikitimiza wajibu wake inavyotakiwa, kuna uwezekano mkubwa watoto kutimiziwa haki zao za msingi ikiwamo ya kupata elimu na siyo kufanyishwa biashara ndogondogo au kutopelekwa shule kwa makusudi.

Ikiwezekana, kila shule ianzishe mradi kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni ili kubaini na kukomesha vitendo hivyo kwa watoto, ambavyo vimekuwa vikisababisha wakose haki ya kupata elimu.

Cha msingi ni kuzingatia kaulimbiu hiyo inayosisitiza na kukumbusha jamii kuhusu umuhimu wa kutambua na kuzitekeleza haki za watoto kwa vile Tanzania imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto.

Haki zao zikitekelezwa kikamilifu, hata vitendo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto katika jamii vitapungua kama siyo kumalizika kabisa, kwani kila mmoja atakuwa na jukumu la kumlinda mtoto.

Inaumiza na inakera zinapokuwapo takwimu kama hizi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kwamba katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya mwaka 2018, watoto 2,365 walibakwa.

Ikumbukwe watoto ni taifa la kesho, hivyo wale ambao wamekuwa wakiendelea kuwafanyia ukatili wajue kuwa wanaharibu taifa la baadaye ambalo wanapaswa kuliandaa sasa.

Wazazi na walezi watambue kuwa mtindo wa kutowapeleka watoto shule na kuwaingiza katika ndoa za utotoni ni ukatili mwingine ambao haupaswi kufumbiwa macho.

Kuna mikoa mitano inatajwa kuongoza kwa matukio ya ukatili nchini yakiwamo ya ubakaji na ulawiti.

Mikoa hiyo na matukio yenyewe kwenye mabano ni Tanga (1,039), Mbeya (1,001), Mwanza (809), Arusha (792), Tabora (616).

Mjadala unaona ni vyema basi mikoa hiyo ikazingatia kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka huu wa 2019 na kutambua kuwa mtoto ni msingi wa taifa endelevu, atunzwe, alindwe na aendelezwe.

Kimsingi kaulimbiu hiyo inapaswa kuwa chachu ya kuwafanya wazazi na walezi wenye mawazo potofu kuachana nayo na kusimama imara katika kumlinda mtoto na kumtimizia haki zake za msingi.

Kilio cha watoto walichokitoa kwenye maadhimisho ya siku yao ya mwaka huu kisikike, waachwe wasome, tena wakiwa huru ili waweze kutimiza ndoto zao za baadaye kwani wao ndio taifa la kesho.

Wakiandaliwa vyema kwa kupewa elimu watakuwa taifa bora la baadaye, kinyume chache wakiendelea kufanyiwa ukatili na kukosa elimu, mwisho wa siku ni kuwa na taifa la ajabu la baadaye.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Upinzani waja na bajeti kivuli ya tril. 29/-

INATOKA UK. 2

kwa pato la taifa kwa madai kuwa nakisi huonekana kuwa ndogo wakati kimsingi bajeti ni tegemezi kwa asilimia 30.

Katika bajeti hiyo, Silinde alilieleza Bunge kuwa katika sekta ya viwanda, wamejielekeza katika kushughulikia uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

Kabla Silinde hajaanza kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hali ya uchumi wa taifa, mpango wa maendeleo wa taifa na makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2019/20, Naibu Spika, Dk.Tulia, alimtaka msemaji huyo kutosoma aya ya 18,30, 31,43,44 na 45.

Aya nyingine zilizozuliwa zisisomwe kwa maelekezo ya Spika wa Bunge, Job Ndugai ni aya ya 46,47,48,49,50,51 na 52 pamoja na sehemu A, I,J,M,O na Q.

**MKWAMO WA UCHUMI NA UKATA**

Silinde alisema: "Mkwamo wa uchumi na ongezeko la ukata imekuwa changamoto kubwa hata miongoni mwa wachumi kuhusu hali ya uchumi nchini hasa inapoonekana biashara nyingi zimefungwa kwa kushindwa kujiendesha, kusinyaa kwa uwekezaji mkubwa, kudorora uwekezaji kutoka nje (FDI) na kuyumba kwa biashara katika sekta ya nyumba.

"Lakini pia, kampuni kwa ujumla wake zinazidi kupunguza wafanyakazi, kuporomoka kwa thamani ya hisa katika soko la mitaji ukata kwenye uchumi, lakini bado serikali inatangaza uchumi kuwa imara."

Msemaji huyo wa kambi ya upinzani, alilieleza Bunge kuwa wanaona miradi inayotekelezwa ipo kisiasa zaidi na hakuna mkakati wala mpango wa kibiashara ambao umewekwa wazi na serikali hadi sasa. Alisema mradi wa reli ya kisasa ya Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ambao unatarajiwa kugharimu Sh. trilioni 17.6 na unaotarajiwa kukamilika mwaka 2021, hauna mkakati endelevu wa kufungamanisha sekta za kiuchumi na mradi huo. Kuhusu mradi wa kufua umeme wa maji katika Bonde la Mto Rufiji (Stiegler's Gorge), Silinde alisema kutokana na ukosefu wa mpango madhubuti wa utekelezaji, kuna shaka kama utafikia malengo yaliyokusudiwa. Mradi huo unatarajiwa kuzalisha megawati 2,100 kwa kutumia maji unakisiwa kugharimu kiasi cha Sh. trilioni nne.

# Wema aswekwa mahabusu siku 7

INATOKA UK. 3

tumbo na Juni 14, mwaka huu nilishindwa kuja nilikwenda Morogoro kikazi, nilimpa taarifa wakili wangu," alidai Wema. Hata hivyo, Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kumbukumbu za mshtakiwa huyo katika kuhudhuria mahakamani si nzuri, lakini alitakiwa kuwaagiza wadhamini wake ili kuiepushia mahakama usumbufu.

"Nimesikia hoja za pande zote mbili. Mahakama yangu itatoa uamuzi Juni 24, mwaka huu, na kwa sababu suala hili linahusu dhamana, mshtakiwa atakwenda rumande mpaka siku ya uamuzi wa mahakama hii," alisema Hakimu Kasonde. Juni 11, mwaka huu, mahakama hiyo ilitoa hati ya kukamatwa Wema baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yake.

Hatua hiyo, ilifikiwa baada ya upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Silvia Mintanto, kuomba hati ya kukamatwa msanii huyo.

Wakili wa utetezi, Reuben Semwanza, alidai kuwa mshtakiwa alifika mahakamani kusikiliza kesi yake lakini alipatwa na ugonjwa wa ghafla.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anadaiwa kuwa Oktoba 15, mwaka jana, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alichapisha video ya ngono na kuisambaza katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFAA YA TANZANIA
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MAPITIO YA MADAI NO. 3 YA 2014

YUSUFU ABDALLA (The Administrator of the Estate of the late KWEGE YUSUPH ................................ MLETA MAOMBI

DHIDI YA

1. SIJALI YUSUFU SELEMAN
2. HAMIS MWINYIMKUU WAKUTI
3. KIZURIA AUCTION MART ENTERPRISES LIMITED
4. NELSON ELIEZA MGENI

............................. WAJIBU MAOMBI

KWA:

KIZURIA AUCTION MART
ENTERPRISES LIMITED
DAR ES SALAAM.

Unajulishwa kwamba, Rufaa katika Shauri tajwa yaliyowasilishwa kwenye Mahakama hii na Mleta Rufaa imepangwa kusikilizwa siku ya Alhamisi tarehe 20 Juni, 2019 saa tatu asubuhi katika Kikao cha Mahakama ya Rufani kinachoendelea hapa Dar es Salaam.

Unatakiwa kuhudhuria mbele ya Mahakama hii kwa muda uliotajwa bila kukosa na endapo hutahudhuria, basi Rufaa husika itasikilizwa na kuamuliwa bila ya wewe kuwepo.

Taarifa hii imetolewa na kupigwa chapa ya Mahakama hii leo tarehe 12 Juni, 2019.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

S. J. KAINDA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFAA

215281602

# Msekwa afunguka

INATOKA UK. 2

"Hatimaye siri yenyewe ilikuja kufichuliwa jioni ya tarehe hiyo (Aprili 22, 1964) baada ya Mkataba wa Muungano kuwa tayari umetiwa saini. Siri ilifichuliwa kwa njia ya taarifa rasmi ya serikali ambayo ilitolewa Ikulu mjini Dar es Salaam iliyotangazwa kwamba:

'Rais Julius Nyerere wa Jamhuri ya Tanganyika na Rais Abeid Karume wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, leo wametia saini mkataba wa makubaliano ya kuunda muungano wa nchi hizo. Makubaliano hayo ni sharti yaridhiwe na serikali zote mbili pamoja na mabunge ya nchi zote mbili," Msekwa anaeleza katika kitabu chake hicho. Msekwa ambaye kipindi hicho alikuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Tanganyika anaendelea kueleza kuwa hata mazungumzo baina ya marais hao juu ya suala hilo, yalibaki kuwa siri ya waasisi hao wawili hadi walipofika hatua ya kutia saini Mkataba wa Makubaliano ya Muungano.

"Lakini, mchakato haukuishia hapo kwani ili mkataba huo upate uhalali wa kisheria na kama ilivyokuwa imeelekezwa katika kifungu kidogo cha VIII cha mkataba huo, ilibidi uridhiwe na vyombo vya uwakilishi vya nchi hizi mbili, ambavyo kwa wakati huo vilikuwa ni Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

"Kazi hiyo ilitekelezwa ipasavyo na vyombo hivyo viwili siku ya Jumamosi Aprili 25, 1964, ambapo Baraza la Mapinduzi la Zanzibar lilitangulia kufanya kikao chake asubuhi ya siku hiyo na Bunge la Tanganyika likafuatia kwa kikao kilichofanyika mchana siku hiyo hiyo.

# Madereva wa malori waondolewa vikwazo

INATOKA UK. 4

serikali inahitaji madereva ambao wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa.

"WFP na serikali tutaendelea kushirikiana katika sekta ya usafirishaji, mafunzo haya yaliyotolewa yatakuwa ni chachu katika kufanikisha Tanzania ya viwanda, kwani hatuwezi kujenga uchumi imara bila ya kuwa na sekta bora ya usafirishaji," alisema Nditiye.

Naye Mkuu wa Idara ya Usafirishaji WFP, Riaz Lodhi, alisema ili mtu awe dereva mzuri, lazima awe na lishe bora, afahamu kwa undani ugonjwa wa Ukimwi, masuala ya jinsia na haki za watoto, pia wanapaswa kufahamu maambukizi ya magojwa ya mlipuko."

Aliongeza kuwa WFP imekuwa ikisafirisha chakula tani milioni 3.5 kwa mwaka kwenda katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zenye matatizo ya uhaba wa chakula.

# Waziri Hasunga awaalika wawekezaji

INATOKA UK. 4

milioni 764 mwaka 2017, ikilinganishwa na Dola milioni 64 mwaka 2015, sasa tunawahimiza wawekezaji kuendelea kuja kuwekeza ili kuimarisha zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhamasishaji wa Uwekezaji kutoka katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mnali, alisema lengo la kuandaa kongamano hilo ni kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na serikali za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameandaa ardhi ya kutosha kwa ajili ya wawekezaji watakaoonyesha nia ya kuwekeza hasa kwenye kilimo cha mboga na matunda.

Alisema TIC pamoja na wadau wengine wanalenga kukuza kilimo cha mazao hayo ili kiwe na manufaa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema katika mkoa huo kuna fursa kubwa ya uwekezaji kwenye kilimo cha mazao hayo ikiwamo miundombinu ya barabara na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe.

Kongamano hilo la kuhamasisha uwekezaji linafanyika kwa siku mbili katika Jiji la Mbeya likiwahusisha wakulima na wawekezaji kutoka zaidi ya mataifa saba duniani ambao wanataka kuwekeza.

# Wauawa tuhuma za kujaribu kupora

INATOKA UK., 5

mfanyabiashara, Abasi Twaha na kumpora Sh. 339,000. Alisema jaribio hilo lilizimwa na askari waliyokuwapo doria eneo hilo.

Alieleza kuwa majambazi hao wakiwa na silaha aina ya shotgun iliyokatwa mtutu, baada ya kuwaona askari waliwarushia risasi na katika majibizano hayo walipata majeraha sehemu mbalimbali za miili na kupoteza maisha wakiwa njiani kupelekwa hospitali.

Alisema Shayo aliuawa Juni 17 majira ya saa mbili usiku akituhumiwa kuvunja nyumba ya Juma Rashid kwa

nia ya kutaka kuiba, lakini wakati akitekeleza azima yake hiyo alitiwa mikononi mwa wananchi wenye hasira na kumshambulia hadi kupoteza maisha wakati akikimbizwa hospitalini.

Kamanda Bukombe alieleza mafanikio yaliyopatikana kutokana na kampeni ya kukabiliana na wahalifu inayoendeshwa na jeshi hilo, ndani ya wiki moja zimeokolewa mali mbalimbali zikiwamo Sh. 339,000 taslimu alizoporwa mfanyabiashara Abasi.

Vitu vingine vilivyokamatwa katika msako huo vikiwamo televisheni, pikipiki, bunduki aina ya shotgun iliyokatwa mtutu na kutengenezwa kienyeji, mapanga, visu, bisibisi na tochi kubwa.

## HABARI KITAIFA

# Makumbusho ya Taifa yaagizwa kujitangaza nje

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Makumbusho ya Taifa kuanzisha kampeni ya kutangaza ndani na nje ya nchi vivutio mbalimbali ambavyo vinapatikana katika makumbusho zote yakiwamo masalia ya binadamu wa kale.

Prof. Mkenda aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea makumbusho hayo na kujionea urithi na hazina ya taifa ambao ni pamoja na mafuvu na masalia ya binadamu wa kale au zamadamu.

Masalia hayo ni pamoja na Australopithecus, Afarensis, Zinjanthropus (paranthropus) boisei, Homo habilis, Homo erectus na Homo sapiens, yenye umri wa tangu miaka milioni 3.6 hadi miaka 200,000 iliyopita.

Alisema matangazo kwenye runinga, redio na magazeti kuhusu vitu vinavyotunzwa Makumbusho ya Taifa, yatajenga uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa makumbusho na hivyo, kufanya watu wengi kuyatembelea. "Msipotangaza hakuna anayewezea kujua kuwa vitu muhimu kama hivi viko hapa Makumbusho ya Taifa, tunatakiwa tuwaambie wananchi ili waje kuviona," alisisitiza.

Prof. Mkenda alisema, "Tunapoelekea kwenye maadhimisho ya miaka 60 tangu kugunduliwa kwa fuvu la Zinjanthropus, fuvu hilo, halitaondolewa Makumbusho ya Taifa kwenda bonde la Olduvai, bali litaendelea kuhifadhiwa na kutunzwa vizuri Makumbusho ya Taifa na badala yake nakala itatumika pale inapohitajika," alisema.

Aidha, amesisitiza kuwa matangazo hayo yawe ya ndani na nje ya nchi (International Promotion) kwa sababu kuna watafiti wengi nje ya Tanzania ambao wangependa kuja kufanya utafiti katika nyanja za akiolojia na paleontolojia. Sambamba na hilo, Prof. Mkenda alimwagiza Mhifadhi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Dk. Freddy Manongi na Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa Prof. Audax Mabulla, kuisimamia kamati inayohusika na maandalizi ya maadhimisho hayo kubuni na kupanga matukio mbalimbali yatakayoleta hamasa katika kuadhimisha miaka 60 ya ugunduzi wa Zinjanthropus na kutangaza vivutio mbalimbali vilivyoko Tanzania. "Matukio tofauti yaandaliwe kuanzia mwezi Julai mpaka Desemba mwaka huu kama sehemu ya kumbukumbu ya ugunduzi wa fuvu la Zinjanthropus boisei," alisema. Akiwa Makumbusho ya Taifa, Prof. Mkenda alitembelea chumba cha kuhifadhi mikusanyo adhimu na kujionea masalia ya binadamu wa kale, hati ya Uhuru wa Tanganyika, Tai ya Uhuru, vinyago vya makabila mbalimbali na vibuyu halisi vilivyotumiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere kuchanganya mchanga kama ishara ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuwa Tanzania, tukio lililofanyika Aprili 26, mwaka 1964.



Dereva wa pikipiki akiwa amebeba abiria, huku amemfunga mbuzi ndani ya boksi, katika Barabara ya Morogoro eneo la Kimara Mwisho, jijini Dar es Salaam wikiendi, kitendo ambacho ni ukiukwaji wa haki za wanyama. **PICHA: JOHN BADI**

# Wananchi wakombolewa maji

**Na Mwandishi Wetu,** MBULU

SHIRIKA la Misaada la Makanisa ya Norway (NCA) na Kituo cha Kimataifa cha Utamaduni cha 4CCP yamekamilisha kiu ya muda mrefu ya wananchi wa vijiji vinavyokabiliwa na ukame katika eneo la Mbulu Vijijini kupata huduma ya majisafi, baada ya kutaabika kwa miongo kadhaa.

Wananchi wa ukanda wa tambarare wa Hydom tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961 hawajawahi kufurahia majisafi ya kunywa, hadi jana Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Mzee Mkongea Alli, kuzindua miradi hiyo ya wahisani.

Alikuwa akizungumza katika kijiji cha Getanyamba, Mbulu Vijijini, wakati akizindua mradi wa maji wa kisima kirefu utakaohudumia zaidi ya wananchi 1,000.

Kabla ya kuzindua mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alimweleza Alli kwamba mradi huo utawawezesha wananchi wa Getanyamba iliyopo Kata ya Geterere, Tarafa ya Hydom kupata majisafi na salama kwa karibu na kupata muda wa kutosha kufanya shughuli nyingine za maendeleo.

"Idadi ya watu waliopo katika kijiji hiki ni 4,250 na wakazi wanaohudumiwa na mradi huu ni zaidi ya 1,000 ambao ni sawa na asilimia 24 ya wakazi wote," alisema Mofuga.

Licha ya mradi huo kupeleka ahueni kwa wananchi hao, bado kuna wananchi wengine 3,250 hawajafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

Akitoa ufafanuzi utekelezaji wa mradi huo, Mratibu wa Kituo cha Utamaduni cha 4CCP, Eliminata Awet, alisema kabla ya kujengwa mradi huo wananchi hao walikuwa wakitembea kilomita 3 hadi 5 kwa siku kwenye korongo la Hydom na Kijiji cha Endagaw.

"Mradi huu ulianza kujengwa Septemba mosi mwaka 2017 kwa kuchimba kisima kirefu cha maji chenye urefu wa mita 100 na kufungwa pampu ya mkono, lakini mwezi Oktoba mwaka 2018, mradi uliboreshwa zaidi kwa kuwekewa miundo mbinu ya kusukuma maji kwa kutumia nishati ya jua," alieleza Awet.

# Shirika lalaani ubakaji watoto

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Maendeleo ya Kimataifa nchini (BRAC), limekemea vitendo vya unyanyasaji wanavyofanyiwa watoto hususan vya ubakaji na kuwaomba Watanzania kuendelea kuvikemea kwa nguvu zote.

Meneja wa Programu ya Elimu wa ABRAC, Suzan Bipa, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika na kwamba bado kuna haja kubwa ya kuhakikisha mtoto analindwa na kupatiwa haki zake zote za msingi ikiwamo kulindwa, kutunzwa, na kuendelezwa.

"Hatuwezi kuendelea kuona mtoto ananyanyaswa na kunyimwa haki zake za msingi, lazima tusimame kuungana na serikali kuhakikisha tunalaani na kupinga unyanyasaji huo," alisema Bipa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Temeke, Teresia Mkwange, alisema matukio ya ubakaji kwa watoto yamekuwa yanatishia usalama wa mtoto.

Aliwaomba wazazi kuhakikisha wanakuwa karibu na watoto wao ili kufuatilia kwa karibu mienendo yao.

Alisema jamii ina wajibu mkubwa wa kulinda watoto dhidi ya ukatili na kutoa taarifa dhidi ya watu wanaowafanyia ukatili ili hatua zichukulie dhidi yao.

# Shingo, uti wa mgongo kuchunguzwa

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU bingwa wa maradhi ya maumivu ya uti wa mgongo kutoka India wanawasili nchini wiki hii na wanatarajia kuwafanyia uchunguzi Watanzania wenye matatizo ya aina hiyo na kuwapa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Hospitali ya Regency, utakakofanyika uchunguzi huo Juni 21 na 22 wiki hii, wataalamu hao bingwa wa maradhi ya mgongo na shingo ni Dk. Viral Shah, Dk. Ritesh Patel na timu ya wataalamu wengine kutoka nchini humo.

Ilisema kwenye taarifa hiyo kuwa jitihada hizo ni kutaka kupunguza rufani za wagonjwa wanaokwenda nje ya nchi kwa matibabu hali itakayosaidia kuwaondolea gharama wagonjwa kwa kupata matibabu ya kibingwa hapahapa nchini.

Ilisema wataalamu hao watafanya uchunguzi wa matatizo mbalimbali ya mgongo kama maumivu ya shingo, maumivu ya uti wa mgongo na mengine yanayohitaji utaalamu wa hali ya juu kama upasuaji.

Kambi hiyo watachagua wagonjwa ambao wana matatizo yanayohitaji matibabu ambayo yatafanyika hospitali hapo.

"Hii ni fursa nzuri kwa Watanzania kuja kuchunguzwa na kupatiwa matibabu ya kibingwa badala ya kutumia gharama kubwa kwenda India," ilisema taarifa hiyo.

## Soko la mahindi, mchele lapatikana nchi 7

WIZARA ya Viwanda na Biashara imesema masoko ya mchele na mahindi yamepatikana katika nchi saba na wamepokea maombi ya mahitaji ya mazao hayo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Stella Manyanya alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Tunduma (Chadema), Frank Mwakajoka, ambaye alihoji ni lini serikali itatafuta masoko ya uhakika ya ndani na nje kwa wakulima wanaozalisha mazao ya chakula kama mahindi na mpunga.

Akijibu swali hilo, Manyanya alitaja nchi hizo kuwa ni pamoja na Oman, Misri, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Burundi na Visiwa vya Comoro.

Alibainisha kuwa wizara yake kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan-Trade) imekuwa ikiratibu jitihada mbalimbali za upatikanaji wa masoko ya mazao mbalimbali yanayozalishwa nchini yakiwamo mahindi na mpunga.

"Jukumu la utafutaji masoko ndani na nje ya nchi, ikiwamo masoko ya mazao ya chakula ni jukumu endelevu na utekelezaji wa jukumu hilo huhusisha taasisi ya Tan-Trade, Balozi za Tanzania nje ya nchi, bodi za mazao, soko la bidhaa za mazao na sekta binafsi," alisema.

Alisema kuwa lengo la kutumia balozi za hapa nchini zilizopo nje ya nchi ni kupata taarifa za kina kuhusu mahitaji ya masoko ya mazao na bidhaa za Tanzania katika nchi husika.

Kadhalika alisema kupitia TanTrade walipokea maombi ya sekta binafsi kutoka Rwanda ya kununua tani 102,000, Burundi (100,000), Zambia (3,000) na visiwa vya Comoro (3,000) za mahindi kwa kipindi cha mwaka 2018/19.

Manyanya alifafanua kuwa kwa mujibu wa takwimu za mauzo ya nje za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tayari takribani tani 39,218 za mahindi zimeshauzwa.

# Ubunifu wapunguza ajali kwa asilimia 43

SERIKALI imesema kupitia Baraza la Taifa la Usalama Barabarani imebuni na kutekeleza mkakati wa kupunguza ajali za barabarani ambao katika awamu ya tatu mpaka sasa umefanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 43.

Aidha, awamu ya nne ambayo inaendelea kutekelezwa wamejipangia kupunguza ajali kwa asilimia 35.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Hawa Mwaifunga.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema ajali za barabarani bado ni tishio kubwa kwa maisha ya Watanzania kutokana na ajali hizo.

"Tunapoteza nguvu kazi ya taifa na familia nyingi zinabaki zikitaabika, je, serikali imejipanga vipi kukabiliana na ajali hizi," alihoji.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema kutokana na athari kubwa za ajali za barabarani kwa taifa, serikali ina mikakati madhubuti ya kupambana na tatizo hilo.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuongeza wigo wa elimu ya usalama barabarani kwa watumiaji wa vyombo vya moto kwa njia ya redio, runinga, machapisho na vipeperushi.

Pia alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuboresha mifumo ya utendaji katika maeneo ya ukaguzi wa mabasi na malori, mfumo wa ufuatiliaji wa magari barabarani na utoaji nukta katika leseni za madereva utakaodhibiti tabia za madereva wazembe.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Ndanda (Chadema), Cecil Mwambe, alimtaka waziri kuwaeleza Watanzania ni namna gani wanatakiwa kutumia alama za barabarani ikiwamo alama ya pundamilia.

"Sasa hivi hata kama hakuna mtu, lakini kuna askari wanasimama maeneo hayo na kuvizia watu wakipita wawakamate sehemu inayofuata, kumekuwa na tabia mbaya sana ya askari wa usalama barabarani kwa vijana wa bodaboda nadhani ni Tanzania nzima."

"Wanapowakimbiza huwa wanawachapa viboko mgongoni na wakati mwingine kuvutwa na kudondoka chini wanaumia, nini tamko la serikali kuhusu hili maana nia ni kuzuia ajali," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema askari hawachapi viboko na hajawahi kusikia wala kuona.

Naye, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alihoji waathirika wa ajali za barabarani hulipwa bima ili kufidia machungu.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Wizara hiyo, Kangi Lugola, alisema suala hilo ni la kisheria na kuwataka Watanzania wanaopata ajali kufuatilia bima ili waweze kulipwa fidia.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: PMO**

# Serikali yabaini, yakamata watuhumiwa dawa za kulevya

BUNGE limeelezwa kuwa tangu awamu ya tano iingie madarakani imewabaini na kuwakamata watuhumiwa mbalimbali ikiwamo watumiaji wa dawa za kulevya za viwandani.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainabu Katimba.

Katika swali lake, Katimba alihoji kama serikali ipo tayari kuwaelekeza Watanzania hususan vijana kuwa ni hatua gani zimechukuliwa tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani katika kuwabaini, kuwachunguza na hatimaye kuwafikisha mahakamani wale wote waliobainika kujihusisha na mtandao wa biashara za dawa za kulevya.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana waliotumbukia kwenye dimbwi la matumizi ya dawa za kulevya," alihoji.

Akijibu maswali hayo, alisema watumiaji wa dawa za kulevya za viwandani mwaka 2016 kulikuwa na makosa 679, watuhumiwa waliokamatwa ni 1,269, wanaume ni 1,127 na wanawake 142.

Aidha, alisema kwa mwaka 2017 kulikuwa na makosa 902, watuhumiwa 1,578 walikamatwa kati yao 1,485 ni wanaume na 93 ni wanawake.

"Mwaka 2018 makosa yalikuwa 702, watuhumiwa 886 walikamatwa kati yao 796 ni wanaume na wanawake 90," alisema.


Hata hivyo, alisema mwezi Januari hadi Machi, mwaka huu, jumla ya makosa ni 133 na watuhumiwa 174 kati yao 162 ni wanaume na 12 ni wanawake.

Kuhusu dawa za mashambani, Masauni alisema mwaka 2016 jumla ya makosa yalikuwa 10,375 na watuhumiwa walikuwa 26,031, huku mwaka 2017 kulikuwa na makosa 8,956 na watuhumiwa walikuwa 12,529.

"Kwa Januari 2019 hadi Machi makosa ni 1,842 kati yao watuhumiwa wanaume ni 2,340 na wanawake ni 202. Watuhumiwa baadhi wamepelekwa mahakamani na wengine upelelezi wa mashauri yao unaendelea na uko kwenye hatua tofauti," alisema.

Kadhalika, alisema Jeshi la Polisi kupitia programu ya kuzuia uhalifu limeendelea kutoa huduma ya urekebishaji kwa waathirika wa dawa za kulevya.

"Kwa kutumia vikundi mbalimbali kama vya michezo chini ya miradi ya kuzuia uhalifu kama vile familia yangu haina mhalifu na klabu za usalama wetu kwanza," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wizara itangaze masoko ya madini nje ya nchi

**Novatus Makunga,**
ARUSHA

WIZARA ya Madini imeshauriwa kuyatangaza nje ya nchi masoko ya madini yanayofunguliwa kwa kasi katika mikoa mbalimbali.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji wa Madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justine Nyari, wakati wa uzinduzi wa soko la kimataifa la madini la Arusha.

Alitaja wanunuzi wakubwa wa madini ya vito vikiwamo tanzanite kuwa ni pamoja na Marekani, Ujerumani, China na Hongkong.

"Huko kote kuna minada ya madini inafanyika mfano pale Tucson, Marekani hivyo ni vyema hao wote wakaja nchini kununua madini katika masoko yetu," alisema Nyari.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliiomba Wizara ya Madini kuuruhusu mkoa huo kuendelea kufanya maonyesho ya madini ya kimataifa kutokana na kuwa kitovu cha biashara hapa nchini.

Gambo alisema pamoja na hatua hiyo pia wizara hiyo isaidie mchakato wa kujenga kituo kikubwa na cha kisasa cha madini katika Jiji la Arusha.

"Wenzetu wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) walishatenga eneo la kutosha miaka mitano iliyopita kwa ajili ya kujenga kituo cha madini," alikumbusha Gambo.

Akizungumza kabla ya kuzindua soko hilo, Waziri wa Madini, Dotto Bitego, alisema wizara yake haina pingamizi la kufanyika kwa maonyesho ya madini katika mji wa Arusha.

Hata hivyo, alisema kuwa tayari mkoa wa jirani wa Manyara ulishatenga eneo maalumu la uwekezaji (EPZD) jirani ni migodi ya madini ya Mirerani wilayani Simanjiro kwa ajili ya maonyesho ya madini.

"Wizara haina pingamizi kwa yeyote atakayewahi ruksa. Kama Manyara wakiwa na kasi sawa au nyinyi Arusha sisi tunachotaka ni pato la madini liongezeke," alisema.

Aidha, Biteko alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha kufanya mkutano wa madalali wa madini kwa lengo la kukata leseni ya shughuli yao ya ununuzi na uuzaji wa madini.

"Leseni za mabroka (madalali) haizidi Sh. 250,000 kwa mwaka, lakini idadi kubwa wanafanya shughuli zao bila ya leseni, hivyo Mkuu wa Mkoa waite uwaelimishe," alisema Biteko.

Waziri alitoa mwezi mmoja kwa biashara zote za madini kuhama kutoka mitaani na kufanyikia katika eneo la soko hilo la kimataifa lililoko katika barabara ya Old Moshi.

"Hii ni kwa mujibu wa sheria ni makosa mtu akikutwa anafanya biashara ya madini katika eneo lisilotambulika na tutamchukulia hatua kwani alikuwa na njama ya kufanya utoroshaji," alionya Waziri.

Alisema kuwa masoko hayo yameanzishwa kwa lengo la kuondoa urasimu na kurahisisha ufanyikaji wa biashara ya madini ambapo yatakuwa yanafanyiwa uthaminishaji hapo hapo badala ya kuhangaika hadi Dodoma.

Kwa upande mwingine Biteko alisema kuwa tangu eneo la Mererani lijengwe ukuta kiasi cha madini ya tanzanite yanayopatikana kimeongezeka na kufikia kilo 949 yakiwa na thamani ya Sh. bilioni 2.7 kutoka kilo 147.7 yenye thamani ya Sh. milioni 943 kwa mwaka 2017.

## CCM yataka mshikamano kuchukua majimbo yote

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, kimewataka wanachama wake kuwa wamoja na wenye mshikamano kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji.

Pia waendeleze mshikamano huo kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2020, ili kuyarudisha majimbo ya upinzani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Arumeru ya Kijani, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Lotha Sanare, alisema ni muda maalumu kwa wanachama wa chama hicho, kuwa kitu kimoja ili kushinda uchaguzi wa mwaka huu na ule unaokuja.

Alisema Wilaya ya Arumeru kuna madiwani 14 wa upinzani na madiwani 13 wa CCM, hivyo wana jukumu zito la kurudisha nafasi hizo ndani ya chama hicho.

"Tunaomba vijana mjitahidi katika kupata viongozi bora kwa sababu wilaya ya Arumeru ni ya muhimu kwetu kutokana na kuwa na wapigakura wengi," alisema Sanare.

Alisema bila ya kuwa na umoja na mshikamano chama hicho, kitayumba hivyo ni jukumu la chama kuwaandaa vijana kuwa kitu kimoja kwa maslahi ya chama hapo baadaye.

Sanare alisema katika uchaguzi wa mwaka 2015, Arumeru ni miongoni mwa majimbo hapa nchini walimpa Rais kura kidogo, na vyama vya upinzani vikipata kura nyingi hivyo aliwataka wanachama kutokurudia kosa walilolifanya katika uchaguzi uliopita.

"Kilichotokea katika uchaguzi uliopita kiwe fundisho na tusirudie makosa tena kikubwa kuhakikishe tunajipanga kwenda kushinda uchaguzi," alisema Lotha.

Mwenyekiti wa CCM wilaya hiyo, Simon Saning'o, alisema lengo la kuzindua kampeni ya Arumeru ya Kijani ni kuwaunganisha vijana ndani ya wilaya hiyo.

Alisema Arumeru ya kijani imelenga kuwahamasisha vijana kurudisha nafasi zote walizopoteza katika uchaguzi uliopita kuanzia ngazi za vijiji, vitongoji, kata hadi ngazi ya jimbo.

"Umoja wa Vijana CCM Wilaya ya Arumeru tumekataa makundi, ili kuimarisha chama kuelekea uchaguzi ujazo," alisema.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Anna Msuya, chama hicho kinawategemea vijana kama nguzo muhimu ya kukiimarisha chama.

"Ushindi wa chama chochote duniani kina tegemea makundi ya vijana na wanawake," alisema Anna.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, akifurahi na wananchi wa Kijiji cha Orkirungrung, Kata ya Edonyoengijape, baada ya kumkabidhi zawadi ya kondoo juzi, kutokana na utumishi uliotukuka kwao. **PICHA:**

## Wazazi, walezi wafunze watoto kufichua uovu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZAZI na walezi wamehimizwa kutoa elimu kwa watoto itakayowawezesha kufichua vitendo viovu wanavyofanyiwa na kufanikisha watuhumiwa kuchukuliwa hatua.

Mwakilishi wa Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) ambaye pia ni msajili wa wanafunzi wa TICD, Godfrey Meliyo, wakati akizungumza kwenye kongamano la wanafunzi wanaozunguka taasisi hiyo.

Kongamano hililenga kujadili na kuzungumza changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto kwenye jamii wanazoishi.

Meliyo alisema kongamano hilo limelenga kuwajengea uwezo na kutoa elimu kwa watoto hao, ili waweze kuzifahamu haki zao za msingi na kujua sehemu sahihi ya kutoa taarifa za matukio wanapofanyiwa ukatili.

Meliyo alisema kuwa, uwepo wa mila na desturi katika jamii zinazowazunguka zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa jamii kushindwa kubadilika na kuzielewa ipasavyo haki za watoto hao.

"Kwa kweli serikali imeendelea kujenga mazingira mazuri kwa watoto ikiwamo kuwapo kwa sheria ya mwaka 2009 inayohakikisha haki za watoto zinazingatiwa, sambamba na kutengeneza mazingira bora ya elimu yanayotoa elimu bure kwa kila mtoto," alisema Meliyo.

Aidha, Mkuu wa Idara ya Jinsia na Maendeleo wa TICD, Dickson Lukumay, alisema taasisi hiyo imeamua kuwakutanisha watoto kutoka shule zinazozunguka chuo hicho kuwajengea uwezo wa kutambua changamoto zao na kuzitolea taarifa katika vyombo vya dola.

Lukumay alisema kuwa, kupitia kongamano hilo watoto hao watakuwa jasiri kueleza changamoto zao wanazokutana nazo na kutoa taarifa sehemu husika na mwisho wa siku kuweza kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili watoto hao.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki kongamano hilo, walisema wamekuwa wakikutana na changamoto mbalimbali katika jamii ambazo huwawia vigumu kuzungumza.

Aidha, waliiomba serikali na wadau mbalimbali waongeze juhudi katika kuwalinda na kuwajali watoto hao dhidi ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa katika jamii.







Mratibu wa Mradi wa kuwawezesha watoto wa kike wa GEP, katika Wilaya ya Moshi, Immaculatha Mworia (aliyesimama), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mvuleni juzi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Viongozi Same waonywa kumaliza kesi za mimba

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI imewapiga marufuku baadhi ya viongozi wa makundi ya kijamii, vitongoji na vijiji wilayani Same, kujadili na kusuluhisha kesi zinazohusiana na wanafunzi kupewa ujauzito ama kuolewa katika umri mdogo.

Aidha, imetaka Jeshi la Polisi na Mahakama kutenda haki katika kushughulikia mashauri yanayohusu masuala hayo kwa kuepuka vitendo vya rushwa bali sheria ifuate mkondo wake.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa masuala ya jinsia, haki za mtoto wa kike iliyoandaliwa na Shirika la World Vision ili kupambana na mimba na ndoa za utotoni nchini.

Alisema kitendo cha kufanya usuluhishi kwa masuala ambayo yanahitaji mkondo wa kisheria, huku wazazi na walezi wakipewa fedha au fidia ni kumnyima mtoto wa kike haki yake ya msingi ya kupata elimu na kutimiza ndoto zake maishani.

Senyamule alisema katika hali isiyo ya kawaida zaidi ya wanafunzi 95 wa shule za msingi na sekondari wamepewa mimba kwa kipindi cha miezi 6 wilayani Same, jambo lililosababisha kukatishwa masomo yao. Kwa upande wake mratibu wa masuala ya jinsia, utetezi na kampeni kutoka Shirika la World Vision, Jesca Ndang'a, alisema kampeni hiyo itafanyika kwa miaka mitano kuunga mkono juhudi za serikali kupinga ndoa za utotoni pamoja na kutimiza malengo ya maendeleo endelevu hususani elimu.

Alisema katika kampeni hiyo watazielimisha familia na jamii kwa ujumla kuepuka vitendo vya ukatili na kuwapa watoto hususani wa kike fursa ya kupata elimu.

Kwa upande wao baadhi ya wadau Ezekel Idrisa na Christina Mmanda wametaka serikali, viongozi wa dini na wanaharakati kwa ujumla kuongeza kasi katika kuielimisha jamii kuhusu athari za mila na utamaduni zilizopitwa na wakati ambazo zinaruhusu ndoa za utotoni.

# Wadau wataka wakalimani taasisi za ulinzi, usalama

**Na Mary Mosha,** HAI

CHAMA cha Viziwi Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjro (Chavita), kimeiomba serikali kuwaajiri wakalimani katika kila kitengo ili kuwasaidia watu wenye ulemavu wafikapo katika taasisi za vyombo vya ulinzi na usalama.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika kongamano la uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya alama kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama na Mratibu wa Chavita Wilaya ya Hai, Pulcaria Aloyce.

Alisema watu wenye ulemavu wa kusikia wanakabiliwa na changamoto wanapofika katika taasisi hizo kama kwenye vituo vya polisi, mahakamani, magerezani na mabaraza ya sheria, hivyo bila kuwapo kwa mkalimani wanakosa haki zao kwa kushindwa kujieleza na kupatikana kwa ushahidi sahihi.

"Tunaiomba serikali kuangalia namna ya kuajiri mkalimani wa lugha za alama katika vyombo vya ulinzi na usalama ili waweze kupata tafsiri mara wanapofika katika vituo hivyo. Pia wakati wa utoaji wa ajira tunaomba wawakumbuke watu wenye ulemavu ili kupatikana mkalimani mmoja katika kila halmashauri ili kurahisisha mawasiliano," Aloyce.

Alisema jukumu hilo ni vyema likasimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, ambayo inahusika na kusimamia masuala ya ulinzi na usalama. Akifungua kongamano hilo Mkuu wa Wilaya, Lengai Ole Sabaya aliyewakilishwa na Ofisa Tarafa ya Kata ya Masama, Nsajigwa Ndagile, alisema watu wenye ulemavu ni binadamu kama walivyo wengine na wanahitajika kupewa huduma zote kama walivyo raia wengine wote wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa sasa tutaishauri serikali kuangalia namna ya kuweka ajira za wakalimani katika kila wilaya, lakini kwa sasa tunawaomba mwendelee kutoa mafunzo ya alama ili watendaji wa idara mbalimbali wapate mafunzo ya alama wawahudumie watu wenye ulemavu," alisema Ndagile.

Kwa upande wao baadhi ya washiriki akiwamo Inspekta wa Jeshi la Polisi katika wilaya hiyo, Zacharia Shabo, alisema mafunzo hayo yataweza kuwasaidia baadhi ya askari kufahamu lugha za alama zitakazosaidia kuwahudumia watu wenye ulemavu wanapofika katika kituo hicho.

"Ni kweli wapo baadhi ya walemavu ambao wakifika katika kituo cha polisi unaanza kubuni ili kuwapa huduma lakini kwa baadhi ya askari wetu kupata mafunzo kunaweza kusaidia mawasiliano kuwa rahisi zaidi," alisema.

Naiman Akyoo ni Mkaguzi Msaidizi wa Magereza kutoka Gereza la Karanga, aliiambia Nipashe kuwa licha ya kazi yao kuwahifadhi wahalifu, lakini kuna changamoto ya mawasiliano, hivyo mafunzo hayo yataleta mabadiliko.

Aidha, Hakimu wa Mahakama ya Bomang'ombe, Regina Samwel, alisema watu wenye ulemavu wamekuwa wakifika kutoa ushahidi katika mahakama hiyo na kuwataka waandike hali ambayo imekuwa ngumu kwao.

"Ambacho tumebaini kuwa watu hawa hawapendi kuambiwa waandike, lakini kutokana na kukosa wakalimani tunateseka kuwaelewa na wakati mwingine tunatumia nguvu kubwa ili kubaini nini alichotamani kukisema, lakini ikiwa tutapata mafunzo haya ya alama, yatatusaidia kufanya kazi kwa uhakikika bila kubaki na mashaka," alisema Hakimu Samwel.

# Vijana waonywa kuacha kulalamika

**Na Paul William,** MOSHI

VIJANA wametakiwa kujitambua kuwa wana jukumu kubwa la kuilinda na kuendeleza nchi dhidi ya maadui wa nje na ndani na kuachana na tabia za kulalamika.

Hayo yalisema na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Kheri James, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Kilimanjaro ya Kijana, ulliofanyika jana.

James alisema kuwa, vijana wanajukumu kubwa la kushirikiana na serikali katika kuwaibua wahalifu na mafisadi wakiwamo wanaofanya biashara haramu za uuzaji wa dawa za kulevya ambapo huathiri kizazi cha sasa na cha baadaye.

"Kijana unaingia katika mitandao ya kijamii unakuta mtu anaichafua serikali au viongozi wako unakaa kimya, badala ya kumjibu kwa hoja. Utakuwa si uzalendo maana vijana tunapaswa kuilinda nchi yetu na maadui wote wasioitakia mema," alisema James.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa, kijana anapoona mtumishi wa serikali anaihujumu nchi halafu akakaa kimya badala ya kutoa taarifa atakuwa miongoni mwa wahujumu uchumi.

Mjumbe huyo wa Kamati Kuu alisema kuwa, vijana wengi wamekuwa wakiongoza katika kulalamika na kuwataka kubadilika kwani serikali ya awamu ya tano imeonyesha kuwa na imani kubwa na vijana na kutoa fursa nyingi, huku ikiwataka kuzichangamkia.

"Jukumu la serikali ni kuwatengenezea vijana fursa na kazi ya vijana ni kuchangamkia fursa si kulalamika kwani wasipowezeshwa kundi la walalamikaji halitaisha hivyo nitoe wito kwa wakurugenzi kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya vijana," alisema James.

James alisema kuwa, lengo la kuzindua mkakati wa kijani ni kuwaambia vijana serikali za mitaa ni nini pamoja na kuwahamasisha kugombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, huku akitumia pia nafasi hiyo kuwataka vijana wasomi kugombea nafasi za uongozi kwenye serikali za mitaa.

Alisema moja ya sababu zinazowaangusha vijana wa CCM mkoa wa Kilimanjaro ni kurudi nyuma, huku vijana wa Chadema wakienda mbele na kuwataka kubadilika ili kuhakikisha wapinzani hawapati nafasi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 18, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 15


Shinyanga yaja na sheria ndogo ili kutokomeza vifo vya uzazi

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

Daphne Selfe mwanamitindo mzee duniani



# Wakurya na mbinu mpya za ukeketaji

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# FAHAMU NAMNA YA KUPATA ‘LOSS REPORT’ KWA NJIA YA MTANDAO (ONLINE)

‘LOSS REPORT’ ni taarifa ya upotevu wa mali au nyaraka ambayo hutolewa na Jeshi la Polisi katika vituo vya polisi mara mwananchi anapotoa taarifa ya upotevu wa mali katika Kituo cha Polisi, ili aweze kupata msaada wa kuipata mali yake au kupewa nyingine kama vile kitambulisho na namba ya simu.

Jeshi la Polisi nchini, katika kuhakikisha linarahisisha upatikanaji wa huduma ya ‘loss report’, mnamo mwezi Mei, 2019 lilianzisha mfumo wa kutoa taarifa ya upotevu wa mali (Loss Report) kwa njia ya mtandao kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kwa sasa huduma hii imeenea nchi nzima kupitia tovuti ya loss report ambayo https://lormis.tpf.go.tz.

Akielezea mfumo huo, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, (SACP) David Misime, alisema kuwa Lormis ni kifupi cha Loss Management Information System.

Mfumo huu ulioanzishwa na Jeshi la Polisi utamwezesha mwananchi kutoa taarifa za upotevu wa mali au nyaraka kwa kupitia mtandao na kuweza kupata ‘loss report’ bila kufika Kituo cha Polisi, isipokuwa kwa anayetoa taarifa ya upotevu wa kitabu cha kumiliki silaha, kadi ya gari, hati ya kiwanja au shamba, huyu itamlazimu kufika kituo cha polisi.

“Wananchi mtumie mfumo huu kwani unaokoa muda na ni wa uhakika na unarahisisha upatikanaji wa huduma ya loss report.” SACP Misime alisema.

Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha mfumo huu ili kuitikia wito uliotolewa na serikali kuwa ifikapo Juni 30, 2019 taasisi zote zinazokusanya maduhuli ya serikali ziwe zimefanya hivyo kwa njia ya kielektroniki kupitia GePG - Government Electronic Payment Gate way.

Hivyo kupitia mfumo huo mwananchi anaweza kutoa taarifa ya kupotelewa mali au nyaraka kwa kutumia kompyuta au simu yenye ‘internet’. Taarifa hiyo inaweza kutolewa akiwa mahali popote pale ilimradi awe na kifaa cha kielektroniki chenye mtandao atakachotumia kutolea taarifa.

Ili kutoa taarifa bila kufika kituoni inambidi mwananchi kutembelea tovuti ambayo nimeitaja awali https://lormis.tpf.go.tz inayopatikana kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Akishaingia kwenye tovuti atabonyeza kitufe cha “Sajili Mali Iliyopotea” na ataendelea kujaza fomu atakayoipata. Baada ya kujaza fomu hiyo atatakiwa kufanya malipo.

Aidha, mfumo huu wa malipo wa loss report unaowawezesha wananchi kulipa malipo hayo kupitia mfumo wa kielektroniki yaani Government electronic Payment Gateway (GePG) unapatikana kwenye mitandao yote ya simu na kwenye benki.



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, (SACP) David Misime. **PICHA: JESHI LA POLISI**

Mwananchi anapojaza fomu ya Loss report kwenye mtandao atapata namba ya malipo (Control number) ambayo kupitia tovuti hiyo ya polisi inaanzia na 99108 na kuendelea/ kufuatiwa na namba nyingine.

Endapo mwananchi ataamua kufanya malipo kupitia benki, anachotakiwa ni kwenda na namba ya malipo (control number) na hapo watamsaidia kufanya malipo.

Kama mwananchi atatumia mitandao ya simu za mkononi atakapoandika kodi ya namba ya kufanyia miamala ya fedha ya kampuni ya simu, baada ya hapo atachagua namba 4(lipa bili), halafu atachagua namba 5 (Malipo ya Serikali) na kisha atainգiza namba ya malipo (Control number) yake na kulipa kiasi cha 500/=

Kwa wale wananchi waliopoteza laini za simu, kadi za benki au vitambulisho na kujaza maombi yao kwa kutumia kadi zao za NIDA au namba ya NIDA hawahitajiki kwenda Kituo cha Polisi kwani mfumo huu wa Loss report umeunganishwa na mfumo wa NIDA ambao una uwezo wa kuthibitisha taarifa za vitambulisho hivyo moja kwa moja (online).

Kwa maana hiyo mwananchi mwenye kitambulisho cha NIDA au namba na akawa amepoteza laini za simu ana uwezo wa kujaza fomu online na kupata loss report yake online.

Kwa wale ambao watatumia vitambulisho vingine na kujaza fomu ya loss report watahitajika kufika Kituo cha Polisi ili kufanya uthibitisho.

Kufika Kituo cha Polisi ni kwa sababu zifuatazo:- Moja ni ili Polisi waweze kuthibitisha kwamba aliyetoa taarifa ni yeye kutokana na kwamba kitambulisho alichotumia hakijaunganishwa na hakitumiwi na watoa huduma wengi kama cha NIDA.

Aidha, wengine wanaotakiwa kufika kituoni ni wale waliopoteza mali zikiwamo vitabu vya kumiliki silaha, kadi za gari na hati za nyumba au mashamba hizi zinahitaji uchunguzi wa polisi ufanyike kabla ya ‘Loss Report’ haijatolewa kwa mhusika.

Pia ambao wanatakiwa kuendelea kutoa taarifa zao katika vituo vya polisi ni wale ambao hawana simu au kompyuta zenye ‘internet’ itakayowezesha kutoa taarifa ya kupotelewa na mali au nyaraka kwa njia ya mtandao (online).

Kwa wananchi wa aina hii, wakuu wa vituo na wahasibu wameshapata mafunzo na maelekezo ya namna ya kuwahudumia.

Mfumo huu wa kulipia kwa njia ya mtandao (online) na kupata loss report kama nilivyosema tulianza na Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, napenda kuwajulisha kuwa mfumo huu unatumika kwa nchi nzima sasa.

Hivyo ninapenda kuwapa taarifa watoa huduma za mawasiliano kuwa kuanzia sasa wawape huduma wananchi wote wanaofika kwao wakiwa na loss report ya kielektroniki.

Watoa huduma pale watakapokuwa na mashaka wanaweza kuthibitisha/ kuhakiki kama Loss report ya mwananchi ni halali au ya kughushi kwa kutumia njia mbili:-

Njia ya kwanza ni kutembelea tovuti ya loss report ya Jeshi la Polisi ambayo ni https://lormis.tpf.go.tz na kwenda kwenye kitufe cha “Angalia Ripoti yako” hapo ataingiza namba ya malipo (Control Number) ambayo atapewa na mwananchi pamoja na namba ya kitambulisho chake, ripoti ikitoka itakuwa ni sahihi na isipotoka itakuwa ni ya kughushi.

Njia ya pili, kwa wale watoa huduma ambao wana mifumo ya kielektroniki na wangependa kujiunga na mfumo huu kupitia ‘Application Program Interface’ (API) ambayo itaweza kuwaunganisha na hapo wataweza kuwahakiki wateja wao kwa njia ya kielektroniki bila ya kufika au kutembelea tovuti yetu.

Ili kupata hii API wawasiliane na Mkuu wa Tehama wa Jeshi la Polisi kwa barua pepe gabriel.mkungu@tpf.go.tz, au incharge wa kitengo cha mifumo ya TEHAMA (godfrey.kapinga@tpf.go.tz).

***Imetolewa na:-***
***Kitengo cha Uhusiano,***
***Makao Makuu ya***
***Jeshi la Polisi,***
***Dar es Salaam,***
***habariphq@gmail.com***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

### Ukicha kutajwa hutotenda jambo

UKIOGOPA kusemwa na watu ufanyapo jambo hulifanyi asilani. Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayedhamiria kulifanya jambo fulani kisha akawa anaogopa wanavyosema watu wengine.

Kwa miaka 20 na ushei nimekuwa nikikosoa maneno yanayotumiwa vibaya na waandishi wa magazeti ya Kiswahili humu nchini. Lengo ni kuwaelimisha waandishi maana halisi (-enye dhati ya asili) ya maneno na jinsi ya kuyatumia katika uandishi. Niliamini watakapofanya hivyo, pia itakuwa funzo kwa wasomaji wasiojua maana ya baadhi ya maneno na jinsi ya kuyatumia.

Katika hilo, baadhi ya wasomaji wa makala zangu za ‘Tujifunze Kiswahili’ kutoka Kenya wamenitumia ujumbe wa simu na barua pepe (e-mail) wakishukuru kujua maana ya baadhi ya maneno na matumizi yake. Hii yadhihirisha “Penye miti hapana wajenzi” yaani panapokuwa na miti mingi aghalabu hapana wa kuitumia. Methali hii huweza kutumiwa kupigia mfano mahali ambapo pana vitu fulani lakini walioko mahali pale hawajui thamani yake!

Tatizo la baadhi ya waandishi wetu ni kutumia maneno ya mitaani kwa dhana kuwa ni maneno ‘mapya’ ya Kiswahili. Kweli ni mapya kwa wanaofuatilia uhalisia na chimbuko la lugha ya Kiswahili lakini si halisi, hivyo si sahihi kuyatumia. Hali hiyo hufanya waandishi kutoandika mtiririko mzuri wa Kiswahili!

Mfano: “Hii ni mara ya pili kwa mtendaji huyo mkuu wa CCM kuwaonya wanachama wanaovizia kumridhi Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein ambaye anatarajia kumaliza mihula miwili ya urais mwakani.”

Nazungumzia maneno mawili ya sentensi hiyo hapo juu, yaani ‘wanaovizia kumridhi.’ Maana ya ‘vizia’ ni jificha mahali kwa nia ya kushambulia ghafla; kitendo cha kusubiri kwa siri ili kumkamata mtu au mnyama; otea. ‘Ridhi’ ni kitendo cha mtu kukubali jambo kwa hiari; ridhia. Hao wanaosemwa ‘wanavizia kumridhi’ Rais wa Zanzibar, ‘hawamvizii’ wala ‘kumridhi’ kwani maneno hayo mawili hayaendani na maana halisi ya ‘vizia’ kama lilivyo neno ‘ridhi’ lisivyoendana na habari ya mwandishi. Kila moja lina maana tofauti na aliyoandika mwandishi kama nilivyoyatolea ufafanuzi hapo juu.

Sentensi ingeandikwa: “Hii ni mara ya pili kiongozi huyo wa CCM anawaonya wanaojiandaa (sio wanaomvizia) kugombea (sio kumridhi) nafasi ya Rais Shein baada ya muhula wake wa pili.”

Hata kupanga sentensi kwa mtiririko mzuri unaoeleweka, siku hizi ni tatizo kwa baadhi ya waandishi: “Maandamano hayo ambayo yaliyoanzia Tazara yalikuwa pia ni kwa ajili ya kuombea taifa amani.” Mwandishi hakuwa na sababu ya kutumia neno ‘ambayo. Kwa jumla sentensi haikupangwa vizuri.’

Ingeandikwa: “Maandamano hayo yaliyoanzia (nimeacha neno ‘ambayo’) Tazara pia yalihusu kuliombea taifa amani.”

“Akizungumza na ... (jina la gazeti) jana Kamishna wa Polisi, Athuman, alisema baada ya agizo walilopewa na Rais Magufuli kuhusiana na tukio hilo, utekelezaji wake ulianza mara moja.”

‘Husiana’ ni kuwa na uhusiano wa damu, kuwa na fungamano la kirafiki. ‘Husika’ ni mtu kuwa na mamlaka kwenye jambo; shiriki katika kitendo fulani. ‘Husisha’ ni kumwingiza au kumshirikisha mtu katika jambo ili aonekane naye anahusika; fungamanisha. ‘Husu’ ni husiana au fungamana na jambo; toa hisa kwa, toa fungu kwa; lazimika kufanya jambo; lazimu.

Kwa hiyo sentensi inayomtaja Kamishna wa Polisi na Rais Magufuli, neno ‘kuhusiana’ halikutumika kwa usahihi. Mwandishi alipaswa kutumia neno ‘husu’ na kuandika: “ ... Kamishna wa Polisi, Athumani alisema baada ya agizo la Rais Magufuli kuhusu tukio hilo, utekelezaji wake ulianza mara” (yaani bila kukawia). “Mkali wa Bocco mzuka kama wote” ni kichwa cha habari kwenye moja ya magazeti yetu ya michezo. ‘Mzuka’ ni neno nililoelezea maana yake mara nyingi lakini ni kama kumpigia mbuzi gitaa! ‘Mzuka’ ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo. “Mkali wa Bocco mzuka kama wote” msomaji anaelewa nini?

Chini ya kichwa hicho iliandikwa: “Meddie Kagere ndiye aliyeibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu baada ya kutupia kambani mabao 23, lakini straika anayemfuata na kinara kwa wazawa ni Salim Aiyee wa Mwadui, unaambiwa jamaa kwa sasa ana mzuka kama wote huko mgodini.”

Maana ya ‘tupia’ ni kitendo cha kuweka kitu juu ya kingine kwa kurushiarushia mahali mbalimbali kama vile ufuta juu ya mkate. Kitendo cha kuweka nguo begani au kichwani. ‘Kamba’ ni neno lenye maana mbili: Ukambaa mnene unaotengenezwa kwa kupindwa na kuziunga nyuzi pamoja. Hapa twapata methali isemayo ‘Ukuukuu wa kamba si upya wa ukambaa.’ Pili ni mnyama mdogo wa baharini mwenye magamba laini na miguu mingi ambaye huliwa.

‘Goli’ kwa muktadha huu, ni nguzo maalumu aghalabu zenye nyavu zinazochomekwa kwenye viwanja vya michezo kama vile kandanda, kuwa ni sehemu ya kuingizwa mpira unaohesabiwa ushindi. Pia ni pambo la kike linalofanana na bangili, livaliwalo mkononi au mguuni.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

## NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Shinyanga yaja na sheria ndogo ili kutokomeza vifo vya uzazi

## • Kutoza faini wajawazito wanaojifungulia nyumbani



Wadau wa afya mkoani Shinyanga wakiwa katika kikao cha kutunga sheria ndogo za kutokomeza vifo vya uzazi. **PICHA: MARCO MADUHU**

VIFO vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi bado vinaendelea kuwa changamoto mkoani Shinyanga.

Hiyo inatokana na baadhi ya wajawazito kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati, kwa kutohudhuria kliniki na hivyo kujifungulia nyumbani ama kwa wakunga wa jadi.

Kitendo hicho kimeendelea kuwa moja ya changamoto zinazosababisha vifo vitokanavyo na uzazi mkoani humo kutotokomezwa licha ya kupungua.

Sasa serikali ya mkoa wa Shinyanga imekuja na mikakati ya kutokomeza tabia ya wajawazito kutohudhuria kliniki na kuendekeza wakunga wa jadi.

Mkakati mmojawapo ni kutunga sheria ndogo ambazo zitawabana wajawazito kuhudhuria kliniki kwa wakati pamoja na kujifungulia kwenye vituo vya afya.

Kwamba kwa watakaobainika kwenda kinyume na sheria hiyo, basi watatozwa faini ya shilingi 20,000.

MGANGA MKUU

Dk. Rashid Mfaume, ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.

Anasema bila ya utungwaji wa sheria ndogo za kuwabana wajawazito kuhudhuria kliniki na kujifungulia hospitali kwa lazima, kamwe vifo vitokanavyo na uzazi mkoani humo havitaweza kutokomezwa.

Anasema wao kama wadau wenye wajibu mkubwa wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi mkoani Shinyanga, wameona ni vyema wakabuni mbinu ya kuvikomesha kabisa.

"Na ndiyo maana tumekuja na mikakati hii ya sheria ndogo zitakazolazimisha wajawazito kuhudhuria kliniki na kwenda kujifungulia hospitalini," anasema.

MAPENDEKEZO YA SHERIA

Dk. Mfaume anataja mapendekezo ya sheria hizo ndogo ambazo zitatungwa na kuanza kutumika kuanzia ngazi ya kijiji kuwa ni pamoja na kuorodhesha wajawazito wote kwenye maeneo husika.

"Baada ya hapo kuwafuatilia kama wanahudhuria kliniki na kuhakikisha wanajifungulia hospitalini, na wale watakaokwenda kinyume basi watatozwa faini ya Sh. 20,000," anasema.

Anabainisha kuwa sheria hizo zitakuwa zikisimamiwa na wenyeviti wa vijiji, ambao ndio wako karibu na wananchi, wakifahamu kaya moja hadi nyingine.

Kwamba wenyeviti hawa pia watakuwa na orodha yote ya wajawazito, na watakuwa wakiwahoji wanafamilia sababu za mjamzito kutohudhuria kliniki kabla ya kuwatoza faini.

"Sheria hizi ndogo ni mapendekezo tu ya awali ambapo zingine zitatungwa huko kwenye ngazi ya kijiji kwa kushirikiana na wanasheria wa halmashauri," anasema na kuongeza:

"Endapo kila mmoja akawajibika kwenye nafasi yake vizuri na kusimamia sheria hizi ndogo, nina uhakika kabisa vifo vitokanavyo na uzazi mkoani hapa vitabaki historia, labda vile tu kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu."

> "Na hiyo inatokana na kutozingatia ushauri ambao wanapewa na wataalamu wa afya na kitendo chao cha kutekeleza mambo yao ya mila na desturi za kizamani na hivyo kujikuta wakipoteza maisha," anasema.

Dk. Mfaume, anasisitiza kuwa vifo vingi mkoani Shinyanga vinatokana na uzembe wa kutopenda kuhudhuria kwenye huduma za kiafya.

Anabainisha kwamba ni pale tu wajawazito wanapokuwa wamezidiwa wakati wakijifungua majumbani ama kwa wakunga wa jadi, ndipo wanaamua kukimbilia hospitali kupatiwa huduma.

"Wakati huo inakuwa tayari wameshachelewa, na wengi wao hufariki dunia kutokana na kuwa wamevuja damu nyingi," anasema.

### MRATIBU HUDUMA UZAZI

Kwa upande wake Joyce Kandolo ambaye ni mratibu wa huduma ya uzazi na mtoto mkoani Shinyanga, anasema mama anapokuwa ameshika mimba anatakiwa kuhudhuria kliniki ndani ya wiki 12.

"Ni ili aanze kupatiwa vipimo na kinga juu ya kulinda ujauzito wake pamoja na kupewa ushauri nasaha ikiwamo kuzingatia lishe bora," anasema.

Joyce afafanua kwamba vifo vingi vya wajawazito mkoani humo hutokana na kuvuja damu nyingi wakati wa kijifungua, kifafa cha mimba, pamoja na kupasuka mfuko wa kizazi.

"Na hiyo inatokana na kutozingatia ushauri ambao wanapewa na wataalamu wa afya na kitendo chao cha kutekeleza mambo yao ya mila na desturi za kizamani na hivyo kujikuta wakipoteza maisha," anasema.

### TAKWIMU ZA VIFO

Joyce anataja takwimu za vifo vya uzazi kwa upande wa kina mama, ambapo mwaka 2017 walifariki kinamama 73, mwaka jana 56 na mwaka huu kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki kinamama 18.

Pia anataja takwimu za vifo vya watoto wachanga ambapo mwaka 2017 walifariki dunia watoto 913, mwaka jana walikuwa 815, na mwaka huu 2019 kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki watoto 218.

"Ili vifo hivi vikome, ni lazima wajawazito wapende kuhudhuria kliniki na kujifungulia kwenye vituo vya afya...wasiendekeze kujifungulia nyumbani na kwa wakunga wa jadi," anasema.

### RC

Zainabu Telack ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anakubaliana na mbinu ya kutunga sheria ndogo za kubana wajawazito kuhudhuria kliniki, lakini pia kujifungulia kwenye huduma za kiafya.

"Zijadiliwe haraka zije kwangu nizibariki ili zianze kufanya kazi," anasema.

Telack anasema ili kumaliza tatizo la vifo vya uzazi mkoani Shinyanga, ni lazima kuachana na tabia ya kubembelezana.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya wamekuwa wakipiga kelele na kutoa elimu ya wajawazito kujifungua kwenye huduma za kiafya,

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA SALOME KITOMARI

# Wakurya na mbinu mpya za ukeketaji

- Binti akipata mimba kabla ya kukeketwa hutupwa mbali ili afe
- Binti ambaye hajakeketwa hazikwi na familia kwani ni mkosi
- Ukoo wa Bwirege maarufu sana kwa mila hii



Mzee wa kimila koo ya Bukira Wangubo Mtongori akitoa elimu juu ya madhara ya ukeketaji katika kijiji cha Kebweye, Kata ya Nyakonga, Wilaya ya Tarime, mkoani Mara.

KUNA mengi yanayoiunganisha dunia kupaza sauti moja katika dhima nzima ya kupigania maendeleo ya binadamu kwenye zama hizi, ilhali haki za makundi tofauti na zaidi yaliyo pembezoni zinapewa kipaumbele.

Miongoni mwa makundi yaliyo pembezoni kwa mujibu ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya mwaka 2016 iliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) ni ya wanawake na wasichana.

Ndiyo maana kwa miongo sasa, dunia imesimama pamoja kutetea haki za wanawake na wasichana dhidi ya ukandamizaji ambao umekuwa ukifanywa kwa kundi hili.

Kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ambao umekuwa ukifanywa dhidi ya wasichana na hivyo kufifisha ndoto zao za kimaisha na pia mchango wao kwa jamii.

Katika Bara la Afrika, Tanzania ikiwamo wanawake na hususani wasichana bado ni waathirika wa ndoa na mimba za utotoni.

Takwimu kutoka vyanzo mbalimbali zinaonyesha kwamba maelfu ya wasichana wanakosa haki ya elimu kwa mfano kutokana na sababu hizo.

Katikati ya madhira hayo, kuna janga la ukeketaji ambalo limepigiwa kelele na linaendelea kupigiwa kelele na dunia hadi sasa ili litokomezwe.

Linapigiwa kelele kwa sababu ya madhara yake kwa wasichana, jamii na dunia kwa ujumla.

Takwimu za Umoja wa Mataifa (UN) zinabainisha kwamba mmoja kati ya wasichana 20, amefanyiwa ukeketaji.

Maana ya takwimu hizo ni kwamba, jumla ya wanawake milioni 200 kote duniani wamefanyiwa ukeketaji kwa maana ya kukatwa, kubadilishwa ama kuondolewa sehemu zao za siri.

## KWA NINI DUNIA INAPAZA SAUTI

Dunia kwa maana ya UN inapaza sauti dhidi ya kitendo hiki kutokana na madhara yake kwa wasichana na wanawake kwa ujumla.

Vyanzo mbalimbali vinataja baadhi ya madhara ya ukeketaji ni pamoja na matatizo ya kimaungo na kiakili ambayo humwathiri mwanamke katika kipindi chote cha maisha yake.

## KWA NINI UNAFANYIKA?

Sasa pamoja na juhudi kubwa za kutokomeza janga hili kuchukuliwa kwenye uga wa kimataifa katika sekta mbalimbali ni kwa nini unaendelea kutendeka, ni swali ambalo wengi wanajiuliza.

Hata hivyo, baadhi ya sababu kubwa zinazotajwa kuwa chanzo cha kuendelea kushamiri kwa ukeketaji hata katika zama hizi za utandawazi ni kukubalika katika jamii, dini, imani potofu juu ya usafi wa mwili na kuhifadhi ubikira.

Na kubwa zaidi kwenye makabila na jamii zinazoendeleza mila hii ni kumwezesha mwanamke aolewe.

Kwamba ameshaingia katika utu uzima na anafaa kuwa mke wa mtu mwenye heshima kimila.

## HALI IKOJE NCHINI?

Yumkini juhudi za wadau yakiwamo mashirika mbalimbali yanayopinga ukeketaji na unyanyasaji wa wasichana na wanawake hapa nchini, zimewezesha serikali kutunga sheria ambazo zinatoa adhabu za faini au kifungo cha hadi miaka 30 kwa anayekamatwa.

Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo ambazo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa mila hiyo katika maeneo mbalimbali nchini, bado ukeketaji unaendelea kufanyika, lakini kwa kificho.

Unafanyika kwa kificho kwa mbinu mpya baada ya serikali kutunga sheria ya kuzuia ukeketaji na adhabu ya hadi miaka 30 kwa mzazi au mlezi atakayekutwa amefanya hivyo.

Kabila la Wakurya lililoko katika mkoa wa Mara, linatajwa kuendeleza ukeketaji likitumia mbinu mpya za kificho.

Linatajwa kuendeleza mila hiyo kwa imani kuwa binti ambaye hajakeketwa katika jamii anahesabika ni laana na mkosi kwa ukoo wake.

## AKIPATA MIMBA

Na inapotokea msichana amepata mimba kabla ya kukeketwa hutengwa na familia au ukoo wake na kutupwa mbali ili afe, mwili wake uoze na kuliwa na wanyama au uishe wenyewe.

## SUALA LA KUZIKWA

Mwili wa binti ambaye hajakeketwa hauzikwi na familia husika kwa kuwa wakifanya hivyo wanaamini kabisa itakuwa ni kukaribisha mkosi kwa familia husika na kuharibu ukoo wao.

Na inapotokea msichana husika amepata mimba, hutengwa na familia au ukoo wake kwa kutupwa mbali ili afe, mwili wake uoze ili uliwe na wanyama au uishe wenyewe.

## VALERIAN MGANI

Valerian Mgani, ni Meneja Mradi wa shirika lisilo la kiserikali la Association for Termination of Female Genital Mutilation (ATFGM), lenye makao yake makuu Masanga, Tarime mkoani Mara, ndiye anayebainisha haya ya jamii ya Wakurya na ukeketaji.

"Mwili wa binti anayefariki ambaye hajakeketwa hauzikwi na familia husika kwani wakifanya hivyo wanaamini kabisa itakuwa ni kukaribisha mkosi katika familia yao na kuharibu ukoo wao," anasema.

Mgani anayabainisha haya kwenye mkutano wa mashirika zaidi ya 12 yanayopinga ukeketaji na unyanyasaji wa wasichana na wanawake yalikutana hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

Mkutano ambao ulizaa umoja wa kuunganisha nguvu nchini kwa minajili ya kukabiliana na mbinu mpya za ukeketaji wa wasichana na wanawake, zinazofanyika sasa.

Mgani anasema kwamba katika kabila hilo la Wakurya ambao bado wanaendeleza mila hiyo kwa siri, ukeketaji hufanyika kwenye mwaka unaogawanyika kwa mbili.

"Lakini ukeketaji na tohara ya majaribio hufanyika mwezi Oktoba na ikitokea binti wa kwanza kufanyiwa amefariki, wazee wa kimila wa ukoo huupaka mwili dawa nyingi wakiamini ni kuondoa mkosi wa kifo kwenye ukoo na kisha huutupa mbali kwenye ukoo mwingine," anasema.

BWIREGE

Mgani anautaja ukoo wa Bwirege kwa Wakurya kuwa ni maarufu sana katika utekelezaji wa mila hii.

"Wameishikilia na hawataki kuiacha, lakini wanafanya mengine ambayo hayana utu ndani yake," anasema.

## YASIYO YA KIUTU

Mgani anatoa mfano wa namna walivyomuokoa binti mmoja wa familia hiyo ya Bwirege hivi karibuni ambaye alipata mimba kabla ya kukeketwa.

Anasema binti huyo alichukuliwa na kupakwa dawa nyingi kwa madai ya kuondoa mkosi kwenye ukoo huo ambayo yalimfanya kuwa kama zezeta.

"Baada ya kumpaka dawa walikwenda kumtupa eneo la Nyamwanga Serengeti karibu na mto Mara... tulipata taarifa kutoka kwenye vyanzo vyetu tukashirikiana na polisi kufuatilia na siku ya pili tulimkuta akiwa kwenye kichaka na upande wa pili kuna wazee wa mila wanafanya mila zao," anasema na kuongeza:

"Kwa kawaida wazee hao baada ya kumaliza mila zao humchukua msichana na kumrusha mto Mara ambako huliwa na wanyama na kupotea... kwa kufanya hivyo wanaamini wameteketeza mkosi ambao ungeweza kuuandama ukoo."

Mgani anabainisha walimchukua binti huyo akiwa hajitambui na kumhifadhi kwenye kituo cha wasichana.

"Na hivi karibuni amejifungua mtoto wa kiume, lakini kazi kubwa sasa itakuwa ni kumuunganisha na familia yake," anasema.

## KIPIGO WASIOTAKA KUKEKETWA

Katika hili, Mgani anatoa mfano wa mabinti wawili waliopigwa na kaka zao kwa kushirikiana na mama zao kwa madai kwamba walikataa kukeketwa na bado wamelazwa hospitalini hadi sasa.

"Sababu za kaka zao kuwashushia kipigo ni ile hofu ya wao kukosa ng'ombe za kuolea kwani hakuna mwanaume anayeoa mwanamke ambaye hajakeketwa," anasema.

## KIFO MJAMZITO ASIYEKEKETWA

Meneja huyo anasema inapotokea binti amefariki kabla ya kukeketwa na alikuwa mjamzito, mwili wake hauzikwi na ukoo husika kwa imani kwamba kufanya hivyo ni kukaribisha mkosi kwenye familia.

"Binti akifa wenye familia hunyamaza... wazee wa mila huupaka mwili dawa za kienyeji ili usiharibike haraka na inapofika usiku vijana huubeba mwili huo na kwenda kuuweka kwenye koo zingine," anasema na kuongeza.

"Wanaweza kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 40 kwa ajili ya kwenda kuutupa... kunapokucha, familia ambapo mwili huo umeachwa nayo husubiri giza liingie, kisha vijana wa familia hiyo nao huubeba mwili huo kwenda kutupa kwingine."

Kwa mujibu wa Mgani, katika kukwepa laana, mwili huo huishia kuachwa porini na kuoza. "Yote hayo yakichagizwa na wazee wa kimila ambao huiaminisha jamii mambo hayo ambayo kimsingi ni unyanyasaji wa mtoto wa kike,"anasema.

## MCHANGO WA NGARIBA

Meneja huyo wa Shirika la ATFGM, anasema katika utafiti wao wamebaini kwamba mila hiyo inaendelea kutokana na kuwa na mahusiano na imani za kishirikina, utajiri na ngariba kupata mali.

Anasema inahusishwa na ushirikina kwa kuwa wanaamini kinyama kinachokatwa kwenye sehemu ya mwanamke kikutupwa kwenye zizi la mifugo, itaongezeka.

"Lakini pia, familia yenye watoto wa kike na kiume hutegemea kupata ng'ombe wengi kutoka kwa watoto wa kike ambao hutumiwa na kaka zao kwenda kuoa kwenye mji mwingine na hivyo familia kutosumbuka kutafuta fedha kwa ajili ya vijana wao kuoa," anasema.

Mgani anasema familia hufurahi kupata mali nyingi kwamba kunapokuwa na watoto wa kike inahesabika ni utajiri na wanapomwangalia mtoto wa kike hawaoni daktari, mwalimu au mfanyakazi wa baadaye bali mifugo ambayo kwao ndio utajiri. Mgani anasema kwenye eneo wanalofanyia kazi kuna ngariba 82 ambao kwa msimu mmoja wa ukeketaji hupata wastani wa Sh. milioni 27 hadi 28 kutegemeana na mabinti ngariba aliowakeketa.

"Ngariba anayepata fedha nyingi hivi kwa msimu mmoja ambao ni mara moja kwa mwaka, ukimwambia aache kazi hii bila kipato mbadala kwake ni ngumu sana," anasema.



Baadhi ya kinamama walioachishwa kazi ya ungariba na kupewa shughuli nyingine ya kuwaingizia kipato.



Wasichana kama hawa wasaidiwe kufikia ndoto zao zikiwamo za kielimu badala ya kuwakeketa ili waolewe. **PICHA: MTANDAO**

## CHANGAMOTO ZINGINE

Kwa mujibu wa Mgani eneo kuwa mpakani ni changamoto kubwa kwa maana jamii ya Kikurya inapoona imebanwa kwa upande wa Tanzania, hukimbilia kutekeleza mila hiyo upande wa Kenya.

Ili kutatua changamoto hii anasema inatakiwa nchi zote mbili kuamua kwa pamoja kushirikiana kuunganisha nguvu ya kupambana na jambo hilo, kwani wakiona wamebanwa upande mmoja wanakimbilia upande mwingine.

Aidha, viongozi wa kimila ambao hunufaika na mila hiyo kwa kupewa ng'ombe na heshima yao kuzidi pale ukeketaji unapofanyika, ni changamoto pia. Anabainisha kuna wakati serikali kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, iliwasainisha makubaliano nao kwamba jamii hiyo itaacha mila hiyo na watashirikiana na wadau pamoja na serikali kuielimisha jamii.

"Lakini viongozi hao wa kimila walipoona msimu wa ukeketaji umekaribia, walienda upande wa Kenya kila mtu kwa sababu zake tofauti tofauti, huku nyuma wakiacha maelekezo ya kukeketa wasichana na wavulana kutahiriwa... tulipowauliza walisema si wao, bali wamefanya wanajamii wenyewe, anasema.

Aidha, anabainisha, wakati wa msimu wa ukeketaji urafiki na wanaopinga suala hilo huisha, kwani vijana wa Kikurya hupakwa dawa za kienyeji ambazo huwafanya kuwa kama vichaa fulani hivi.

"Na ukifanya mchezo wanaweza kukukata mapanga...ikifika wakati huo tunajificha kabisa...hata hivyo wanaopinga kutoka kwenye jamii yao tuliowafundisha, hutumia mbinu kuwaokoa baadhi ya wasichana," anasema na kuongeza:

"Jambo hili ni gumu sana lakini bado tutandelea kuokoa mabinti wanaopitia changamoto hizi."

## MABINTI WAKIMBILIA KANISANI

Akizungumzia juu ya idadi ya mabinti wanaotoroka kukeketwa, meneja huyo anasema mwaka jana zaidi ya mabinti 300 wa upande wa Kenya, walikimbilia kanisani katika usharika wa Kebaroti.

"Walikutwa wakiwa chini ya mti kila mmoja akitokea eneo tofauti akijaribu kuokoa maisha yake kwani upande wa Kenya, mila hiyo haijapigwa marufuku kama Tanzania," anasema.

## WANAVYOSAIDIA

Mgani anabainisha wameunda vikundi vya ngariba na wasichana ambao wameelimishwa na kupewa mtaji wa cherehani ili wafanye shughuli za kuwaingizia kipato mwaka mzima, ikiwa ni pamoja na elimu ya mara kwa mara ya madhara ya ukeketaji.

## LHRC

Kwa upande wake, Ofisa Programu Jinsia, Wanawake na Watoto wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Getrude Dyabene, anasema sheria ya elimu haizuii mtu mzima kukeketwa kwani imemtaja mtoto ni aliye chini ya miaka 18.

Anasema upo umuhimu wa kuwa na sheria ya kulinda makundi yote kwani kinachofanywa sasa na baadhi ya jamii ni kukeketa watoto wa kike waliozidi umri wa miaka 18 na wengine wakiwa darasa la kwanza.

## MKURUGENZI

Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, anasema ili kukabiliana na mbinu za wanajamii katika dhima ya kupinga ukeketaji kunahitajika nguvu ya pamoja ya mashirika na jamii husika, kwani kila siku zinaibuka mbinu mpya za kutekeleza mila hii.

"Mila hii ni sugu kwenye baadhi ya jamii za wafugaji kwani wao wanamuona mtoto wa kike ni mali na si anayetakiwa kwenda shule ili atoe mchango kwa jamii yake," anasisitiza.

# Shinyanga yaja na sheria ndogo ili kutoko

Inaendelea Uk. 15

lakini bado hali inaonekana kuwa ngumu, hivyo lazima nguvu itumike," anasema na kuongeza:

"Pamoja na sheria hizi kuanza kutumika, pia endeleeni kutoa elimu."

Mkuu huyo wa mkoa anasema serikali inajitahidi kuboresha huduma za afya, ili pamoja na mengine kukomesha vifo vya uzazi, lakini anasema anasikitika kwamba wajawazito wanakuwa wagumu kwenda kupatiwa huduma stahiki.

Telack anasema mwaka jana mkoa huo umejenga vituo 11 vya afya na tisa vipo tayari kuanza kutumika.

"Nasikitika pamoja na juhudi hizo zote, tunaonekana kama vile tunacheza," anasema.

**MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko ni miongoni mwa washiriki waliohudhuria kikao cha mapendekezo ya utungwaji wa sheria hizo ndogo za wajawazito.

Anasema licha ya sheria hizo kupitishwa na kuanza kutumika pia wahudumu wa afya nao wanatakiwa wawe na kauli nzuri wanapokuwa wakitoa huduma ya uzazi.

Anabainisha kwamba kumekuwa na malalamiko toka kwa kinamama kuwa hukumbana na lugha za matusi wanapokwenda hospitali na ndiyo moja ya sababu za wao kuamua kujifungulia nyumbani ama kwa wakunga wa jadi, mahali ambapo hakuna matusi.

"Sasa ili sheria hizi ndogo zilete matokeo chanya, ni lazima wahudumu wa afya muachane kabisa na matumizi ya lugha chafu, pale mnapokuwa mkiwahudumia wajawazito… tumieni lugha laini itakayowahamasisha wapende kujifungulia hospitali, ndipo tutafanikiwa kwa asilimia 100,"anasema.

**WAZIRI**

Naye Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee, na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anakemea tabia ya wahudumu wa afya kuendelea kutoa lugha chafu kwa wajawazito pale

## JE, WAJUA?

# Daphne Selfe mwanamitindo mzee duniani



MIAKA 70 kati ya miaka 91 aliyonayo sasa, ameitumia katika majukwaa ya maonyesho ya mitindo ya mavazi duniani.

Hili linamfanya Daphne Selfe, raia wa Uingereza, kushikilia rekodi ya 'modo' mwenye umri mkubwa zaidi duniani, ukilinganisha na warembo wengine wote waliowahi kushiriki fani hiyo.

Alianza rasmi shughuli za uanamitindo mwaka 1945, wakati huo akiwa na umri wa miaka 21 tu.

Tangu wakati huo mpaka sasa amekuwa akifanyakazi ya uonyeshaji mavazi kwenye maonyesho makubwa ya mitindo ya mavazi, huku akihakikisha anadumisha mvuto wa umbo lake la kimitindo kwa kufanya mazoezi ya mwili.

Amekuwa akionyesha mitindo ya mavazi ya aina mbalimbali kuanzia yale ya ndani na mavazi ya aina nyingine kama vile mavazi ya kutokea, ofisini, mavazi ya kiutu uzima na pia amekuwa akialikwa katika halfa kadhaa za kutafuta vipaji vipya vya wanamitindo wanaonyesha mavazi.

Kwa miaka yote 70 ya kuonyesha mavazi majukwaani, mrembo Selfe amekuwa akiifurahia kazi hiyo inayomwingizia kipato kikubwa hasa kwa kuzingatia kuwa umri mkubwa alionao sasa umemwongezea mvuto kwa wapenzi wa maonyesho ya mavazi.

Ameshaonyesha mavazi ya kampuni nyingi kubwa za mitindo duniani kama Vogue na Marie Claire na mwonekano wake ndani ya mavazi ya mitindo mbalimbali yameonyesha kuwavutia vijana na 'wazee



wenzake' kupenda na kununua mavazi ya kampuni hizo.

Kwa mwaka huu alipanda jukwaani mwezi Februari aliposhiriki katika maonyesho ya mavazi ya kampuni za Vogue na Marie Claire.

# UTAFITI

## UTOAJI DAMU: UKWELI KUHUSU NANI ANAWEZA KUCHANGIA DAMU

KUNA masharti mengi yanayoambatana na kutoa au kuchangia damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wanaohitaji.

Lakini pia kuna imani nyingi potofu na mambo yasio ya kweli ambayo watu wanayaamini.

Labda swali la kujiuliza ni kwamba je, kuna masharti ya kuchangia damu? Katika hili kuna mengi ya kubainishwa kutokana na ukweli kuwa shughuli hii imezungukwa na imani mbalimbali potofu.

Kumekuwa na imani potofu kuhusu utoaji damu na ndiyo maana utafiti umefanyika kulibaini hili ikiwamo fikra kuhusu watu wasiokula nyama, kuwa hawawezi kutoa damu.

Wasiwasi unatokana na kiwango cha madini ya chuma (iron), kiini kikuu cha damu mwilini kwamba watu wasiokula nyama hawapati madini haya ya kutosha.

Kwamba iwapo damu yako haina madini ya kutosha, hauwezi kuruhusiwa kutoa damu kutokana na usalama wako.

Hata hivyo, inabainishwa kitaalamu kwamba kama unakula lishe bora yenye virutubisho vya kutosha, basi bila shaka utapata madini ya chuma ya kutosha mwilini.

**WENYE MICHORO (TATTOO), KUTOBOLEWA MWILI**

Hawa wanaweza kuchangia au kutoa damu pamoja na kuwa na michoro ya tatoo au kutobolewa miili yao, tofauti na baadhi ya watu wanavyoamini.

Hata hivyo, kuna sheria kwa maana kuwa ni lazima kusubiri kwa miezi minne kutoka siku waliochorwa tatoo au kutobolewa mwilini, kabla ya kutoa damu.

Na iwapo mtu ametoa damu kati ya miezi minne na mwaka mmoja baada ya kuchora tatoo au kujitoboa mwili, huenda akafanyiwa ukaguzi wa ziada katika kituo cha kutoa damu.

JE, KUNA KIWANGO CHA MWISHO CHA DAMU?

Hapa hakuna sababu ya kuwa na hofu, kwani mtu mzima yeyote ana kiasi cha pointi 10 za damu mwilini.

Hivyo unapotoa mchango wa damu huwa unatumia kama pointi moja, na mwili hufanya kazi kurudisha seli na maji uliyopoteza mwilini.

Kwa kawaida damu uliochangia inarudi mwilini baada ya siku moja.

**VIPI KAMA NI MGONJWA?**

Kwa kawaida mtu anastahili kupona kikamilifu baada ya maambukizi ya aina yoyote angalau siku 14, kabla ya kutoa damu. Na iwapo mtu amekuwa akinywa dawa za antibiotic, inabidi asubiri siku saba baada ya kumaliza kunywa dawa ndipo aweze kuchangia damu.

Na kama mtu anatumia dawa maalum, aulize katika kituo kilicho karibu naye iwapo anaweza kuchangia damu.

SHERIA ZA KUSHIRIKI NGONO

Inawezekana kutoa damu wakati wowote isipokuwa iwapo wewe ni mwanamume ambaye umeshiriki mapenzi ya jinsia moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Kuna sheria kwa wapenzi wa jinsia moja wanaume inayofanya kuwa vigumu zaidi kwao kuchangisha damu.

**SIFA ZA KUCHANGIA DAMU**

Kwa ujumla, unaweza kuchangia damu iwapo una nguvu na afya, una uzito wa kati ya kilo 50 hadi 160 na una umri wa kati ya miaka 17 na 66. Aidha, hata kama una umri wa zaidi ya miaka 70 na umewahi kutoa damu katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

**BBC**

# omeza vifo vya uzazi

wanapokuwa wakiwapatia huduma ya uzazi. Dk. Ndugulile anakemea tabia hiyo alipokuwa mkoani Simiyu kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wakunga Duniani mwaka huu.

Anasema serikali ya awamu ya tano imedhamiria kupunguza tatizo la vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi na ndiyo maana imekuwa ikiboresha huduma za afya pamoja na kutenga bajeti kubwa.

"Nawaomba wahudumu wa afya na wauguzi, wakunga mtoe huduma zinazostahili kwa wajawazito na kuacha kuwatolea lugha chafu ili kuwahamasisha kwenda katika vituo vyetu vya afya, mahali ambapo ni salama na hivyo kupunguza vifo vya uzazi," anasema.

**RAIS**

Na kwa upande wake Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA), Feddy Mwanga, anawataka wauguzi wakunga kuzingatia maadili ya taaluma yao, kwa kutoa huduma stahiki kwa wajawazito ili kupunguza vifo vya uzazi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack.

# UTAFITI: Kuna manufaa makubwa kuzungumza na mtu usiyemjua

KATIKA shughuli zetu za kila siku, tunakutana na watu tusiowajua au kufahamiana nao, iwe ni kwenye magari ya usafiri wa umma, hotelini, kwenye bustani au madukani.

Lakini wengi wetu tunahofia kusema nao kwa kuhofia tutachukuliwa vipi ama tunafikiria huenda tusielewane nao.

Hata hivyo, wataalamu wanasema hakuna haja ya kujitenga na mtu usiyemjua ukikutana naye kwa mara ya kwanza kwa kuzingatia kigezo hicho.

Utafiti wao mpya unaashiria kuwa huenda mara nyingine watu wanapuuza umuhimu wa kutangamana na wenzao lakini mazungumzo kati yao huenda yakawaacha wote wakiwa na furaha.

Huo ni mfano mzuri kuwa kuzungumza na mtu usiyemjua ukiwa njiani kuelekea kazini, kunaweza kuwa na manufaa kwenu nyote kuliko vile mlivyotarajia.

Ili kubaini hilo, watafiti walizungumza na baadhi ya wasafiri katika vituo vya mabasi na treni jijini Chicago nchini Marekani.

Walitaka kufahamu jinsi walivyojihisi walipozungumza na watu wasiojuana nao wakiwa safarini, wakilinganisha na walivyobaki kimya au kufanya kitu kingine.

Baadhi ya wale waliohojiwa walihisi kuwa kuzungumza na watu wasiofahamiana nao kungeliwaweka katika hali ngumu ambayo ingeliwafanya kuonekana wasumbufu au wao wenyewe kukwazika kwasababu hawajui kama majirani zao wangelipendelea kushiriki mazungumzo hayo.

Hata hivyo, walipofanya uchunguzi zaidi kwa kuwapa jukumu hilo watu waliowashirikisha katika utafiti huo, walibaini wale waliozungumza na watu wasiojuana nao walifurahia safari yao.

Utafiti huo ulibaini kuwa karibu asilimia 40 ya wasafiri walikuwa tayari kuzungumza na watu wasiojuana nao.

Kila aliyeshiriki utafiti huo alijaribu kusema na abiria aliyekaa naye na wote waliafiki kuwa walifurahia mazungumzo baina yao.

Hofu kuwa mtu usiyemjua huenda asiwe na haja ya kusema nawe ndio kizingiti kinachotufanya kutoweza kujenga uhusiano na watu wengine zaidi ya wale tunaojuana nao.

Aidha, utafiti unaashiria kwamba hali ya watu kujenga mazingira kuwa mtu mgeni huenda asiwe na haja ya kusema nao kwa kuzingatia mazungumzo ya awali baada ya kusalimiana ni dhana potofu.



Abiria wakiwa katika mazungumzo safarini.

**MAWAZO YA WATU WASIOJUANA**

Uchunguzi mwingine uliofanywa katika magari mengine ya usafiri wa umma pia ulipata matokeo sawa na yale ya awali na walishangaa kujiona wakifurahia kuzungumza na watu waliokutana nao kwa mara ya kwanza.

Umuhimu wa mawasiliano kati ya watu wawili wasiojuana ulibainika pale uchunguzi zaidi ulipofanywa katika chumba cha watu cha kusubiri kupatiwa huduma.

Watafiti waligundua kuwa watu wasiojuana wanaweza kufahamiana kwa njia rahisi sana, wote wakichukulia kitendo cha wao kusemezana kama sehemu ya utu na ustaarabu katika jamii.

Bila shaka, hakuna mtu anaweza kufurahia mtu au watu asiowafahamu wakijaribu kujileta karibu kwa sababu hajui dhamira yao.

Lakini hatua yenyewe ya kumsalimia mwanadamu mwenzako hupokelewa vyema kuliko watu wanavyodhania.

Ni watu wachache huzungumza na watu wasiowajua lakini wengi wao hufurahia kuzungumza nao wakihisi nia yao si mbaya.

Kitu kimoja muhimu ambacho watu hunufaika nacho wakisemezana japo hawajuani ni kuwa, kila mmoja wao anapata fursa ya kubadilishana mawazo na mwenzake pale mazungumzo yao yanapofanikiwa kuendelea baada ya salamu za kawaida. Ikitokea wawe na maoni sawa juu ya jambo fulani hata wakiachana na kila mmoja wao akielekea katika shughuli zake, atasalia na kumbukumbu ya kwamba si yeye peke yake aliye na msimamo fulani kuhusu jambo fulani.

**MSONGO WA MAWAZO**

Kuzungumza na mtu usiyemjua pia wakati mwingine hukuondolea msongo wa mawazo, hali ambayo itakufanya kutulia.

Kwa mfano unapojikuta si wewe pekee unayechelewa wakati mwingine au kuchukua muda mrefu barabarani kutokana na msongamano wa magari.

Wanadamu ni viumbe wanaopenda kutangamana, ndio maana kila mtu ana mtu ambaye anaamini anaweza kusema naye akiwa na furaha, huzuni au msongo wa mawazo.

Mtu au watu hao huwafanya wajisikie wamefarijika.

Badala ya kujitenga ukiwa na matatizo, wataalamu wanashauri ujaribu kadri uwezavyo kuzungumza na mtu hata kama hamjuani, kwani kufanya hivyo kutakuepusha na mawazo mabaya kama vile kujiingiza katika unywaji wa pombe kupita kiasi, hali ambayo itakuwa na athari kwa afya yako.

Kuwa na mahusiano mazuri katika jamii ni moja ya viungo muhimu vinavyotufanya kuwa watulivu na wenye furaha na kwa kiwango fulani huchangia jinsi tunavyojitahidi kutafuta kazi na kama kazi ipo tuweze kutafakari jinsi ya kujiendeleza maishani.

**KUVUNJA UKIMYA**

Kundi la Profesa Epley lilijaribu kulinganisha matokeo ya utafiti wao wa Chicago kwa kufanyia majaribio matokeo hayo kwa niaba ya BBC, jijini London, nchini Uingereza.

Utafiti huo mpya ulihusisha wasafiri 700 wa reli ya Greater Anglia kuingia jijini London.

Watafiti walishirikiana na kampuni za usafiri kutoa taarifa ya mapema kwa wasafiri kuwa wanaendesha kampeni ya kuimarisha utangamano wa kijamii katika vyombo vya usafiri.

Ili kufikia lengo hilo, kampuni za usafiri ziliwashauri wateja wao kusemezana na wasafiri wenzao hata kama hawajuani.

Mpango huo ulijumuisha treni zote za kampuni ya Virgin zinazohudumu katika eneo la Magharibi mwa jiji hilo ambazo zilishiriki kampeni ya "chat coach".

Pia zilisambaza kadi zinazowaomba abiria kusemezana na zingine zikiwaomba kufurahia uwepo wao pamoja kwa tabasamu.

Aidha, ziliwashauri watu wa matabaka mbalimbali kutangamana kwa kutumia huduma ya usafiri ya Glider inayounganisha Ireland Kaskazini na miji ya Mashariki na Magharibi mwa Belfast.

**MATOKEO**

Huenda ukafikiria ni watu wacheshi pekee ndio walionufaika na kampeni hiyo.

Lakini uchunguzi wa kina umebaini kuwa kila mtu alifurahia kuzungumza na mtu asiyemjua kwa mara ya kwanza, wakielekezwa kutabasamu na watu walio karibu nao.

Watafiti walibaini kuwa mazungumzo kati ya watu wawili wasiofahamiana hutegemea na tabia ya mtu binafsi na hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Wanasema baadhi ya watu huenda wasifurahie kwa sababu ni wapole na wanapendelea kuwa kivyao.

Hali hiyo huenda ikamwathiri yule anayependa kuzungumza kwa sababu atafikiria amepuuzwa.

Hofu ya kuogopa kupuuzwa inaelezea kwa nini baadhi ya miji ina watu wengi ambao hawana muda na wenzao.

Pia unaweza kukuta watu wawili wamekaa pamoja, lakini kila mmoja anatumia simu yake ya mkononi kupitisha muda kwa kuangalia picha au kufuatilia matukio katika mitandao ya kijamii.

**UKARIMU USIO NA MIPAKA**

Hata hivyo, wataalamu wanasisitiza umuhimu wa mtu kuzungumza na mtu yeyote au kujaribu kuwakaribisha wale wanaojaribu kujileta karibu nao kwa sababu utafiti umebaini ufanisi wa mazungumzo kama hayo.

Walitoa mfano wa watu kuishia kuwa marafiki na hatimaye wapenzi kutokana na mazungumzo ya watu wawili waliokuwa hawajuani.

"Wakati mwingine ikimuona mtu asiyekujua akijaribu kusema nawe, msikilize ila tumia busara yako kutathmini dhamira yake kwako." Wanasema wataalamu wa masuala ya kisaikolojia. BBC

Hata katika mazingira hayo, makatazo ya kihisia na lugha yaliyojengwa katika jamii za zamani zinazokataza mahusiano ya aina fulani (uhuru wa unyunba, maadili) bado yapo na yanasisitizwa na wataalamu, wakati ambapo jamii imebadilika.

Wanawake wanapokuwa sasa wanajilisha wenyewe, makatazo hayo hayafai kitu kwani msingi wake ni kuilinda 'mali' ya mtu fulani 'isiibwe...'



# WADAU SABATO KASIKA

**KUMEKUWA na mjadala juu ya umri unaofaa kumpeleka mtoto shule za bweni. Wadau wanajadili.**



**MARTHA SIMKONDA (MKAZI WA JIJINI MBEYA)**

JAMBO la kwanza kutambua ni kwamba elimu ni ya muhimu kwa mtoto na ni miongoni mwa haki zake za msingi anazotakiwa kupewa. Pia kuna faida kumpeleka shule ya bweni ikiwamo ya kuongeza bidii katika masomo, kuliko kuwa nyumbani ambako anaweza kupewa majukumu mengine na kujikuta akikosa muda wa kukazania masomo. Ninasema hivyo, kwasababu wapo baadhi ya wazazi huwa hawataki kuona mtoto hana kazi ya kufanya, hivyo watampa kazi badala ya kumwaacha ajisomee. Kwa maana hiyo sioni tatizo la mtoto kupelekwa shule ya bweni. Hata hivyo, jambo la msingi kuzingatia ni umri, kwani si vizuri kumpeleka shule ya bweni mtoto wa kuanzia miaka mitano hadi 10. Umri huo bado mtoto anahitaji kuishi na wazazi wake, akiendelea kupata malezi kuliko kwenda kukutana na tabia ambazo wakati mwingine zinaweza kumharibu. Ni vyema ikaeleweka kwamba watoto wadogo huwa wanapenda kuiga kila kitu, hivyo wakiwekwa shule za bweni wanaweza kuibuka na tabia ambayo hawakutoka nayo nyumbani kwao. Sina maana kwamba huko shuleni hakuna malezi mazuri, ila ninataka nieleweke kuwa ni vyema kuwe na umri maalum wa kumpeleka mtoto shule za bweni, ambao itakuwa rahisi kukabiliana na mazingira mapya huku akizingatia kile alichofundishwa nyumbani kwao badala ya kupelekwa mbali na wazazi wakati bado hajafikia umri wa kuishi mbali na kwao.



**ARAFA MBIZO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIDHANI kama ni vizuri kumpeleka mtoto kuishi bweni angali mdogo. Kufanya hivyo ni sawa na kumuonea, kutokana na ukweli kwamba anatakiwa kwenda huko akiwa tayari ameshajitambua. Wazazi waache kuharakisha kuwapeleka watoto wao huko kwa lengo la kutaka wabaki huru ili waendelee na shughuli zao. Wanawakosesha watoto mapenzi yao na kujiongezea gharama zisizo za lazima kwa kulipa ada kubwa kwa mtoto, ambaye bado hajajitambua vizuri. Ushauri wangu ni kwamba wazazi na walezi wasikwepe majukumu ya malezi kwa watoto wao kwa kisingizio cha kuwapeleka shule za bweni, kwani sasa umekuwa kama mtindo fulani hivi wa kupeleka watoto bweni kuanzia hata chekechea na shule ya msingi. Wanaofanya hivyo wanaweza kuwa na lengo zuri, lakini kuna haja ya kuangalia na kutafakari kwa kina hasara na faida zinazopatikana katika mtindo huo. Inawezekana wakapata elimu bora, lakini binafsi siamini kwenye suala la tabia, kwasababu wapo baadhi ya watoto huwa wanabadilika tabia na kuwa wakorofi kutokana na maisha ya bweni, kwa kuwa wanakutana na wale walioshindikana na kuiga matendo yao. Inawezekana mtoto akaharibika hata akiwa nyumbani, lakini hii ya kuishi bweni anakuwa huru zaidi kushiriki katika vitendo vibaya bila woga.



**SWAUMU MSHAM (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**


KUMPELEKA mtoto shule ya bweni ni muhimu sana kuzingatia umri wake. Itakuwa ni kosa kumpeleka mtoto, ambaye bado anahitaji kuwa karibu na wazazi wake. Kwa wale ambao angalau wameshajitambua wanaweza kupelekwa huko. Ni kweli kuna changamoto nyingi zikiwamo za usafiri wa kwenda shule, kwa watoto wanaoishi mijini, kwa kuamka alfajiri kwenda shule, huku wengine wakikosa usafiri. Inawezekana baadhi ya wazazi wanachoka na kero hiyo na kuamua kuwapeleka shule za bweni. Lakini sioni mantiki kumpeleka huko mtoto mdogo. Malezi bora kwa mtoto ni ya wazazi wake. Jambo hili ni la kujadili kwa umakini sana, kwasababu kupeleka mtoto angali mdogo kwenda kuishi bweni ni kumfanya ajifunze tabia ambazo hakulelewa nazo nyumbani kwao, kwani kule anakutana na wenzake wenye tabia tofauti wakiwamo wakorofi. Katika mazingira ya aina hiyo anaweza kuangukia kwenye tabia mbaya. Ninajua kuwa zipo shule zinazofuatilia sana watoto ili kuhakikisha wanakuwa salama, kuhakikisha wanakuwa na tabia njema na kuhakikisha wanahudhuria vipindi vya masomo kikamilifu. Lakini ni vyema mtoto akapelekwa huko akiwa angalau na miaka kuanzia 14. Chini ya hapo, bado anahitaji kuwa karibu na wazazi wake ili aendelee kukomaa kiakili na kukua kimwili hadi kufikia umri huo ndipo apelekwe bweni akiwa na uelewa wa kutosha, kutambua jema na baya ili aweze kuepuka yale ambayo anaona hayafai kuigwa.



**EZZA TIMBA (MKAZI WA JIJINI MWANZA)**

WATOTO wadogo kupelekwa shule za bweni ni sawa na kuwakosesha upendo wa wazazi wao. 'Matron au patron' hawawezi kuwaangalia wote na kuisoma saikolojia. Lengo la kuwapeleka huko ni zuri, lakini kuzingatia umri ili watoto wasikose malezi ya wazazi ni muhimu zaidi ingawa inawezekana wazazi wa siku hizi wamekuwa wakikwepa majukumu ya malezi na kuwaachia watumishi wa ndani. Binafsi sioni ni kwa nini walimu ndio waachiwe jukumu la malezi kwa watoto wetu. Ina maana wakiharibika tutalaumu walimu? Tutimize wajibu wetu kama wazazi wa kuhakikisha watoto wanapata malezi bora, ambayo yatawafanya wawe raia wema wa baadaye. Zamani wanafunzi walikuwa wakienda bweni wakiwa sekondari, lakini leo hata watoto wa shule za awali nao wanapelekwa bweni! Inashangaza sana. Kwanza nieleweke kuwa sipingi kuwapo kwa shule za bweni ila ninapinga mtoto mwenye umri mdogo kupelekwa bweni. Mtoto mdogo anatakiwa kuishi na wazazi wake. Kila mzazi anayetambua hilo hana budi kuacha uvivu na kusaidia watoto wake kukua katika malezi mazuri.

Pia sina uhakika kama shule zote zimeandaliwa vizuri ili kupokea wanafunzi wa bweni. Kinachotokea sasa ni kwamba baadhi ya wazazi wa siku hizi hawana nafasi ya kukaa na watoto wao, wanatumia muda mwingi kwenye shughuli zao, ndio maana wanalazimika kupeleka watoto bweni ili wapate muda wa kuhangaikia maisha ya kila siku wakidhani watoto wakiwa bweni ndio wanapata malezi mazuri. Niwaambie kuwa kwa watoto wadogo kuishi bweni siyo vizuri, waachwe wanaojitambua kwanza.



**FATUMA KUSAGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KURUHUSU mtoto mwenye umri mdogo kwenda kuishi bweni wakati bado anahitaji kupata malezi ya wazazi na upendo wa wazazi ni kosa. Kama mzazi ana uwezo wa fedha kiasi hicho, basi awe anampeleka mtoto shule asubuhi na kumfuata jioni siyo kumwacha bweni. Kuishi na wazazi ni vizuri zaidi kuliko kumwacha alelewe na shule. Upo umri unaofaa kumpeleka mtoto bweni hasa ule wa kuhitimu elimu ya msingi, lakini siyo mtoto wa miaka sita hadi 10. Huyo bado hajajitambua, anahitaji kupata malezi ya wazazi. Kuna uwezekano mkubwa mtoto kuwa na mapenzi kwa walimu zaidi kuliko wazazi iwapo atapelekwa bweni angali mdogo. Kwa kawaida mzazi anatakiwa kutenga muda wa angalau saa mbili kwa ajili ya kukaa na mtoto wake hata kama ana shughuli nyingi za kufanya. Vinginevyo ni kusababisha mtoto apate walimu wengine wa kumfundisha tabia mbaya. Wazazi wajitahidi kuishi na watoto wao hadi pale wanapofikia umri wa kupelekwa shule za bweni, kwasababu kuna hasara kubwa inayoweza kupatikana kwa kupeleka watoto wadogo bweni. Kumekuwapo na taarifa mbalimbali zinazohusu mabadiliko ya tabia za baadhi ya watoto wanaopelekwa bweni, ambazo zinasikitisha. Kama mzazi anajimudu kimaisha, awe anampeleka mtoto shule asubuhi na kumfuata jioni.



HABARI MBEYA

## Kamati ya maji yavunjwa, yatuhumiwa ufisadi

**Na Nebart Msokwa,**

SONGWE

MKUU wa Wilaya ya Songwe, Samwel Opurukwa, amekerwa na Kamati ya Maji ya Kijiji cha Saza wilayani humo kudaiwa kung'ang'aniana mapato ya maji na kuivunja, huku akiagiza iundwe upya ili kuwashirikisha wananchi.

Alitoa uamuzi huo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazindua mradi wa maji ya kisima kirefu katika kijiji hicho kilichochimbwa kwa msaada na kampuni ya uchimbaji dhahabu wa Shanta Mine pamoja na wananchi.

Alisema kamati hiyo ni tatizo na inaweza ikasababisha miradi ya maji kufa, hivyo ili kuepusha hatari ni lazima iundwe upya na wananchi washiriki katika kuiunda ili wahuni wasijipenyeze kutafuna mapato.

"Hii kamati haifai hata kidogo, sasa naivunja na naagiza iundwe upya chini ya usimamizi wa mhandisi wa maji na wananchi wote wa kijiji hiki washiriki kikamilifu, watu wanajitolea miradi halafu wengine wanatafuna mapato," alisema Opurukwa.

Aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwasaidia wananchi wa kijiji hicho kupata huduma hiyo kwa maelezo kuwa wilaya hiyo ni miongoni mwa maeneo yenye changamoto kubwa ya maji.

Alisema kwa sasa serikali imeshatoa fedha nyingi kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji katika baadhi ya vijiji na kata ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo na kwamba tayari makandarasi wanaendelea na kazi.

Akikabidhi kisima hicho kwa Mkuu wa Wilaya, Meneja Msaidizi wa Uhusiano wa Jamii wa mgodi wa Shanta, Edson Katabwa alisema kisima hicho kimegharimu zaidi ya shilingi milioni 31.

Kaimu Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Medson Ngairo, aliahidi kutekeleza agizo la Mkuu wa Wilaya la kuunda upya Kamati ya Maji ya Kijiji.

Aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji, ili kuepuka kusababisha ukame ambao unaweza ukawatesa miaka yote.

# Wazee walia wapiga ramli kuwaangamiza

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

WAZEE wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kuwaondoa waganga wa jadi maarufu kama 'lambalamba' waliotapakaa wilayani humo kupiga ramli chonganishi zinazosababisha ukatili dhidi ya wazee hao.

Walitoa kilio hicho mwishoni mwa wiki kwa uongozi wa wilaya hiyo wakati wa maadhimisho Siku ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wazee, yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Chimala wilayani humo na kuhudhuriwa na wazee mbalimbali.

Katibu wa wazee hao, Hezron Kapwela, alisema lambalamba wamekuwa wakipiga ramli ambazo zinawahusisha wazee na imani za kishirikina wakidai kuwa ni wachawi hivyo kusababisha ukatili dhidi ya kundi hilo.

Alisema baadhi ya vijiji wananchi wake wamekuwa wakidai kuwa kuna uchawi unafanyika na hivyo kuwaita waganga hao ili wawaondolee hali hiyo na wakifika wanaanza kuwachonganisha wananchi hao na wazee wao, hivyo akaiomba serikali kuwakomesha lambalamba hao.

"Kikundi hicho kimekuwa kikisababisha unyanyasaji kwa wazee, wamekuwa wakiwatoza wazee fedha nyingi wakidai ni za ukaguzi kwenye makazi yao, lakini pia wamekuwa wakidai kuwa wazee ni wachawi, hivyo kusababisha wananchi wawachukie na kuwanyanyasa," alisema Kapwela.

Kapwela pia alisema asilimia kubwa ya wazee wilayani Mbarali wanakabiliwa na maisha magumu kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watoto yatima wanaoachiwa na watoto wao wanaofariki kutokana na Ukimwi.

Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Mbarali ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Chimala, Francis Mtega, alisema tatizo la lambalamba katika wilaya hiyo ni kubwa na maisha ya baadhi ya watu wakiwamo wazee na baadhi yao kupoteza mali zao.

Kwa mujibu wa maelezo lambalamba kundi hilo limekuwa likiwalaghai zaidi vijana hasa maeneo ya vijijini na kuwaaminisha hawaendelei kiuchumi kwa sababu ya baadhi ya wachawi wanaokwamisha juhudi zao na kuwashawishi kuwa wanao uwezo wa kuondoa tatizo hilo.

"Hawa watu wana nguvu na ushawishi, wanashawishi sana watu vijijini na kuwaambia kuwa kijiji kinatakiwa kisafishwe kwa kupita nyumba kwa nyumba ili wenye vitu vibaya viondolewe, sasa cha ajabu wazee wetu hawa ndio wanaolengwa zaidi," alisema Mtega.

Alisema kutokana na uwepo wa watu hao, serikali ya wilaya hiyo ilishaanza kuchukua hatua za kukomesha kwa kuwazuia viongozi wa vijiji kutoruhusu shughuli za lambalamba kufanyika na kwamba atakayebainika anaruhusu apelekwa mahakamani.

Aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidii ili watajirike badala ya kuendelea kushikilia imani za kishirikina kuwa wanarogwa, huku akisisitiza kuwa hakuna namna ya kuwa tajiri bila kufanya kazi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, Ofisa Mipango wa wilaya hiyo, Emmanuel Kishimbo alisema serikali ya wilaya hiyo inawathamini na kuwalinda wazee.

Alisema serikali inatambua mchango wa wazee katika maendeleo na hivyo itaendelea kushirikiana nao ikiwa ni pamoja na kupigania maslahi yao mbalimbali.




Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mwanasha Tumbo (mwenye baibui), akiwa katika picha ya pamoja juzi na wanafunzi na wazazi katika mdahalo wa Siku ya Mtoto wa Afrika katika ukumbi wa CWT, Wilaya ya Muheza. Wapili kulia ni Ofisa Maendeleo ya Jamii anayeshughulikia watoto, Potina Guga, (katikati) ni Meneja wa Benki ya NMB Muheza, Anna Chimalilo na wa pili kushoto ni Meneja wa Benki ya CRDB Muheza, Bonifasi Shija. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wananchi wafaidi neema ya maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Chunya mkoani Mbeya wameanza kunufaika na mradi wa majisafi na salama wa Msasani-Kiwanja, wanausifu kuwa umewaepusha na maradhi na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu na kutumia muda mwingi kufuata huduma hiyo.

Mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka huu, Rais John Magufuli, alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa mji huo alipokuwa ziarani Mbeya wakidai kuwa hawapati huduma ya maji safi kutokana na mradi huo kuchukua muda mrefu na hauna dalili za kukamilika.


Kufuatia malalamiko hayo, Rais Magufuli, alimwagiza Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, kuhakikisha mradi unakamilika haraka na wananchi wanaanza kunufaika, huku akisisitiza kuwa miradi mingi ya maji imekuwa ikisuasua. Wakizungumza na Nipashe wilayani humo baadhi ya wananchi walisema maji yanayotoka kwenye chanzo hicho ni bora kuliko ya maeneo mengine kwa maelezo kuwa hayana kiwango kikubwa cha madini kama ilivyo kwa maeneo mengine.

Mmoja wa wananchi hao, Lucia Mwambete alisema walianza kupata maji mwanzoni mwa mwezi Mei na kwamba awali walikuwa wanatumia maji kutoka kwenye vyanzo vingine, lakini yalikuwa hayafai kutokana na kuwa na chumvi nyingi.

Alisema maji waliyokuwa wanayatumia awali pamoja na kuwa na chumvi nyingi, lakini pia yalikuwa yanatoka mara moja moja na wakati mwingine walikuwa wanamaliza mwezi bila kupata huduma hiyo hali iliyokuwa inawalazimu kwenda kutafuta ya kwenye makorongo. Meneja wa Mamlaka ya Maji wa Mji wa Chunya, Atanus Msangula, alisema mradi huo una visima vitatu na vinavyozalisha maji lita 48,000 kwa saa na sasa umekamilika na usambaza maji lita 1,000,000 kwa siku.

Alisema kiwango hicho cha upatikanaji wa maji ni sawa na asilimia 81 ya mahitaji ya wananchi wa mji huo na hivyo changamoto imepungua kwa kiasi kikubwa.

Msimamizi wa Kampuni ya Make Engineering and Water Works Ltd, iliyojenga mradi huo wa maji, Tanda John, alisema tangu mradi huo uanze kufanya kazi hawajapata changamoto ya aina yoyote na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji bila tatizo.





# Wazalishaji wadogo umeme kutambuliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanza kuwatambua wazalishaji wadogo wa umeme pamoja na kuwasimamia hata kama wanazalisha umeme kwa kiasi kidogo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa kikao kati yake na watumishi wa Tanesco wakiwamo wa Mradi wa Umeme Vijijini (REA) zaidi ya 261.

Alisema ni wajibu wa Tanesco na REA kuwatambua wazalishaji wadogo wa umeme na lazima ifike mahali ufanyike utafitiunaoweza kusaidia kuongeza umeme katika maeneo mbalimbali hata kwa wale wenye leseni za Ewura.

"Ni lazima tuwatambue na kuwasimamia ikiwamo kuwaingiza ili REA na Tanesco wawasimamie kwa sababu wana mchango mkubwa sana katika hili," alisema Dk. Kalemani.

Waziri Kalemani alisema watendaji hao wameitwa ili kutafakari walichokifanya 2018/2019 na kujipanga pya kutekeleza majukumu yao= katika mwaka wa fedha unaoanza Julai Mosi ili kuhakikisha huduma zinakuwa imara muda wote katika maeneo mbalimbali.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanakwenda kutekeleza majukumu ili kutimiza azima ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

"Changamoto zilizopo katika gridi ya taifa, Ngara bado kuna changamoto ambapo watu wanasema bora wabaki na mafuta yao, tumepeleka gridi kwa lengo la kutatua kero, lakini inazidi, Liwale, Geita changamoto zimeonekana."

Aidha, aliwataka kusimamia kupeleka umeme kwenye taasisi kama vyuo, shule, makanisa, hospitali na nyingine kusaidia jamii ya maeneo husika.

Alisema ajenda moja wapo itakayojadiliwa katika kikao hicho ni utekelezaji wa Sh. 27,000 kupeleka umeme vijijini kwa nchi nzima.

Alisema kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda, kunatakiwa kuwa na kitengo cha kufuatilia maeneo ya kiuchumi na namna ya kuwapelekea umeme katika maeneo hayo. "Kuna wateja wa kawaida wanalalamika hawajaunganishiwa umeme miezi miwili au mitatu, mtu katoa pesa yake analalamika tu, lazima tukubaliane hapo tukarekebishe na kufikisha umeme katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji," alisema.

Pia alisema miradi ya REA inayoendelea kusuasua ipo, inayokwenda kwa wastani na kwa kasi na makandarasi wanaoshindwa kufanya kazi lazima wachukuliwe hatua kama serikali.

"Mahusiano ya mameneja na wateja sio mazuri, lazima mbadilike na myatafute hayo mazingira, njia pekee lazima myatembelee maeneo yote msibaki maofisini tu," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. Hamis Mwinyimvua, alisema kikao hicho ni kwa ajili ya kupeana maelekezo ya kazi, mahali pa kurekebisha na pa kuongeza bidii.

# Jiji lamaliza mgogoro wa viwanja

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amemaliza mgogoro wa ardhi uliodumu kwa zaidi ya miaka 20 kwa wakazi eneo la C Centre lililopo Kata ya Nkuhungu, baada ya kufikiwa makubaliano katika kikao cha pamoja kati ya wakazi wa eneo hilo na maofisa ardhi wa halmashauri.

Akizungumza katika kikao hicho kilichojumuisha makundi hayo mawili,

Kunambi alisema kuna kila sababu ya serikali kuwasaidia wananchi hao kupata stahiki zao katika eneo hilo, lakini wanatakiwa kuwa wakweli na waadilifu.

Alisema kila mkazi wa eneo hilo atambue kuwa yeye ni mvamizi kwenye eneo hilo, lakini serikali ya Rais John Magufuli haiwezi kuwaacha wananchi wake wakitaabika, ndio maana wameamua kufanya hisani kwa kuhakikisha kila mtu anapata kiwanja eneo hilo kwa ajili ya kujenga.

Alisema kama mtu mwenye haki ya kupata eneo la C Centre akalikosa kwa sababu yoyote ile, halmashauri itajitahidi kumtafutia eneo jingine, lakini kwanza watatangulia kumaliza waliokuwa wakiishi hapo kwa miaka mingi bila kuwa na mahali pengine mbadala pa kuishi.

"Naomba wakazi wa eneo hili muwe na subira, kila mmoja atapatiwa stahiki yake kinachotakiwa ni watu kuwa wakweli," alisema Kunambi.

Kufuatia makubaliano hayo, wakazi wa eneo hilo wameonyesha kufurahishwa na walichoahidiwa kutekelezewa na Mkurugenzi wa Jiji, huku wakiahidi kudumisha mshikamano katika eneo hilo.

Hata hivyo, Kunambi ameahidi kupima upya eneo hilo ili kukidhi hitaji la wananchi hao na kuhakikisha zoezi hilo linakamilika ndani ya miezi miwili.

Aliongeza baada ya kukamilisha zoezi hilo, hategemei kuona malumbano yakiendelea, na kuwataka waendeleze ujenzi pale watakapokabidhiwa viwanja.

Baadhi ya wajumbe waliowakilisha wananchi wanaoishi katika eneo hilo walimshukuru Kunambi na kuahidi kusimamia mambo waliyokubaliana ikiwamo kuhakikisha hakuna udanganyifu utakaojitokeza kwenye kuwatambua wanaotakiwa kupewa viwanja katika eneo hilo.




Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Tabora (WETCO), Mrisho Simba (kulia), akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 228 kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ikiwa ni gawio kutoka Benki ya CRDB, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango aagiza msako wizi benki kimtandao

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameziagiza benki na taasisi za fedha kufanya uchunguzi wa kuhusu taarifa za wizi wa fedha kwa njia ya mtandao unaolalamikiwa na baadhi ya wateja katika benki.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya Sh. bilioni 6.78 ikiwa ni gawio kutoka benki ya CRDB kutokana na kupata faida kwa mwaka 2018.

Waziri Mpango aliziagiza benki na taasisi za kifedha kufanya uchunguzi wa kina kuhusu malalamiko kwa baadhi ya wateja kuibiwa fedha zao kwa njia ya mtandao.

"Bahati nzuri nimefuatilia malalamiko hayo, sijasikia benki ya CRDB ikitajwa... ninawapongeza kwa utendaji wenu mzuri, endeleeni hivyo," alisema.

Aidha, alizitaka benki hizo kuwekeza kwenye mifumo ya kielektroniki ili kuendana na kasi ya mabadiliko ulimwenguni.

Aliishukuru benki hiyo kwa kuipatia serikali kiasi hicho cha fedha kama gawio kutokana na kupata faida yao mwaka 2018, na kuzitaka benki zote kuendelea kutoa elimu ya kifedha kwa wananchi ili kuepuka kuibiwa na watu wasio waaminifu.


Pia aliwataka wananchi kununua hisa kwenye benki ili kunufaika na sehemu ya gawio linalotolewa baada ya faida.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Ally Laay, alisema benki hiyo inamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 80 na serikali asilimia 38.

Laay alisema kati ya hizo, asilimia 21 zinazotokana na mfuko wa uwekezaji wa Danida, ambapo asilimia 15 zinatokana na mashirika na taasisi mbalimbali za umma.

Mkurungenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajidi Nsekela, alisema kila mwaka benki hiyo imekuwa ikitoa gawio kwa wanahisa wake kulingana na kiasi chao cha uwekezaji, na mwaka huu itatoa zaidi ya Sh. bilioni 21.

Nsekela alibainisha kuwa katika gawio hilo, kila hisa itapata kiasi cha Sh. 8.





Madereva wa bodaboda wakiwa wamepanga foleni pikipiki zao jana, katika gulio la Jumatatu eneo la soko kuu la vyakula na mboga, Muheza Mjini mkoani Tanga wakisubiri abiria. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri aweka wazi msimamo wa serikali ukatili wa watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, amesema serikali haijakaa kimya katika kufuatilia vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto vinavyoendelea katika jamii.

Akizungumza juzi katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika katika kijiji cha SOS, Castico alisema Zanzibar imekuwa ikitekeleza mpango wa kitaifa wa miaka mitano wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye lengo la kuzuia udhalilishaji wa nyanja zote.

Alisema juhudi mbalimbali zinachukuliwa na serikali kuhakikisha watoto wanalindwa bila kuvunjiwa haki zao kisheria ili kufikia malengo yao kimaisha.

Katika kuhakikisha azma hiyo inatimizwa, waziri huyo aliitaka jamii na taasisi zinazosimamia sheria kila mmoja kwa nafasi yake achukue jukumu la kuwalinda watoto ikiwamo kupatiwa haki zao za msingi.

Naye Mkurugenzi wa Miradi wa SOS, Asha Salim Ali, aliiomba serikali kuhakikisha sheria zinasimamiwa vizuri ili watoto walindwe na kutunzwa.

Alisema bado jamii haijawa tayari katika mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili dhidi ya watoto, hivyo serikali haina budi kubuni mbinu na njia bora za kuwashajihisha ili kutoa ushirikiano pindi watoto wanapofanyiwa ukatili. Baadhi ya wazazi waliofika kwenye maadhimisho hayo, wakiwamo Maryam Ali na Khadija Bakari, walisema vitendo vya udhalilishaji vinasababisha athari katika jamii pamoja na kwenye familia, hivyo serikali izidishe nguvu ili kutokomeza kabisa ukatili kwa watoto.

Pia walisema endapo serikali itashindwa kudhibiti tatizo hilo, taifa litashindwa kupata vijana bora na wenye nguvu za kufanya kazi. Katika maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na taasisi mbalimbali za kutetea haki za wanawake na watoto, ikiwamo SOS, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Action Aid, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar, Save the Children na C-sema, watoto kutoka shule mbalimbali walicheza na kujifunza michezo mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu, kikapu, kuvuta kamba na magunia.

# Tatizo la maji kuwa historia 2020

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati imesema wananchi wa Zanzibar wataondokana na tatizo la majisafi na salama ifikapo mwaka 2020 baada ya kukamilika kwa miradi muhimu inayotekelezwa na serikali na washiriki wa maendeleo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Juma Makungu, alisema hayo jana wakati akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kujua lini tatizo la majisafi na salama litamalizika.

Makungu aliitaja baadhi ya miradi ya majisafi na salama inayotekelezwa na washirika wa maendeleo likiwamo Shirika la Misaada la Japan (JICA) ambalo linasimamia mradi wa majisafi na salama Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema mradi huo ni muhimu na umejikita katika kulipatia ufumbuzi tatizo la majisafi na salama katika mkoa huo kwenye baadhi ya shehia.

Naibu Waziri aliutaja mradi mwengine unaotekelezwa na serikali ya India wa uimarishaji wa miundombinu ya maji mjini ambao uko katika hatua ya kumtafuta mkandarasi.

Alisema mradi huo ukimalizika utasaidia kwa kiasi kikubwa kulipatia ufumbuzi tatizo la maji na kuyawezesha baadhi ya maeneo ya mjini kupata huduma hiyo bila kikwazo chochote.

Mradi mwingine, kwa mujibu wa Makungu, ni wa uchimbaji wa visima na usambazaji wa maji vijijini ambao unafadhiliwa na serikali ya China. Alisema mradi huo umelenga kuimarisha huduma za majisafi katika maeneo ya Chaani Bandamaji kwa kuchimba visima viwili na kazi za ulazaji mabomba.

Alisema katika mradi huo, kazi za kujenga matangi na kulaza mabomba ya kusambaza majisafi na salama zitafanyika.

Makungu alisema mradi wa uendelezaji wa visima vya Ras Al-Khaimah ikiwamo ujenzi wa visima vilivyoko Unguja na Pemba unaendelea katika hatua nzuri.

Alisema kazi zinazoendelea kufanyika kwa sasa ni pamoja na kuviendeleza visima vilivyochimbwa na gharama za umeme na ununuzi wa mabomba. Alieleza kwamba mradi wa Ras Al-Khaimah umetengewa Sh. bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha visima hivyo na kuanza uzalishaji wa maji.

"Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ikikamilika kwa kiasi kikubwa wananchi wa Zanzibar watafaidika na huduma ya majisafi na salama, hivyo kurahisisha huduma za maendeleo."

# Wahoji uchakavu wa nyumba za maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati imetakiwa kuharakisha ukarabati wa nyumba za maendeleo ambazo baadhi yake ziko katika hali mbaya ikiwamo ya Kengeja.

Mwakilishi wa Viti Maalumu, Tatu Mohamed Ussi, wakati akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, alisema baadhi ya nyumba za maendeleo hazikaliki kwa sasa na baadhi zinahatarisha maisha ya wakazi wake.

Alitoa mfano nyumba za maendeleo zilioko Kengeja, Pemba, ambazo alisema zimechakaa na baadhi wakazi wake wamezikimbia ili kuokoa maisha yao.

"Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Ardhi atuambie lini nyumba za Kengeja zitafanyiwa ukarabati kwa sababu zimechakaa sana," alisema.

Aidha, Mwakilishi wa Wingwi, Said Omar Said, alisema nyumba za maendeleo zilizoko Pemba ikiwamo Mtamani zinahitaji ukarabati ili kuziokoa na hatari ya kuanguka.

"Hizi nyumba ni juhudi za Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, kwa hivyo tunatakiwa tuzifanyia kazi kwa kuzikarabati," alisema.

Akijibu hoja za wajumbe hao, Waziri wa Wizara hiyo, Salama Aboud Talib, alisema Shirika la Nyumba la Zanzibar linakusudia kuzifanyia ukarabati nyumba 49 zikiwamo 10 zilioko Pemba kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

Alikiri kwamba nyumba nyingi za maendeleo ziko katika hali mbaya tangu zilipojengwa kwa zaidi ya miaka 40.

"Mheshimiwa Spika, wizara imejipanga kuhakikisha nyumba za maendeleo zinafanyiwa ukarabati. Nyumba 49 zimepangwa kujengwa zikiwamo 10 zilizoko Pemba," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kuidhinisha Sh. bilioni 156.582 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

# Ulinzi wa watoto wahimizwa

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kuzingatia kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ya mwaka huu, ili kutambua na kutekeleza haki za mtoto, ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Hayo yalisemwa Jumapili na Katibu Tawala Msaidizi wa Mipango na Uratibu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Yokobety Malisa, kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika.

Maadhimisho hayo kimkoa yalifanyika kwenye viwanja wa Shule ya Msingi Makuburi yakiwa na kaulimbiu isemayo; "Mtoto ni Msingi wa Taifa Endelevu: Tumtunze, Tumlinde na Kumwendeleza".

"Kaulimbiu hii inasisitiza na kutukumbusha umuhimu wa jamii yetu kutambua na kuzitekeleza haki za watoto kama ambavyo nchi yetu imeridhia mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto," alisema Malisa.

Alisema haki hizo zikitekelezwa ipasavyo, vitendo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto havitakuwapo katika jamii, kwa vile kila mmoja atakuwa na jukumu la kumlinda mtoto.

Aidha, Malisa aliwashukuru viongozi na watendaji wa mkoa na halmashauri za manispaa za mkoa wa Dar es Salaam na wadau mbalimbali zikiwamo asasi za kiraia kwa kufanikisha maadhimisho hayo.

Malisa alitaja baadhi ya mashirika ya kiraia yaliyofanikisha maadhimisho hayo kuwa ni Ekama Development Foundation Tanzania, Save the Children, African Child Support, Kiwohede, Yowea Foundation na Voice of Women.

# Dar waeleza mwarobaini ukatili kwa watoto

**Na Yasmine Protace**

BAADHI ya wananchi wamesema vitendo vya unyanyasaji dhidi ya watoto vinaweza kukoma ikiwa jamii haitawafumbia macho wahusika.

Walisema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, yaliyofanyika juzi.

Wananchi hao walisema kuyafumbia macho matukio ya ukatili kumesababisha kuongezeka na kuwaathiri zaidi watoto.

Katika maadhimisho hayo Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ulitumia usafiri wa daladala katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kwenda maeneo ya Mbagala, Mawasiliano, Kariakoo, Tegeta na Kisemvule Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Lengo la kutumia usafiri huo ni kuzungumza na abiria waliokuwa katika magari hayo na kuchukua maoni yao kuhusu Siku ya Mtoto wa Afrika.

Ofisa Habari wa TGNP Mtandao, Monica John, alisema wameamua kutumia usafiri wa daladala kwa sababu inakuwa rahisi kuzungumza na jamii ambayo inatumia usafiri huo.

"TGNP Mtandao tumeona siku hii tuifanye katika usafiri wa daladala na itasaidia kutokana na watu wengi kutumia usafiri huo, watakuwa wameweza kutoa maneno yao kwa sababu baadhi yao hawakuweza kufika viwanjani," anasema.

Alisema kwa upande wa TGNP Mtandao inatilia mkazo kumlinda mtoto dhidi ya ukatili wa kingono. Asha Juma, ambaye alikuwa katika usafiri wa daladala akitokea Mawasiliano kuelekea Mbagala, alisema ameamua kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika katika daladala badala ya ukumbini au viwanjani.

Alisema kufanya hivyo kumeweza kusaidia wasafiri walioshindwa kufika viwanjani, lakini wameweza kupaza sauti zao wakiwa katika daladala.

Alisema kila mwaka watoto wanakumbukwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba ukatili dhidi yao umatokomezwa.

"Tunaadhimisha kumbukumbu hii kila mwaka, lakini kuna kila haja ya kutowafumbia macho wanaoharibu maisha watoto wetu," alisema.

Aliongeza kuwa elimu iendelee kutolewa kutokana na baadhi ya watu kufanyiwa matendo ya kikatili, na kuwa watu wa karibu wamekuwa wakiogopa kuwachukulia hatua.

Shamsa Selemani, mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mabibo, alisema ulinzi kwa watoto uendelee kutolewa na jamii.

Pia alisema wanafunzi waache tamaa, kwa kuwa hali hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa kufuta ndoto zao.




Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 3.5 kwa Suleiman Hussein baada ya kuibuka mmoja wa washindi wakubwa kutoka Kanda ya Pwani, katika promosheni inayojulikana 'Wakala Cash In Promotion'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumia bandari bubu Nkasi waonywa

**Na Mary Geofrey,** NKASI

MKUU wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, amewataka watumiaji wa bandari bubu katika wilaya hiyo, kuacha mara moja na badala yake kutumia Bandari ya Kipili, iliyofanyiwa ukarabati na Mamlaka ya Bandari (TPA).

Aidha, ameahidi kufanya operesheni maalum kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, kuzuia matumizi ya bandari bubu zote zilizopo na zinazofanyakazi katika maeneo ambayo hayajarasimishwa na kuisababisha serikali kukosa mapato.

Mtanda aliyaeleza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea Bandari ya Kipili ambayo imefanyiwa ukarabati na TPA kwa gharama ya Sh. milioni 430 ikiwamo ujenzi wa eneo la kuegesha magari makubwa na madogo.

"Baada ya uboreshaji huu mkubwa kukamilika, bandari yetu imekuwa ya kisasa, hivyo ni wakati mwafaka kwa wanaofanya shughuli za bandari kuanza kuitumia na kuachana na bandari bubu zote zinazozunguka wilaya hii ya Nkasi," alisema Mtanda na kuongeza:

"Natoa wito kwa watumiaji wa bandari bubu zote kuacha kuzitumia mara moja, hii bandari inajitosheleza. Tutafanya operesheni maalum kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama tutakaowakamata wanatumia bandari zilizopigwa marufuku tutawachukulia hatua za kisheria."

Akiwa katika bandari bubu ya Kirando, Mtanda alisema TPA wameshabaini bandari bubu 45 zilizopo katika wilaya hiyo na zitakazorasimishwa ni tano na nyingine zitafungwa ili kuongeza ufanisi wa mamlaka.

Awali Meneja wa Bandari ya Kigoma, ambaye anasimamia bandari zote za Ziwa Tanganyika, Ajuaye Msese, alisema bandari hiyo haikuwa na barabara ya kuingia na eneo la kuegesha magari hali iliyokuwa inasababisha usumbufu kwa watumiaji.

Alisema tayari eneo hilo limeshafanyiwa ukarabati, hivyo wafanyabiashara na wenye vyombo vya usafiri wanapaswa kuanza kufanya shughuli zao eneo hilo lenye usalama na maofisa wa mamlaka zote zinazosimamia shughuli za bandari.

Aidha, alisema Wakala wa Barabara (Tanroad) wameshajenga barabara ya kuingia katika bandari hiyo, hivyo hakuna changamoto inayowazuia wenye vyombo vya usafiri na wafanyabiashara kuacha kuitumia.

Alisema bandari hiyo awali ilikuwa ikihudumia meli ya MV Liyemba, iliyopata ajali mwaka jana katika Ziwa Victoria na kwamba ilikuwa msaada kwa wakazi wa maeneo hayo kwa ajili ya kusafirisha abiria na mizigo yao.

Pia alisema biashara kuu inayofanyika katika bandari hiyo ni usafirishaji wa mazao ya nafaka kama mchele, sukari, maharage na mahindi kwenda nchi ya Demokrasia ya Congo.

Naye msimamizi wa bandari hiyo, Hamis Mselemu, alisema gharama za kusafirisha mizigo zinalingana na zile wanazotozwa wafanyabiashara katika bandari bubu.

Pia alisema tani moja ya mizigo wanatoza Sh. 6,000 na kuwataka wanaotumia bandari bubu kutumia ya Kibili kwa sababu ina kina kirefu zaidi ya nyingine.

# Mwingine mwenye dalili za ebola aonekana Kenya

**NAIROBI, Kenya**

WAKATI mtoto wa miaka mitano akifariki Uganda kwa ugonjwa wa ebola, madaktari katika Hospitali ya Kericho nchini Kenya, wanamchunguza mwanamke ambaye ameonesha kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Mwanamke huyo anaripotiwa kuwa na dalili zinazowapata wagonjwa wanaougua ugonjwa wa ebola.

Maofisa wa afya katika Jimbo la Kericho walisema kuwa mwanamke huyo alikuwa ametoka eneo la Malaba, ambalo lipo mpakani mwa Kenya na Uganda.

Hata hivyo, hakuna ripoti yoyote iliyotolewa ya kuwapo kwa ugonjwa wa ebola karibu na mpaka wa Malaba, isipokuwa eneo la Magharibi mwa Uganda.

Sampuli za damu za mgonjwa huyo zimechukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Imeelezwa kuwa mwanamke huyo alikwenda hospitali binafsi siku ya Jumapili na alikuwa na homa kali, maumivu ya kichwa, viungo, koo na alikuwa akitapika.

Mwanamke huyo alitibiwa ugonjwa wa malaria kwenye hospitali hiyo lakini hali yake ilizidi kuwa mbaya.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa alifanyiwa tena kipimo cha malaria na majibu yalionyesha haumwi ugonjwa huo.

Kutokana na hali hiyo, wahudumu wa afya walimpa rufani kwenda Hospitali ya Kaunti ya Kericho ambayo ina uwezo wa kulaza wagonjwa, lakini muda mfupi mwanamke huyo akaanza kuharisha.

Matokeo ya awali ya vipimo yanatarajiwa kuwa tayari katika kipindi cha saa 12 mpaka 24.

Idara ya huduma za afya ya Jimbo la Kericho ilieleza kuwa inafuatilia kwa karibu suala hilo na inafanya kazi pamoja na serikali kuu kuhakikisha kuwa hatua madhubuti zinafuatwa za uwapo wa usalama wa kiafya kwa wengine.

Serikali ya Jimbo la Kericho imewahakikishia wananchi kuwa hospitali ya jimbo ina uwezo na ina vifaa kuhakikisha mgonjwa huyo anatengwa, ili kuwalinda wagonjwa wengine waliopo katika hapo, huku ikiwataka watu kuwa watulivu na wenye subira.

Wiki iliyopita Shirika la Afya Duniani (WHO) lilithibitisha mtoto wa miaka mitano nchini Uganda kugundulika kuwa na ugonjwa wa ebola.

Wizara ya Afya nchini Uganda na WHO walituma kikosi maalumu kutambua endapo kuna watu wengine walioambukizwa.

Waziri wa Afya Uganda, Jane Ruth Aceng, aliwaambia waandishi wa habari kwamba familia ya mtoto huyo iko katika uangalizi maalumu, wakiwamo watu wawili walioonyesha kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Taarifa za baadaye zilieleza kuwa mtoto huyo alipoteza maisha.

Tayari wahudumu 4,700 nchini Uganda wamepewa chanjo dhidi ya ugonjwa huo, huku zaidi ya watu 2,000 wameripotiwa kuugua nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika kipindi cha miezi 10.

Mlipuko wa ugonjwa wa ebola ni wa pili kwa ukubwa nchini DRC, kukiwa na ripoti ya kutokea maambukizi mapya wiki za hivi karibuni.

Baadhi ya watu wamekuwa hawawaamini watoa huduma za afya, hivyo hufanya wenye dalili za ugonjwa huo kukwepa matibabu.

Zaidi ya watu 1,300 wameshapoteza maisha tangu Agosti mwaka jana.

***BBC***



Aliyekuwa Rais wa Sudan, Omar al-Bashir (mwenye mavazi meupe) akiwa kwenye ulinzi mkali akipelekwa kwa mwendesha mashtaka kuhojiwa tuhuma za rushwa zinazomkabili. **PICHA: REUTERS**

# Omar al-Bashir atolewa gerezani, asomewa mashtaka ya rushwa

**KHARTOUM, Sudan**

ALIYEKUWA Rais wa Sudan, Omar al-Bashir amejitokeza hadharani kwa mara ya kwanza tangu alipoondolewa madarakani Aprili, mwaka huu.

Bashir alikuwa akitolewa gerezani katika Mji Mkuu, Khartoum kwenda kwenye ofisi ya mwendesha mashtaka ambaye alimsomea mashtaka ya rushwa yanayomkabili

Akiwa amezungukwa na askari wa usalama, kiongozi huyo wa zamani mwenye miaka 75 alikuwa amevaa vazi lake jeupe na kilemba.

Bashir alipinduliwa madarakani baada ya miezi kadhaa ya maandamano nchini humo.

Waendesha mashtaka wanasema kuwa fedha nyingi za kigeni zilikutwa kwenye magunia nyumbani mwake baada ya kuondolewa madarakani alikohudumu kwa takribani miaka 30.

Bashir alionekana akishuka kwenye gari kuingia kwenye ofisi ya mwendesha mashtaka, akitabasamu na kuzungumza na walinzi, lakini baadaye alirejea akiwa na uso usio na furaha.

Bashir pia anashtakiwa na Mahakama ya Kimataifa, ICC, akishutumiwa kuongoza vitendo vya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya binadamu katika eneo la Darfur, shutuma ambazo amezikana.

Wakati huohuo, Mohamed Hamdan "Hemeti" Dagolo ambaye ni Makamu wa Rais wa Jeshi la Junta aliahidi kuwafikisha mbele ya sheria watu waliosababisha ghasia zilizotokea hivi karibuni.

Kwa mujibu wa wanaharakati wa upinzani, zaidi ya watu 100 waliuawa Juni 3, mwaka huu.

Mamlaka ya Jeshi la Sudan, limekuwa likikosolewa na mataifa duniani kuhusu namna walivyokabiliana na waandamanaji. Sudan imeshaondolewa uanachama wa Umoja wa Afrika (AU)

Wakati huo huo, Mjumbe wa Marekani barani Afrika, Tibor Nagy Ijumaa baada ya kutembelea Khartoum, ametaka kufanyike uchunguzi kuhusu mauaji yaliyotekelezwa.

***BBC***

# Kanisa Anglikana Kenya lapiga marufuku siasa madhabahuni

**NAIROBI, Kenya**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Anglikana Kenya, Jackson Ole Sapit, amesema ni marufuku kwa wanasiasa nchini humo kutoa hotuba zao kwenye madhabahu katika makanisa ya kianglikana.

Askofu Sapit alisema wanasiasa hutumia madhabahu kuligawanya taifa na kuwakejeli wapinzani wao.

Kauli hiyo imetolewa ikiwa zimepita siku chache tangu kanisa hilo kupiga marufuku michango ya wanasiasa.

"Hatutaruhusu madhabahu kuwa mahali pa kupigia siasa, iwapo tutawaruhusu wanasiasa kuzungumza na washirika, watafanyia tu kule nje baada ya ibada, tunataka kusikia neno la Mungu sio siasa," alisema Askofu Ole Sapit.

Alisema kanisa liko njia panda, kwa miaka, na kwamba wanasiasa wamekuwa wakitumia rasilimali zao kuchangia kwenye miradi ya kanisa, kwani baadhi yao ni washirika.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa wanasiasa wengi nchini Kenya wamekuwa wakiyatumia makanisa kupiga kampeni na hutumia madhabahu kwa maslahi yao wenyewe.

Hali hiyo, ndiyo iliyomlazimu Askofu Sapit kujaribu kulisafisha. Sio mara ya kwanza kwa wanasiasa kusuluhishia tofauti zao kwenye madhabahu.

Jumapili iliyopita ibada katika kanisa moja la Kianglikana lililoko katika Jimbo la Kiambu ilisitishwa baada ya mwanasiasa mmoja kuanza kumtusi mpinzani wake alipopewa nafasi ya kuwasalimu waumini, hali hiyo iliwalazimu waumini kuanza kumzomea hadi ibada ikasitishwa. Hatua ya kanisa hilo, inajiri miezi michache tu baada ya kupiga marufuku michango ya wanasiasa kanisani.

Askofu Sapit aliwakosoa wanasiasa ambao hutumia pesa zao kama chambo cha kutumia madhabahu kuelezea mambo yao.

Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka Kenya, Noordin Haji, alisema baadhi ya wanasiasa hutoa fedha haramu kanisani.

"Kama viongozi wa dini na taasisi, mna haki ya kukataa fedha ambazo hamfahamu zinapotoka, mna uwezo wa kujenga asasi za kutambua vyanzo vya fedha zile na kama hamna uwezo huo, basi sisi tupo tutawasaidieni." Alisema Haji.

Askofu Sapit alisema ataendelea kuwahamasisha waumini jinsi ya kukabiliana na ufisadi.

Baadhi ya Wakenya wanasema kuwa kanisa ndilo kizingiti kikuu cha vita dhidi ya ufisadi, huku likiendelea kupokea mamilioni ya fedha kutoka kwa wanasiasa waliopotoka kwa ajili ya kukamilisha miradi yao. Kanisa hilo nchini Kenya linajiunga na kanisa Katoliki ambalo huwa haliruhusu wanasiasa kupiga siasa ndani ya kanisa.

***DW***

# Zimamoto kukopa fedha za kununua vifaa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji nchini, linatarajia kukopa fedha kutoka nchi za nje kwa ajili ya kununua vitendea kazi pamoja na magari ya jeshi hilo, ili kuondoa tatizo la upungufu wa magari nchini.

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza ziara yake mkoani Shinyanga ya kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali zinazolikabili jeshi hilo.

Alisema jeshi hilo lina upungufu mkubwa wa vitendea kazi nchi nzima yakiwamo magari ya kuzimia moto na hatua walizozichukua hadi sasa licha ya serikali kuwatengea bajeti, wameamua kutafuta fedha za mikopo kutoka nchi za nje ikiwamo Australia na Ubelgiji, ambako wapo kwenye hatua za mazungumzo.

"Naipongeza serikali ya awamu ya tano chini ya Rais wetu Dk. John Magufuli, tangu imeingia madarakani tumekuwa tukitengewa bajeti ya fedha kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kututatulia changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikilikabili jeshi letu," aliongeza.

Pia alitoa wito kwa wananchi kuweka ving'amuzi vya moto kwenye nyumba zao pamoja na kuwa na kifaa cha kuzimia moto (Fire Extinguisher), ili pale yatakapotokea majanga ya moto waweze kukabiliana nayo mapema kabla ya kuleta madhara makubwa.

Katika hatua nyingine aliwataka askari wa jeshi hilo kuendelea kujituma kufanya kazi kwa bidii, licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali likiwamo la upungufu wa vitendea kazi.

**"Naipongeza serikali ya awamu ya tano chini ya Rais wetu Dk. John Magufuli, tangu imeingia madarakani tumekuwa tukitengewa bajeti ya fedha...**

# Bajeti pendekezwa yawakuna viwanda

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda (CTI) limeeleza kukoshwa na mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha kwa kuwa yamejibu kilio cha muda mrefu cha wenye viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa CIT, Leodegar Tenga, alieleza kufurahishwa na mapendekezo hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano maalum wa kuchambua bajeti hiyo iliyowasilishwa bungeni Alhamisi.

Alisema wadau wa viwanda walikuwa wakishirikishwa kutoa maoni yao na kubainisha kuwa katika mapendekezo ya bajeti hiyo, asilimia kubwa na mambo muhimu waliyokuwa yamependekezwa na CTI yamejibiwa.

"Ni bajeti ambayo tunaamini imesikiliza kilio cha wenye viwanda kwa asilimia kubwa sana, na ni imani yetu kwamba itasaidia sana katika kuhamasisha ukuaji wa viwanda maana ndiyo shughuli yetu kubwa.

"Kusema ukweli imekidhi na tunaishukuru serikali na Rais John Magufuli kwa bajeti hii na tunaamini itatupeleka kwenye lengo letu la uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2015.

"Kuna andiko ambalo tuliliandika huko nyuma la kuhusiana na kuboresha mazingira biashara katika viwanda, safari hii Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amelizungumzia kwa kirefu, kwamba serikali ya awamu ya tano itahakikisha maazimio ya andiko hilo yanatekelezwa," Tenga alisema.

Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yamefanyiwa kazi na yalikuwa kilio cha muda mrefu kwa wenye viwanda kuwa ni kupunguza utitiri wa taasisi ambazo pamoja na changamoto nyingine, zilikuwa zinasababishwa na uwapo wake kufanya kazi zinazofanana, lakini pia zilikuwa zinachelewesha kupitisha uamuzi, kuongeza gharama na kusababisha usumbufu.

Tenga alisema wenye viwanda pia wameguswa na uamuzi wa serikali kupunguza utitiri wa tozo kutoka kwenye taasisi hizo na zile za halmashauri ambazo ni mzigo kwa wenye viwanda.

Aliongeza kuwa wenye viwanda pia wamefurahishwa na uamuzi wa serikali kupandisha kodi kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani.

Hata hivyo, Tenga alisema CTI wangependa kuona maeneo mengine mawili nayo yafanyiwe kazi. Alisema changamoto bado ipo kwenye viwanda vya vyuma na vinavyosindika mafuta ghafi.

"Kuna watu wanatengeneza vyuma huko nje kwa bei ya kutupwa na kwa bahati mbaya sana katika nchi zao wamekuwa wakipewa misaada na serikali zao, kuna wengine wanasaidiwa kabisa ili watengeneze kwa urahisi, kwa hiyo kama wanasaidiwa na nchi zao, na sisi tuna haki ya kuomba 'protection' (ulinzi) ili viwanda vyetu vifanye vizuri zaidi na nchi yote unapohitaji uchumi wa viwanda, chuma ni muhimu," alisema.

"Pia tuna viwanda vyetu hapa ambavyo vina mitambo ya kusindika mafuta ambavyo kodi yake ni asilimia 25. Kodi hiyo bado ni gharama na ndiyo maana ya ombi la wanachama wa CTI ni kwamba kwa sababu Kenya na Uganda wanaruhusiwa kuingiza mafuta hayo kwa asilimia sifuri, basi tulidhani na sisi tungekwenda huko huko kama wenzetu ili tuwe ushindani, kinyume chake hatuwezi kushindana," Tenga alisema.

Katika mkutano huo, Makamu Mwenyekiti wa CTI, Shabbir Zavery, alisema bajeti ya mwaka huu ni ya maendeleo, akieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na utamaduni mzuri uliowekwa na serikali ya awamu ya tano wa kushauriana.



Watoto na watu wazima wakifuatilia maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Makuburi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwanafunzi wa chuo kikuu auawa kwa kuchomwa kisu

**Na Romana Mallya**

MWANAFUNZI wa mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Kampala, Anifa Simpolianusy, amedaiwa kuuawa na wezi kwa kuchomwa kisu kifuani akiwa karibu na maeneo ya chuo hicho, Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, athibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuiambia Nipashe jana kuwa upelelezi unaendelea na taarifa kamili inatarajiwa kutolewa leo.

Taarifa kuhusu mauaji hayo zilizotolewa na serikali ya wanafunzi ya chuo hicho juzi, zilidai kuwa Anifa mwenye namba ya usajili DMLT/19935/701/DT, alikuwa mwanafunzi wa mwaka wa pili, akichukua Stashahada ya Maabara (Diploma in Medical Laboratory).

Taarifa hiyo ilidai kuwa mwanafunzi huyo aliuawa kwa kuchomwa kisu kifuani upande wa kulia na watu wasiojulikana.

"Tunasikitika kusikia taarifa hii ya ghafla na zenye maumivu, Anifa amekufa leo (Jumapili) saa 10 usiku kwa kuchomwa kisu cha kifuani upande wa kulia na wezi kwenye kona karibu na chuo," taarifa hiyo ilieleza.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI**, Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI



## VYETI VIMEPOTEA



115281502

**ABUBAKARI S. NDWATA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.351/012** kilichotolewa na BAGAMOYO SEKONDARI. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0131/0501** kilichotolewa na MAZENGO SEKONDARI. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/IR/RB/3622/2019.**

## CHETI KIMEPOTEA



115278802

**SIMON BRIGHT MZIRAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1278-0136** kilichotolewa na MBEZI SEKONDARI OCTOBER, 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/63305/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
***(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)***

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 42/2019**

**Ombi la SAFINA RAMADHANI MDABA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu CHIKU ALLY MLWALE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 1/7//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 12/6/2019

115280002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
***(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)***

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 42/2019**

**Ombi la SAFINA RAMADHANI MDABA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu RAMADHANI SELEMANI MDABA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 1/7//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 12/6/2019

115280002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JENIPHER JEREMIAH SUNGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOYA NADIA** yenye namba za usajili **T 425 BNH.** Chassis namba **SXN10-0046301.** Engine NO. **3S – 7888969.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/1070/2019.**

115280102


## CHETI KIMEPOTEA



115280902

**YUSTER MWAKUKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0478/0027** kilichotolewa na KIPOKE HIGH SCHOOL mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TUR/RB/158/19.**


## CHETI KIMEPOTEA



115280802

**BROWN L. KASWELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1144-0074** kilichotolewa na ISIMILA SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/SEL/RB/7109/2019.**

## CHETI KIMEPOTEA



115279402

**ADEODATHA F.J. MDENDEMI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.307/1** kilichotolewa na DODOMA CENTRAL SEKONDARI mwaka 1986. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MB/RB/10403/2016.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ISSA MROPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SENKE yenye namba za usajili **T 553 CYH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DSM/RB/66511/2019.**


115280502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AGRICULTURAL INPUTS TRUST FUND** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T. 659 AZR** yenye engine namba **502672P.** Chassis namba **70030108,** Model namba **MF375 2WD.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi. **KAH /RB/505/2019.**

115280302

## CHETI KIMEPOTEA



115279202

**YUSUPH ZABRON SAKUSI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0101-0489** kilichotolewa na AZANIA SEKONDARI mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **STK/RB/6066/2019.**


Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza

Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0767 223 311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# NDOMBELE AJIPELEKA SPURS

**LONDON, England**

TANGUY Ndombele ameisifia Klabu ya Tottenham Hotspurs na amebainisha kwamba angependa kujiunga na kikosi hicho cha kocha Mauricio Pochettino.

Spurs imekuwa kwenye mazungumzo na Lyon kwa ajili ya kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Sky Sports imebainisha, lakini pia amekuwa akiwaniwa kwa udi na uvumba na miamba wa soka la Italia, Juventus.


Sky Sports imebainisha kwamba, Ndombele ametoa mustakabali wake wa baadaye wakati akiwa likizo na sasa ameamua kwenda kwenye Ligi Kuu ya England na si sehemu nyingine bali Tottenham.

Akizungumza na Gazeti la Telefoot la Ufaransa, Ndombele amesema: "Ni kweli Tottenham ni timu na klabu kubwa. Walimaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu na walicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kuna klabu nyingine kubwa, lakini kila mchezaji anapenda kucheza katika klabu kubwa. Na mimi naiona Tottenham kama sehemu nzuri zaidi ya kwenda kucheza."

"Kwa sasa nipo likizo, lakini majaliwa yangu ya baadaye nayaona si ya kuendelea kucheza pale Lyon, ningependa kujiunga na kocha Mauricio Pochettino kwani ni mmoja wa makocha wakubwa Ulaya."



# HAZARD: POGBA WE NJOO REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

WAKATI joto la mshambuliaji wa Manchester United, Paul Pogba likizidi kufukuta pale Old Trafford na yeye akibainisha wazi anataka kuondoka, kiungo mpya wa Real Madrid, Eden Hazard amemuita kikosini nyota huyo.

Gazeti la AS la nchini Hispania limeripoti kwamba, Hazard amezungumza na Pogba na kumtaka akajiunge naye pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Hazard amenukuliwa akisema kwamba, yeye anataka kucheza na wachezaji bora na hivyo, anamuona Pogba kama mmoja wa wachezaji hao na anastahili kucheza naye hapo Real Madrid.

Hazard alitua Real Madrid wiki iliyopita kwa kitita cha pauni milioni 150 na alitambulishwa rasmi kwa mashabiki 50,000 Alhamisi.

Imemchukua muda mrefu hadi Hazard kutua Real Madrid, huku akiacha pengo kubwa huko Chelsea kutokana na wakati hao wa Stamford Bridge kuwa na adhabu ya kuzuiwa kusajili, hivyo itawachukua muda mrefu kupata staa wa kiwango kama chake kuziba pengo.

Hazard anamtaka Pogba aende akajiunge naye huko Bernabeu kukifanya kikosi hicho kuwa na makali ya kutisha na amekuwa akihusishwa na wababe hao wa Barnebau.

Real Madrid wanajaribu kuishawishi Man United ili iwauzie staa huyo anayesakwa kwelikweli na Kocha Zinedine Zidane, ambaye amepanga kuijenga upya Los Blancos.

Hazard pia amemzungumzia pia Kylian Mbappe, ambaye pia mashabiki wanamtaka akakipige kwenye kikosi chao.

"Nataka kucheza na wachezaji bora, na hao ndio wachezaji bora. Lakini, hilo si jambo langu kuzungumza kuhusu usajili."

# Griezmann kuinunulia Atletico Madrid Felix




**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid imeripotiwa kukaribia kumnasa nyota wa Benfica, Joao Felix na watatumia fedha watakazozipata kwa kumuuza Antoine Griezmann ili kumsajili mchezaji huyo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, klabu kadhaa barani Ulaya zimekuwa zikisaka saini yake kipindi hiki cha majira ya joto, hasa baada ya kuwa na msimu mzuri zaidi na miamba hao wa soka la Ureno.

Klabu ya Manchester City ni moja ya timu ambayo imekuwa ikiwinda saini ya mshambuliaji huyo ili atue pale kwenye dimba la Etihad, huku pia wapinzani wao wa jiji moja, Manchester United wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Felix.

Lakini Atletico ndiyo inayoonekana kushinda katika mbio za usajili wa kinda huyo na anatajwa kwamba, ada yake ni pauni milioni 107 watazipata kwa kumuuza mshambuliaji wao nyota, Griezmann, kwa mujibu wa Gazeti la Marca.

Felix alifunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mechi 43 alizoichezea Benfica msimu uliopita na mkataba wake wa sasa na Benfica unamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2023.

Atletico pia imeripotiwa kuwa inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 44.6 kwa ajili ya kumsajili nyota wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes.

# HABARI MICHEZO



## PSG KUMFUNGULIA MLANGO NEYMAR

**PARIS, Ufaransa**

Klabu ya Paris Saint-Germain itakuwa tayari kumruhusu nyota wake wa Brazil, Neymar kuondoka kama tu watapata ofa kubwa na ya kueleweka, kwa mujibu wa Gazeti la L'Equipe.

PSG imebainisha kwamba ipo tayari kumuuza mchezaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto, lakini watahitaji tu ofa iliyonona kumuachia mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona.

Kurudi kwa Mkurugenzi wa Michezo, Leonardo kulitangazwa rasmi Ijumaa, hivyo klabu hiyo inajiandaa kutengeneza kikosi cha kwanza, huku mchezaji mmoja wakiwa tayari kumwachia akiwa ni Neymar.

Habari hizi ni za mara ya kwanza kwa klabu hiyo kuzibainisha tangu mchezaji huyo alipojiunga na timu hiyo kipindi cha majira ya joto mwaka 2017 kwa mkataba wa miaka mitano na sasa ni wazi kwamba, suala la Neymar kutaka kuondoka hapo jijini Paris lipo wazi.

L'Equipe pia limeripoti kwamba, mchezaji mwenyewe alianza kuonyesha ishara ya kutotaka kuendelea na klabu hiyo, kutokana na matukio yake ya vurugu hasa kwa staili ya maisha yake.

Neymar amekuwa na matukio ya kutoelewana na baadhi ya wachezaji wenzake klabuni hapo hali iliyomfanya kufungiwa mechi kadhaa na pia kwa sasa anakabiliwa na tuhuma za kumbaka mrembo mmoja hotelini jijini Paris.

Zaidi ni kwamba, L'Equipe limeripoti kuwa matajiri wa klabu hiyo kutoka nchini Qatar wameamua kwamba mchezaji huyo sio tena nguzo ya klabu hiyo na hivyo wanataka kumuuza ili kurudisha fedha zao na kuendelea na uwekezaji.

Klabu ambazo zinatajwa kuwania kumsajili mchezaji huyo, ni pamoja na klabu yake ya zamani ya Barcelona, huku taarifa zaidi zikisema kwamba, Rais wa Real Madrid, Florentino Pérez pia anataka saini ya mshambuliaji huyo.



# ABRAMOVICH

## AMHAKIKISHIA LAMPARD UKOCHA CHELSEA

**LONDON, England**

FRANK Lampard ameripotiwa kwamba atachukua nafasi ya ukocha pale Chelsea ndani ya siku chake zijazo baada ya kuhakikishiwa kwamba atakaa kwa kipindi cha angalau miaka miwili kwenye 'kiti cha moto' cha hapo Stamford Bridge.

Maurizio Sarri ameondoka Chelsea na kwenda kujiunga na Juventus, na Lampard sasa anaonekana kuwa mtu anayefaa kuchukua mikoba hiyo katika timu ambayo ameichezea kwa kipindi cha miaka 13.

Gazeti la The Sunday Times limeripoti kwamba, mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich amempigia simu Lampard na kumhakikishia nafasi hiyo ya ukocha katika klabu hiyo.

Ikizingatiwa kwamba, Chelsea kwa sasa imefungiwa kutofanya usajili kipindi cha majira ya joto, ina maana kwamba Lampard anaweza kukaa hapo kwa msimu wa 2019-20 na 2020-21.

Hata hivyo, 'Blues' hao watalazimika kulipa fidia kwa Klabu ya Derby ambayo Lampard anainoa kwa sasa ili kuweza kumruhusu kocha huyo atue pale 'darajani'.

# Arsenal, Saliba sasa wafikia makubaliano

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kwamba imefikia makubaliano na Saint-Etienne ya Ufaransa kwa ajili ya kumsajili beki wake, William Saliba.

'Washika Bunduki' hao wa London wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi kipindi hiki cha majira ya joto na hivyo wanaona kwamba, Saliba mwenye umri wa miaka 18, ambaye alikuwa na msimu mzuri hapo Saint-Etienne, anafaa kutua katika Uwanja wa Emirates.

Kwa mujibu wa Gazeti la Foot Mercato, Arsenal imekubali kumsainisha Saliba kwa mkataba wa miaka mitano na sasa kilichobaki ni kumalizana tu na Saint-Etienne.

Saliba ambaye ni mchezaji wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 19, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa ikiwamo Manchester City na Manchester United.



Hata hivyo, Arsenal ndio imeonekana kumvutia zaidi beki huyo ambaye amebainisha kwamba anataka kucheza kwenye Ligi Kuu ya England.

Arsenal msimu uliopita safu yake ya ulinzi ilikumbwa na dhoruba, huku Shkodran Mustafi akisababisha makosa kadhaa na Laurent Koscielny akisumbuliwa na majeraha na sasa Unai Emery anataka beki mpya kwa ajili ya kuimarisha safu hiyo.

Emery pia ana Sokratis, Rob Holding (ambaye kwa sasa anaendelea kupona kutoka majeruhi), pamoja na Konstantinos Mavropanos, hivyo ujio wa Saliba utaimarisha zaidi beki yake.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BRAZIL INAWEZEKANA BILA NEYMAR - ALVES

**RIO, Brazil**

Dani Alves anaamini Brazil haiwezi kuwa dhaifu kutokana na kukosekana kwa Neymar wakati huu wakisaka mafanikio kwenye fainali za Copa America.

Neymar alienguliwa katika kikosi kinachoshiriki michuano hiyo kutokana na kuumia kifundo cha mguu wakati wakicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Qatar na kuonekana kuwa pigo kwa wenyeji hao, ambao Ijumaa walianza fainali hizo kwa ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bolivia.

Wakati pia akisifu ubora wa mchezaji mwenza huyo wa Paris Saint-Germain, Alves ambaye kwa sasa amekabidhiwa jukumu la unahodha, anaona Brazil si dhaifu wakati ikicheza bila Neymar, 27.

"Ninaamini kuwa kila wakati tunakuja timu ya taifa, tunavaa jezi hii, tunapaswa kuthibitisha hilo, haijalishi Neymar yupo ama la, tunapaswa kuthibitisha hilo kwa sababu tunawakilisha timu ya historia, inayoheshimiwa sana duniani kote," aliuambia mkutano wa wanahabari juzi, Jumapili.

"Lakini wakati unapokuwa na ziada, kama Ney, unakuwa imara kidogo. Lakini huwezi kuwa dhaifu bila yeye, unaongeza tu ubora, unaongeza nguvu zako, lakini huwezi kupungua bila yeye.

"Majukumu yetu yanabaki kama yalivyo - tunawakilisha historia na tunapaswa kuilinda historia hii kwa heshima kubwa."

Ni Cafu (142) pekee na Roberto Carlos (125) walioichezea Brazil mechi nyingi zaidi ya Alves (110) na beki huyo wa pembeni wa PSG, ambaye anamaliza mkataba wake, hana mpango wa kupunguza kasi yake katika timu hiyo ya taifa.

Alves alisema macho yake yapo Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, lakini kwa sasa anapaswa kuendelea kuonyesha kiwango.

"Ni [Kombe la Dunia 2022] ni lengo nililo nalo, lakini siwezi kuruhusu mimi binafsi kutazama mbali zaidi mbele, kwa sababu wakati unapotazama mbali mbele unasahau kutazama ulipo sasa," alisema.

"Siwezi kusahau kutazama nilipo sasa kwa sababu fursa ninayopaswa kuwa nayo hapa haiwezi kuharibiwa na ya mbeleni na si iliyopita. Cha kujali ni kilichopo sasa.

"Ninapindua mwenyewe. Unapofikia umri fulani, unaanza kuongeza mashaka, mengi ya yanayozungumzwa juu ya uteuzi ni upya au klabu zinapaswa kuongeza, kuwa na wachezaji zaidi, vijana, lakini wote katika klabu na timu ya taifa, inajithaminisha yenyewe kwa matokeo."

Brazil itaivaa Venezuela katika mchezo wao wa pili wa Kundi A utakaopigwa Salvador leo Jumanne.

## KWA UFUPI

**RAKITIC, COUTINHO, WATAJWA UNITED**

Manchester United inaweza kumsajili kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31, na mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Philippe Coutinho, kama Mfaransa Paul Pogba, 26, ataachana na klabu hiyo. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**COUTINHO AIFUNGULIA CHELSEA**

Kiungo mshambuliaji wa Barcelona, Mbrazil Philippe Coutinho, 27, amefungua milango ya kujiunga na Chelsea**. *(Express)***

**PSG SASA KUMUUZA NEYMAR**

Paris St-Germain ipo tayari kumuuza mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27. ***(L'Equipe - in French)***

**BALE ANUKIA MKOPO BAYERN**

WINGA wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale, 29, anawindwa kwa mkopo wa muda mrefu na mabingwa wa Ujerumani, Bayern Munich. ***(Sun)***

**NDOMBELE AITAKA TOTTENHAM**

KIUNGO wa Lyon, Mfaransa Tanguy Ndombele, 22, amependekeza kuwa atafungua milango ya kutua Tottenham. ***(Telefoot - in French)***

**CONTE AMTAKA CAHILL INTER**

BEKI wa England, Gary Cahill, 33, anatakiwa na kocha wake wa zamani, Antonio Conte kujiunga naye katika kikosi cha Inter Milan baada ya kuondoka Chelsea. ***(Sport Mediaset - in Italian)***

**UNITED YAMGEUKIA DUMFRIES**

Manchester United inamtaka beki wa kulia wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Denzel Dumfries, 23. ***(Sun)***

**LIVERPOOL YAMTAKA TOKOZ**

Liverpool imeingia katika mbio za kuisaka saini ya kiungo wa Besiktas, Mturuki Dorukhan Tokoz, 23, wakati huu Udinese ikiwa tayari imepokea ofa na kuikata. ***(Fotomac - in Turkish)***

**GUARDIOLA AMTAKA RIESGO ETIHAD**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaitaka huduma ya kipa wa Eibar, Mhispania Asier Riesgo, 35, pale Etihad**. *(Sun)***

**BUFFON KUPUMZIKA SOKA**

KIPA mkongwe wa Italia, Gianluigi Buffon, 41, atapumzika soka kwa msimu mmoja baada ya kukataa ofa ya kuongeza mkataba wa mwaka mmoja hapo PSG. ***(Corriere dello Sport, via Goal)***

**RAIS PSG AKERWA TABIA ZA MASTAA**

Rais wa PSG, Nasser Al Khelaifi ameonya kwamba hataki tena kuona "tabia ya mtu maarufu" kutoka kwa wachezaji wake. ***(France Football - in French)***

**ARSENAL KUMSAJILI SALIBA**

Arsenal inakaribia kumsajili beki Mfaransa William Saliba kutoka Saint-Etienne. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 sasa anaweza kutolewa kwa mkopo msimu ujao. ***(L'Equipe - in French)***

**MAUPAY, SEVILLA WATETA**

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Neal Maupay, 22, yupo katika mazungumzo na wakali wa La Liga, Sevilla. ***(L'Equipe - in French)***



## HABARI MICHEZO

# YANGA YAJICHELEWESHA UWANJA KWA MAKONDA

**Na Somoe Ng'itu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema ataikabidhi Yanga eneo la kujenga uwanja wa kisasa ifikapo Ijumaa baada ya viongozi wa klabu hiyo watakapokamilisha nyaraka muhimu zinazohitakija ili kukamilisha mchakato huo.

Makonda alitoa ahadi ya kuipa Yanga eneo la kujenga uwanja lililopo Kigamboni, katika harambee iliyoendeshwa na klabu hiyo Jumamosi iliyopita, ambapo pia zilikusanywa Sh. milioni 920, ikiwa ni fedha taslimu na ahadi kutoka kwa viongozi waliohudhuria na wanachama mbalimbali wa klabu hiyo.

Akizungumza jana jijini, Makonda, aliitaja nyaraka mojawapo ambayo bado haijakabidhiwa kuwa ni katiba ya klabu pamoja na cheti cha usajili.

"Eneo limepatikana, na leo kama mlivyoona, nimekutana na viongozi wao ambao wamenikabidhi baadhi ya nyaraka, wamewasilisha asilimia 75 ya nyaraka ambazo watakiwa kuzitoa ili kuandikishwa kiwanja hicho," alisema Makonda.

Aliongeza kuwa anaamini mchango huo utasaidia kuiweka klabu yao katika ramani nyingine na vile vile wataitumia kujiendeleza kama zilivyo timu nyingine za ndani na nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, alisema jana kuwa wanamshukuru kiongozi huyo kwa kuwapa kiwanja hicho, na chini ya uongozi wake, watakitendea haki.

Msolla alisema kwamba watalitumia eneo hilo kwa kufanya malengo yaliyoelekezwa na si kitu kingine.

"Hatutamwangusha kiongozi wetu, tutalitendea haki, tayari eneo hilo limeshakuwa katika mipango ya maendeleo ya klabu," Msolla alisema.

Aliongeza kuwa bado anawashukuru mashabiki wa Yanga wanaoendelea kuichangia klabu yao na kuelekeza kwamba mchakato huo ni endelevu.

**WA AFCON 2019...**




Washindi watatu wa droo ya kwanza ya Promosheni ya Tigo ya 'Soka la Afrika', Rehema Liku (kushoto), Geofrey Mutta (wa pili kushoto) na Kalaghe Rashid wakiwa wenye nyuso za furaha baada ya kukabidhiwa tiketi zao, na mtaalamu wa huduma za ziada wa kampuni hiyo, Ikunda Ngowi (wa pili kulia), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kwenda kushuhudia fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri. **PICHA: JOHN BADI**

# Azam kambini kujiwinda Kagame Cup

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC, kinatarajia kuingia kambini leo kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame ambayo yatafanyika kuanzia Julai 7 hadi 21, mwaka huu jijini Kigali, Rwanda, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema kuwa kikosi hicho kitaanza mazoezi kikiwa chini ya kocha wake mpya Mrundi Etienne Ndayiragije.

Iddi alisema kuwa programu na maandalizi yote ya timu hiyo yatafanyika chini ya usimamizi wa Ndayiragije ambaye ametua klabuni hapo kurithi mikoba iliyoachwa na Mholanzi Hans van der Pluijm.

**"Tunaanza mazoezi kama tulivyosema, sisi ndio ma bingwa mara mbili mfululizo wa mashindano ya Kombe la Kagame, tunajua kwamba si mashindano mepesi, la zima tujipange ili tukatetee kombe hili na hatimaye kubakia mikononi mwetu," alisema kiongozi huyo.**

Aliongeza kuwa wataanza kambi hiyo bila nyota wake watano ambao wako kwenye timu za Taifa mbalimbali, na watakapomaliza majukumu yao, wataungana na wenzao kwenye kambi hiyo.

"Ni utaratibu tu, tunajua wachezaji ni mali ya klabu, lakini ni fahari kuona wachezaji wako wanaitwa na mataifa yao, watarejea baada ya kumaliza majukumu yao," alisema Idd.

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba pamoja na watani zao, Yanga wameshatangaza kujitoa kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), wakitoa sababu mbalimbali.

## Yosso Simba, Yanga watinga nusu fainali

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU za vijana za umri chini ya miaka 20 za Simba B na Yanga B, zimefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya umri huo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Simba B ndiyo ilikuwa ya mwisho kutinga hatua hiyo baada ya juzi usiku kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya yosso wenzao kutoka Kagera Sugar.

Mchezo huo ulikuwa na ushindani muda wote, licha ya kikosi cha Simba B kwenda mapumziko kikiwa mbele kwa mabao 3-0.

Timu nyingine zilizotinga hatua hiyo ni Azam U-20 na Mtibwa Sugar U-20.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa jana jioni kila timu itajua mpinzani wake katika hatua hiyo ya nusu fainali ambayo itachezwa leo.

"Tutawatangazia nani anacheza na nani, ni suala la kiufundi baada ya kumalizika kwa hatua ya nane bora," alisema Ndimbo.

Aliongeza kuwa pia, mashindano ya umri chini ya miaka 15, yanaendelea vyema katika viwanja vyote vitatu hapa nchini, na wanawapongeza wachezaji kwa kuonyesha uwezo licha ya kucheza mechi asubuhi na mchana.

## Chiba FC, Lion Kids hakuna mbabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Chiba FC na Lion Kids zimeshindwa kutambiana baada ya kutoka sare tasa katika mwendelezo wa michuono ya Ndondo inayojulikana kama Kipwida Cup inayoendelea katika Uwanja wa Maungani.

Akizungumzia mchezo huo Kocha wa timu ya Chiba FC, Ali Juma alisema timu yake ilishindwa kutumia nafasi walizopata na kusababisha kupoteza nafasi nyingi za wazi. Alisema upungufu huo ataufanyia kazi katika mchezo unaofuata ambao wanakutana na timu ya Nyamanzi hapo kesho.

Kwa upande wake kwa timu ya Lion Kids, Mwinyi Shego alisema licha ya timu yake kutawala mchezo katika dakika zote, makosa madogo madogo katika safu ya ushambuliaji yalisababisha kushindwa kuzifumania nyavu za wapinzani wao.

Alisema kwa ujumla mchezo ulikuwa mzuri licha ya mapungufu madogo yaliyopo kwa washambuliaji, hivyo mchezo unaofuata atahakikisha washambuliaji wanatulia na kucheza kwa akili ili waweze kupata mabao.

Michuano hiyo ya Ndoto Kipwida Cup kwa mwaka huu imeshirikisha jumla ya timu 20.

# Michezo

Jumanne Juni 18, 2019

Nipashe




## Abramovich amhakikishia Lampard ukocha Chelsea

HABARI UK 29

LA TATU HILO...



Kipa wa Ecuador, Alexander Dominguez (chini), akishindwa kuamini kilichotokea baada ya Luis Suarez nyuma yake kumzidi maarifa na kuifungia Uruguay bao la tatu wakati wakishinda 4-0 juzi, kwenye mechi ya Kundi C ya michuano ya Copa America ambayo Edinson Cavani pia alitupia mabao mawili. **PICHA: MTANDAO**

# KAGERE SASA WA MABILIONI SIMBA

## ●●● Zamalek yategwa baada ya kuamua kuanguka wino miaka miwili Msimbazi, uongozi wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameonyesha kuwa na jeuri ya fedha baada ya kufanikiwa kumwongeza mkataba mpya mshambuliaji wake, Meddie Kagere, na "kuzika" ndoto za Zamalek ya Misri kumnasa Mnyarwanda huyo.

Kagere, ambaye mkataba wake wa awali ulikuwa unamalizika Juni mwakani, sasa ataendelea kukaa kwa Wekundu wa Msimbazi hao kwa misimu mingine miwili.

Hata hivyo, chanzo chetu ndani ya Simba kimeliambia Nipashe kuwa uamuzi wa kumapa Kagere mkataba wa miaka miwili zaidi ni kutokana na idadi kubwa kuanza kuisaka saini yake. Mbali na Zamalek, imeelezwa pia Al Ahly nayo inavutiwa na mshambuliaji huyo aliyemaliza msimu wa Ligi Kuu Bara akibeba Kiatu cha Dhahabu baada ya kutupia mabao 23.

Hatua hiyo, imeifanya Simba ambayo sera zake mara zote ni kutoa fursa kwa wachezaji wanaopata dili nono nje ya nchi, kumpa mkataba mapema ili kutega mamilioni kwa klabu itakayoonyesha kupagawa zaidi na huduma ya Mnyarwanda huyo.



Aidha, Simba imesema kuwa ofa ya kumuuza Kagere kwa thamani ya Sh. bilioni 1.2 kutoka kwa Waarabu hao, halijawahi kufika rasmi katika klabu yao.

"Mchezaji Bora na Mfungaji Bora wa Mwaka, Meddie Kagere, ataendelea kuwa nasi tena kwa misimu miwili ijayo, huyu ni hazina kwetu na bado yupo sana kwa machampioni," ilisema taarifa iliyotolewa na Simba jana.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa klabu yao itaendelea kusajili wachezaji wenye uwezo ambao wataisaidia kutimiza malengo yao.

"Mchezaji wa kigeni atakayesajiliwa Simba ni lazima awe na uwezo kuliko waliopo, hayo ndiyo malengo yetu, kama ni mshambuliaji, basi awe ni zaidi ya Kagere, Bocco au Okwi, huo ndio mtazamo wetu," alisema Manara. Naye Meneja wa Kagere, Patrick Gakumba, aliweka wazi kwamba Simba ndiyo ilimkataa mshambuliaji, Juma Balinya ambaye amesajiliwa na Yanga baada ya kueleza hataweza kufikia malengo wanayoyahitaji.

## Stars yatafutiwa Sh. bilioni moja

**Na Somoe Ng'itu**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya kuanza kwa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) Misri 2019, serikali imewaomba wadau wa michezo nchini kuichangia timu ya Taifa (Taifa Stars), kiasi cha Sh. bilioni moja ili kutoa motisha kwa wachezaji wa kikosi hicho, imeelezwa.

Taifa Stars itaanza kurusha karata yake ya kwanza katika fainali hizo Jumapili kwa kuwavaa Senegal, halafu itakutana na majirani zao, Kenya na itamaliza mechi za hatua ya makundi kwa kupambana na Algeria Julai Mosi, mwaka huu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema wachezaji wao tayari wako Misri lakini ili waweze kuwa na ari na morali ya juu, wanatakiwa kupewa motisha kama ambavyo wapinzani wao wanavyoahidiwa. "Wako Misri kwa ajili ya kupigania vita ya ubingwa wa Afrika, kuna vita ya ndani na nje ya uwanja, nchi nyingi zimekuwa zikijiandaa kwa mbinu tofauti, ila vita vingine ni vita vya kisaikolojia," alisema Waziri Mwakyembe.

Aliitaja akaunti ya Benki ya NBC, ambayo wananchi watachangia kuwa ni 0111010009781 ambayo ni ya Sports Development Fund iliyofunguliwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) au CRDB akaunti namba 01J0119996700 ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF). Kiongozi huyo aliendelea kuwashukuru Watanzania kwa kuiunga mkono Taifa Stars kuanzia wakati inasaka tiketi za kushiriki fainali hizo na mpaka sasa ilipo Misri ikisubiri kuanza kwa mashindano hayo.

"Tuma chochote ulicho nacho, na ukishatuma, andika ujumbe mfupi katika namba 0735 414043, itaonyesha jina la Oscar Zablon, kwa ajili ya kuweka rekodi na baadaye tutawatambua kwa mchango wao," alisema Mwakyembe.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars, Paul Makonda, alisema Jumamosi kutakuwa na sala maalumu kwa ajili ya kuiombea timu hiyo ili ifanye vizuri katika mechi yake ya kwanza na michezo mingine itakayofuata.

"Maandalizi yapo, nguvu ya fedha ipo, lakini mkono wa Mungu, hauepukiki, hii itawasaidia wawe na ujasiri wa kuwajibu wapinzani wao," alisema Makonda. Alizikumbusha kampuni na taasisi 41 ambazo ziliahidi kuichangia timu hiyo, kuwasilisha michango yao katika akaunti hizo kwa sababu muda wa kufanya hivyo umefika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >